

**KUTOJITOKENZA KWA LUGHA YA KITAMATHALI NA UREJELEAJI WA  
KIJINSIA KATIKA *WIMBO ULIO BORA***

**MARIGA EDWARD**

**TASNIFU HII IMETOLEWA KWA MADHUMUNI YA KUTOSHELEZA BAADHI  
YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI**

**CHUO KIKUU CHA NAIROBI**

**2019**

## **UNGAMO**

### **MTAHINIWA**

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kutolewa katika chuo kikuu chochote kwa madhumuni ya kutosheleza mahitaji ya shahada yoyote.

Sahihi ..... Tarehe .....

### **MARIGA EDWARD**

C50/80169/2015

### **WASIMAMIZI**

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu tuliotolewa kama wasimamizi wa kazi hii katika chuo kikuu cha Nairobi.

Sahihi ..... Tarehe .....

### **DKT. OMBOGA ZAJA**

Sahihi ..... Tarehe .....

### **DKT. HANAH MWALIWA**

## **TABARUKU**

Kazi hii naitabarukia mke wangu Aphline kwa kunihimiza kuendelea na kazi hii kila nilipoonyesha kutamauka. Ulikuwa nguzo imara wakati wa kufanya utafiti na hata wa kuiandika tasnifu hii. Ubarikiwe kwa msaada wako ambao ulikuwa bila kifani na pia johari kwangu katika safari hii.

## SHUKRANI

Kufanikiwa kwa kazi hii kulitokana na wahusika mbalimbali kutoa michango tofauti tofauti ambayo ilikuwa johari kuu kwangu na kwa sababu hiyo wanastahili shukrani tele. Kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema katika kipindi kizima cha kutafiti na hata kuiandika kazi hii. Pamoja na haya, ninamshukuru Mungu kwa kunipa ukakamavu wa kustahimili changamoto mbalimbali na kunifikisha mwisho wa safari hii.

Aidha nawashukuru wasimamizi wangu Dkt. Zaja Omboga na Dkt. Hanah Mwaliwa. Ushauri wenu wa kitaalamu ulikuwa kiunzi muhimu katika kufaulu kwa kazi hii. Mlikuwapo kunipa mawaidha ya kiusomi kila nilipowahitaji. Mtagusano wangu nanyi ulinipa mwelekeo wa kiusomi na kunipa pia ari ya kutafiti zaidi. Kwa kunifaa kiasi hiki, Mungu awabariki sana.

Vilevile, ninawashukuru wahadhiri wangu walionifaa katika kozi mbalimbali katika masomo yangu ya uzamili. Wahadhiri hawa ni pamoja na Dkt. Zaja Omboga, Prof. Rayya Timammy, Prof. Iribe Mwangi, Prof. John Habwe, Prof. Kineene wa Mutiso, Prof. Mwenda Mbatiah, Prof. Mbuthia, Dkt. Jefwa Mweri, Dkt. Jerono, Dkt. Mukhwana, Mwalimu Mary Ndung'u na Mwalimu Leonard Sanja. Mungu awape afya mzidi kuwafaa wengine pia.

Kundi lingine la kushukuru ni wanafunzi wenzangu wa uzamili. Nawashukuru kwa kunitia moyo pamoja na ushauri wenu uliokuwa wa manufaa kwangu. Wanafunzi hawa ni pamoja na Irene Kilingo, Christine Oyaro, Gloria, Ronald Aloo na Cyrus Moindi. Baraka za Mola ziwe juu yenu daima.

Mwisho nawashukuru rafiki zangu Davi Were na Kelvin Ogelo. Msaada wenu wa kiurafiki ulinipa msukumu zaidi wa kutaka kukamilisha kazi hii. Mawaidha yenu ya busara mliyonipa kila mara yalinipa motisha ya kuzikabili changamoto zilizoandamana na safari hii. Mungu awabariki.

## IKISIRI

Utafiti huu ulilenga kuchunguza kutojitokeza kwa lugha ya kitamathali na urejeleaji wa kijinsia katika *Wimbo Ulio Bora* kama matini lengwa, matini hii inapolinganishwa na matini chanzi *Song of Songs*. Kitabu hiki ni cha ishirini na mbili katika agano la kale kwa mujibu wa tafsiri ya King James Version. Katika utafiti huu, tamathali tulizojikita kwazo ni pamoja na tashbihi, sitiari pamoja na tashihisi. Tulibainisha tamathali hizi katika matini chanzi na vilevile jinsi ambavyo tamathali hizi zilivyohawilishwa katika matini lengwa. Jambo lingine ambalo tuliliangazia ni lugha inayorejelea jinsia ya kiume na ya kike katika matini chasili huku tukilinganisha na matini lengwa kwa lengo la kubaini ulinganifu katika kujitokeza kwa urejeleaji huo wa kijinsia. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Newmark (1988) ya tafsiri ya masuala mahususi ya kitamaduni. Tuliangalia makundi matano ya masuala mahususi ya kitamaduni yanayopendekezwa na nadharia hii. Pamoja na kufanya hivi, tulichunguza jinsi masuala haya mahususi yanavyojitokeza katika matini lengwa kwa kuilinganisha matini hiyo na matini chasili. Utafiti tuliufanya ulikuwa wa maktabani kwa kuwa data tuliyokusanya ilikuwa data isiyo msingi ambapo tulitegemea habari zilizohifadhiwa kwa njia ya maandishi katika bibilia ya Kiingereza (tafsiri ya King James) na tafsiri yake katika lugha ya Kiswahili (Swahili Union Version). Matokeo ya utafiti huu yamedhihirisha masuala mbalimbali ya kitafsiri. Kwanza ni kwamba, lugha ya Kiingereza kupitia matini chanzi *Song of Songs* inadhihirisha urejeleaji wa kijinsia. Urejeleaji huu umejitokeza katika vitengo mbalimbali kama vile nomino, virai nomino, vivumishi pamoja na viwakilishi. Lugha ya Kiswahili kupitia kwa matini chanzi *Wimbo Ulio Bora* hata hivyo, inadhihirisha kwa kiasi kidogo tu urejeleaji huu wa kijinsia. Aidha utafiti huu vilevile ulizichunguza tamathali tatu husika (tashihisi, tashbihi na sitiari) kwa kutathmini kujitokeza kwa tamathali hizi katika matini lengwa ambapo matokea yalionyesha kuwa tamathali hizi zimekosa ulinganifu kwa kiasi kikubwa matini mbili husika zinapolinganishwa. Aidha, tulitafitia masuala mahususi ya kitamaduni kwa kuyagawa katika makundi yake matano kama anavyopenekeza Newmark (1988) na kisha kuchunguza mikakati iliyotumika katika kuyahawilisha masuala haya hadi lugha lengwa. Utafiti huu umebainisha kwamba kutojitokeza kwa lugha inayorejelea jinsia, ukosefu wa ulinganifu wa kitamathali na kidhana kunatokana na tofauti kati ya lugha mbili husika ambapo tamaduni zinazoambatana na lugha husika (Kiswahili na Kiingereza) zinadhihirisha mielekeo tofauti katika kuyadhihirisha masuala ya kijinsia, kitamathali na kidhana.

## YALIYOMO

<b>UNGAMO</b> .....	ii
<b>TABARUKU</b> .....	iii
<b>SHUKRANI</b> .....	iv
<b>IKISIRI</b> .....	v
<b>VIFUPISHO VYA MANENO</b> .....	ix
<b>SURA YA KWANZA</b> .....	1
<b>UTANGULIZI</b> .....	1
1.0 Usuli Wa Mada .....	1
1.2 Tatizo la Utafiti .....	5
1.3 Maswali ya Utafiti .....	6
1.4 Madhumuni ya Utafiti .....	6
1.5 Sababu za Kuteua Mada hii .....	7
1.6 Upeo na Mipaka .....	8
1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada .....	8
1.8 Msingi wa Nadharia .....	14
1.8.1 Dhana ya utamaduni .....	16
1.8.2 Dhana ya Masuala Mahususi ya Kitamaduni .....	17
1.8.3 Migao ya Masuala Mahususi ya Kitamaduni .....	18
1.8.4 Mikakati ya Kutafsiri masuala mahususi ya kitamaduni .....	21
1.9 Mbinu ya Utafiti .....	26
1.9.1 Uteuzi wa Sampuli .....	26
1.9.2 Mbinu za ukusanyaji data .....	26
1.9.3 Uchanganuzi na uwasilishaji wa data .....	27
<b>SURA YA PILI</b> .....	28
<b>UJIELEZAJI WA KIJINSIA KATIKA SONG OF SONGS</b> .....	28
2.0 Utangulizi .....	28
2.1 Nomino za kawaida .....	28
2.1.1 Wanyama .....	28
2.1.2 Binadamu .....	30
2.2 Virai nomino .....	34
2.3 Viwakilishi .....	39
2.3.1 Viwakilishi vya nafsi .....	39
2.3.2 Viwakilishi vimilikishi .....	45

2.4 Vivumishi vinavyoashiria jinsia.....	49
2.5 Mahitimisho .....	49
<b>SURA YA TATU.....</b>	<b>51</b>
<b>ULINGANIFU WA KITAMATHALI KATIKA SONG OF SONGS NA WIMBO</b>	
<b>ULIO BORA.....</b>	<b>51</b>
3.0 Utangulizi .....	51
3.1 Tashihisi, Tashbihi na Sitiari.....	52
3.1.1 Tashbihi .....	52
3.1.2 Sitiari .....	53
3.1.3 Tashihisi.....	55
3.2 Tashbihi, tashihisi na sitiari katika Song of Songs na Wimbo UlioBora.....	56
3.2.1 Tashbihi .....	56
3.2.2 Sitiari .....	67
3.2.3 Tashihisi.....	70
3.3 Mahitimisho .....	75
<b>SURA YA NNE .....</b>	<b>77</b>
<b>MASUALA MAHUSUSI YA KITAMADUNI.....</b>	<b>77</b>
4.0 Utangulizi .....	77
4.1 Ikolojia .....	78
4.1.1 Wanyama na ndege.....	78
4.1.2 Mimea.....	81
4.1.3 Pepo .....	83
4.1.4 Milima .....	84
4.1.5 Mashamba.....	85
4.1.6 Mabonde .....	86
4.1.7 Chemchemi na vijito vya maji.....	86
4.2 Vifaa vya kitamaduni .....	87
4.3 Utamaduni wa asasi na taasisi za kijamii .....	93
4.4 Utamaduni wa kazi na burudani .....	94
4.5 Utamaduni wa ishara na tabia .....	96
4.6 Mahitimisho .....	97

<b>SURA YA TANO</b> .....	99
<b>HITIMISHO NA MAPENDEKEZO</b> .....	99
5.0 Utangulizi .....	99
5.1 Hitimisho .....	99
5.2 Mapendekezo .....	101
<b>MAREJELEO</b> .....	103



## **VIFUPISHO VYA MANENO**

<b>LL</b>	Lugha Lengwa
<b>LC</b>	Lugha Chanzi
<b>HL</b>	Hadhira Lengwa
<b>ML</b>	Matini Lengwa
<b>MC</b>	Matini Chanzi
<b>UC</b>	Utamaduni Chanzi
<b>UL</b>	Utamaduni Lengwa
<b>ML</b>	Msomaji Lengwa
<b>TY</b>	Tafsiri Yetu
<b>KHJ</b>	Kama Hapo Juu
<b>n.k</b>	na kadhhalika

## SURA YA KWANZA

### UTANGULIZI

#### 1.0 USULI WA MADA

*Song of Songs* ni kitabu cha ishirini na mbili katika Agano la Kale (mgao wa kwanza kati ya miwili ya Biblia). Kitabu hiki kina sura nane na mistari 117 kwa mujibu wa Tafsiri ya **King James Version**. Kitabu hiki cha *Song of Songs* ni kitabu ambacho kinajumuisha mashairi mengi yanayowasilishwa na wahusika watatu au sauti husika za aina tatu; sauti ya mwanamke, sauti ya mwanamume na sauti ya wahusika kundi (Mabinti wa Yerusalemu). Hali hii ya wahusika hawa kuwasilisha usemi wakipishana zamu, inalifanya shairi hili kuwa shairi la kimaigizo au shairi la kiutendaji. Makundi haya matatu ya wahusika katika kitabu hiki yanawasilisha masuala tofauti kuhusu wahusika wa jinsia ya kike au wale wa jinsia wa kiume na hivyo hakuna mtiririko maalumu wa vitushi katika kitabu hiki, kilichoko ni msambao mpana wa kusifiana kati ya makundi haya na kwa njia hiyo kunaibuka lugha iliyo na mwelekeo mahususi wa utambulishaji na ujielezaji wa kijinsia.

Kitabu hiki ni kusanyiko la mashairi yaliyopangwa kama mazungumzo kati ya mwanamwali na mpenziwe wa kiume. Mhusika wa tatu au korasi (Mabinti wa Yerusalemu) mara kwa mara anawazungumzia wapenzi hawa kwa njia ya kujaliza na kuendeleza ujitokezaji wa sifa za wahusika wawili wa kimsingi. Shairi la kwanza linawasilishwa na mwanamwali ambaye anatamani kuwa karibu na mpenziwe na kufurahia mabusu yake. Anaelezea kuwa rangi ya ngozi yake ni nyeusi kwa sababu familia yake inamtuma kufanya kazi kwenye shamba la mzabibu. Anamtafuta mpenziwe kwa juhudi kuu na kumlinganisha na mchungaji anayetanga. Kufikia hapa, Mabinti wa Yerusalemu (korasi) wanamhimiza kufuata mifugo (mpenziwe) mpaka kwenye hema yake.

Wapenzi hawa wanalala pamoja kwenye mkeka ambapo mhusika Mwanamume anapata fursa kuusifu urembo wa mpenziwe akimlinganisha na paa huku akilinganisha macho yake na macho ya njiwa. Pamoja na haya, mpenzi huyu wa kiume anaeleza juu ya mazingira ya kijani kibichi yanayovutia na yaliyo na rutuba. Mwanamwali naye anajirejelea kwa kumlinganisha na ua la waridi na lililofunikwa na kivuli cha mpenziwe ambaye ni mti wa matunda. Anamlinganisha mpenziwe na paa anayewasili kumchukua wakati mimea inapochanua. Mwanamwali huyu

anajivunia kuwa mpenziwe sasa anachunga zizi lake la kondoo katikati ya ua lake. Pamoja na haya, anawaonya wanawake wengine (Mabinti wa Yerusalemu) wasiyachochee mapenzi.

Mwanamwali huyu anaona kwenye ndoto kuwa anamtafuta mpenziwe kwenye barabara za miji na kwamba anapompata, anamchukua na kumpeleka nyumbani. Anatazamia harusi ya kifahari ambapo mpenziwe bwana harusi aliye na furaha tele anajitokeza kama mfalme Suleimani. Bwana harusi kufikia hapa anazungumza akivilinganisha viungo mbalimabli vya mwili wa mpenziwe na wanyama wapendwao wenye tija, lakini pia anavilinganisha viungo vya mpenzi wake na vito vya madini ya thamani. Bwana harusi anamwita mpenziwe ashuke kutoka kwenye vilele vya milima ili awe naye. Kwa matamano makuu, mwanamume anamrejelea mwanamwali kama bustani iliyofungwa yenye majani mengi. Mwanamwali anaagiza upepo kuvuma juu ya bustani yake na kisha kumwalika penziwe katika bustani hilo. Mwanamume anakula kwenye bustani na kisha kuwaalika marafiki zake kusherehekea pamoja naye. Katika ndoto nyingine, mwanamwali huyu anamsikia mpenziwe akibisha kwenye mlango usiku wa manane lakini anatoweka. Tena anazunguka kwenye mitaa ya miji kumtafuta mpenziwe lakini wakati huu, walinzi wa mji wanamjia. Anawauliza Mabinti wa Yerusalemu wamsaidie kumpata mpenziwe. Mabinti hawa wanamuuliza kutoa wasifu wa kimaumbile wa mwanamume huyo. Analijibu swali hili kwa kuvilinganisha viungo vya mwili wa mpenzi wake na madini ya thamani na wanyama.

Wapenzi hawa wawili wanapatana kwenye bustani ambapo mwanamume huyu anaendelea kukisifu kila kiungo cha mwili wa mpenziwe. Anamuuliza mwanamwali wake acheze densi na kumlinganisha na mtende na matiti yake kusifiwa kama matunda ya thamani yanayoenziwa. Mwanamwali anamwalika mpenziwe waende mashambani na vijijini kwa ahadi kuwa atampa mapenzi yake katikati ya mashamba ya mizabibu inayochanua. Mwanamwali huyu anatamani kuwa mwanamume huyu angekuwa nduguye wa kiume kwa kuwa watu hawangezugumzia hali yao ya kuonyesha mapenzi yao hadharani. Anamwambia mwanamume huyu atie muhuri kwenye moyo wake kwa mapenzi yake kwa maana mapenzi yana nguvu.

Pamoja na maelezo hayo mafupi juu ya yale yanayojiri katika kitabu hiki, kitabu hiki cha *Song of Songs* kimepata ufasiri wa aina mbalimbali. Fasiri hizi ni pamoja na fasiri ya kidini, kitafsiri na kifasihi miongoni mwa fasiri nyingine. Katika fasiri ya kidini, kitabu hiki kinachukuliwa kuwa ni istiaara ya uhusiano kati ya Mungu na Waisraeli. Miongoni mwa Wakristo, kitabu hiki kinachukuliwa kuakisi uhusiano kati ya Kristo na kanisa. Fasiri nyingine ni ya kifasihi ambayo

inakiona kitabu hiki kama mkusanyiko wa mashairi ya kimapenzi yanayodokeza mahusiano ya kibinadamu. Kwa mujibu wa mwelekeo huu, kitabu hiki kinachukuliwa kama shairi la kimaigizo. Hii ni kwa sababu wahusika wake wanagawika katika makundi matatu dhahiri ambayo ni pamoja na mhusika wa kike, mhusika wa kiume na mhusika kundi (Mabinti wa Yerusalemu). Katika uigizaji huu, kuna sehemu zinazozungumzwa na mwanamke, zile zinazozungumzwa na mwanamume na sehemu za mhusika kundi.

Katika fasiri ya kitafsiri, kitabu hiki kinaangaliwa kwa misingi ya dhana zinazopatikana ndani mwake. Dhana hizi zinajumuisha dhana za kimazingira, kimahusiano, kiutamaduni na dhana za kijamii miongoni mwa dhana nyingine. Fasiri hii imeegemezwa kwenye misingi kwamba dhana hizi zinazopatikana katika lugha chanzi zikihawilishwa katika lugha lengwa, huweza kuibua masuala fulanifulani ya kifasihi na kitafsiri. Ntarangwi (2004) anasema, “Kazi ya uhakiki haifanyiki kisdafa tu bali huwa imepangwa kutokea.” Anaongeza kwamba, “Kile anachokisema mhakiki kuhusu kazi yoyote ya fasihi hutegemea kwa kiwango kikubwa mtizamo wa kihakiki anaoufuata.” Hivi ni kumaanisha kwamba uhakiki huanza kwa maoni ya msomaji (mhakiki) kuhusu kazi anayoizingatia. Tunakubaliana na maoni haya kuwa uhakiki unashawishiwa na mwelekeo au msimamo wa kihakiki wa mhakiki wa kazi husika. Kwa hivyo na kwa misingi hiyo, katika utafiti huu, tutachunguza na kukichanganua kitabu cha *Song of Songs* kwa misingi ya mielekeo ya kifasihi na kitafsiri.

Kifasihi, tutajikita katika kudadavua wahusika waliomo katika kitabu hiki hasa kwa kumakinikia maelezo wanayotoa kujirejelea na hata kuwarejelea wahusika wengine. Hii ni kwa sababu, katika mazungumzo haya ya kujirejelea na kuwarejelea wahusika wengine katika mashairi haya, kunaibuka lugha ya kitamathali inayojumuisha jazanda, tashbihi, uhuishi na sitiari miongoni mwa tamathali nyingine. Tamathali hizi, ambazo zinaakisi zaidi uhalisia wa maisha ya sehemu za nyanjani, zimechota pakubwa katika mazingira hayo ya kishamba ambapo yamedhihirisha maswala ya ikolojia, kwa mfano kunadhihirika lugha na tamathali zinazohusu mimea, matunda, wanyama, miti ya matunda mahususi, na kwa upande mwingine kuna lugha inayohusiana na mambo ya kimaumbile kama vile milima na mabonde, konde na sehemu za malisho, pepo na mizimu. Udhihirikaji wa mambo haya ya kiikolojia ni suala tata katika michakato ya kutafsiri, kwa hivyo katika uchanganuzi wetu, tutazingatia mwelekeo wa kifasihi ambapo tutajikita mwanzo katika kuichanganua matini chasili *Song of Songs* kwa lengo la kutaka kuonyesha uibukaji wa lugha ya kitamathali, mahusiano ya lugha hiyo na miktadha ya kiutamaduni, pamoja na ujitokezaji wa lugha hiyo kuashiria uana/ujinsia wa

wahusika. Kwa upande wa pili tutaangalia na kuchanganua kiulinganishaji *Wimbo Ulio Bora* ambayo ndiyo tafsiri ya *Song of Songs* katika lugha ya Kiswahili. Ili kufanya hivyo, tutajikita kwenye dhana au masuala mahususi ya kitamaduni na jinsi ambavyo masuala hayo yamehawilishwa hadi lugha lengwa (Kiswahili). Kitafsiri, tutamakinikia dhana au masuala mahususi ya kitamaduni yanayojitokeza katika matini chasili *Song of Songs* na tafsiri yake katika lugha ya Kiswahili *Wimbo Ulio Bora* ili kubaini jinsi masuala haya yalivyohawilishwa hadi lugha lengwa na kupambanua kama kuna ruwaza fulani inayodhihirika katika uhawilishaji huu.

Kwa kukiangalia kitabu cha *Song of Songs* kwa misingi ya mielekeo ya kifasihi na kitafsiri, kitabu hiki kinadhihirisha upekee fulani unaohusiana na lugha ya kitamathali ambao unachochea kufanyiwa utafiti ili kubaini masuala mengi ya kifasihi na kitafsiri. Hii ni kwa sababu kitabu hiki kinadhihirisha mwegemeo mkubwa wa ufasiri wa kifasihi japo ni matini ya kidini na hili ni jambo mojawapo linalotushawishi kuifanyia matini hii utafiti wa kifasihi. Upekee huu unatokana na uwepo wa ithibati wa matini hii kuibua mijadala ya aina mbalimbali ikiwemo mijadala ya masuala ya kifeministi, masuala ya ubabedume na masuala ya utabaka, hasa ikizingatiwa kwamba huyu mwanamwali na kipenzi chake wana wasifu wa kishamba tofauti na Binti Yerusalem aliye na wasifu wa kimji. Yana (2018) anasema kuwa jazanda inachukuliwa kama mojawapo ya matatizo yenye ugumu wa kuhawilishwa katika michakato ya tafsiri. Hii ni kwa sababu tamathali hizi aghalabu huhusishwa na kutowiana kwa njia nyingi katika lugha mbili husika. Aidha tamathali hizi zinaathiriwa na utamaduni. Maoni haya ya Yana yanaashiria kuwa tamathali huwa na upekee au umahususi wa kiutamaduni ambao unapohawilishwa kutoka lugha moja hadi nyingine unastahili kutiliwa maanani. Hii ndiyo sababu tumekusudia kuchunguza jinsi ambavyo masuala mahususi ya kitamaduni yalivyotafsiriwa kutoka lugha ya Kiingereza hadi lugha ya Kiswahili katika *Song of Songs* na tafsiri yake katika lugha ya Kiswahili, *Wimbo Ulio Bora*. Katika utafiti huu, tutaongozwa na nadharia ya Newmark ya tafsiri ya maswala mahususi ya kitamaduni.

Sababu kuu ya kukifanyia kitabu cha *Song of Songs* utafiti wa kiutamaduni ni kuwa, kazi yetu inahusu kuzibainisha na kuzichanganua urejeleaji wa kijinsia pamoja tashihisi, sitiari na tashbihi zinazodhihirisha sifa za upekee wa kitamaduni. Katika misingi hii, kitabu hiki kinadhihirisha masuala mengi mahususi ya kitamaduni ambayo tunaamini yatatusaidia kuafikia malengo ya utafiti wetu kwa kutupa data itakayoibua mijadala ya kiusomi inayohusiana na tafsiri za dhana za kitamaduni kwa upande mmoja na kwa upande wa pili

mijadala inayohusiana na lugha inayojibainisha katika misingi ya uashiraji wa kijinsia. Aidha, tutaongozwa na nadharia ya Newmark (1988) ya masuala mahususi ya kitamaduni ili kubaini ni mikakati gani miongoni mwa ile mikakati anayopendekeza Newmark (1988) ilikuwa muhimu katika kutafsiri masuala mahususi ya kitamaduni ili kupata tafsiri ya *Wimbo Ulio Bora* na kufanya tafsiri hii kueleweka kwa wasomaji wa lugha lengwa. Aidha, usomaji wetu umedhihirisha kuwa kuna ithibati kuwa katika kutafsiri *Song of Songs* hadi *Wimbo Ulio Bora* mtafsiri ametumia mikakati mbalimbali ya tafsiri alivyopendekeza Newmark (1988). Data tutakayochunguza itahusisha tashbihi, sitiari na uhuishi kutoka kwa matini chanzi (*Song of Songs*) na data hiyo itachunguzwa kwa kulinganishwa na data sawia itakayochotwa kutoka tafsiri yake katika lugha ya Kiswahili (*Wimbo Ulio Bora*) ili kubaini ulinganifu na utojitokezaji wa masuala haya katika matini lengwa.

## 1.2 Tatizo la Utafiti

Utafiti huu ulikitwa katika usomaji na uchanganuzi wa fasihi tafsiri ambapo kimsingi katika utafiti huu tulijishugulisha kuonyesha changamoto zinazohusiana na uhawilishaji wa mambo matatu ya kimsingi katika michakato ya kutafsiriwa kwa *Song of Songs* kutoka Kiingereza hadi *Wimbo Ulio Bora* katika Kiswahili. Kwanza utafiti huu ulilenga kuonyesha kujitokeza au kutojitokezakwa lugha iliyo na uashiraji wa kijinsia katika *Wimbo Ulio Bora* ambayo ni tafsiri ya *Song of Song* matini hizi mbili zinapolinganisha. Pili, utafiti huu vilevile ulipanika kuonyesha changamoto zinazojitokeza katika kuhawilisha lugha ya kitamathali; tashihisi, sitiari na tashbihi kutoka utamaduni chanzi wa *Song of Songs* hadi utamaduni lengwa wa *Wimbo Ulio Bora*. Tatu, kwa kuwa tamathali zinazojitokeza katika *Song of Songs* zina mahusiano ya karibu na utamaduni pamoja na mazingira yaliyoshawi kuibuka kwao, kuna haja kuonyesha changamoto zinazohusiana na uhawilishaji wa dhana mahususi za kitamaduni kutoka lugha chanzi ya *Song of Songs* hadi lugha lengwa ya *Wimbo Ulio Bora*.

Utafiti huu ulichochea na uelewa wetu kwamba kutokana na kuwepo kwa tofauti miongoni mwa lugha mbalimbali, mifumo ya ujielezaji kijinsia, maana zinazoekezwa katika tamathali za lugha na uibukaji wa dhana mahususi za kijamii, hutofautiana kutoka lugha moja hadi nyingine. Tofauti hizi kati ya lugha tofauti hudhihirika katika fasihi yao na masuala mengine mahususi ya kitamaduni. Kwa sababu hii, kunatokea hali za utata na pengine hali za utohakika wa kimaana wakati masuala ya ujielezaji wa kijinsia, ubainikaji wa maana za kitamathali na ujitokezaji au utojitokezaji wa dhana unapotathminiwa katika miktadha lengwa. Hii inaweza kuwa na maana kwamba maana zilizopo katika lugha chanzi zinapohawilishwa hadi lugha

lengwa zinaweza kukosa kuibua uelewa sawia, zinaweza kuzua utata wa uelewa au kuibua changamoto sawia na hizo. Vinginevyo ni kwamba tofauti hizi za ujielezaji, maana za kitamathali na dhana mahususi za kitamaduni ambazo zinadhihirika kati ya lugha mbili tofauti huweza kusababisha muachano mkubwa kati ya matini chanzi na matini lengwa. Katika matini tulizozirejelea; *Song of Songs* kama matini chanzi na *Wimbo Ulio Bora* kama matini tafsiri, kuna ithibati inayoweza kutetewa ya kudhihirika kwa muachano mkubwa wa ujielezaji kijinsia, ulinganifu wa maana za kitamathali na kutojitokeza kwa dhana mahususi za kitamaduni. Muachano huu wa ujielezaji, tamathali na dhana ndio msingi wa tatizo letu la utafiti; kutojitokeza kwa lugha ya ujielezaji kijinsia, ulinganifu wa kitamathali na kidhana katika *Wimbo Ulio Bora* kama lugha lengwa kwa kurejelea *Song of Songs* kama kitovu cha lugha chanzi. Tulijitahidi kulichunguza na kulifanyia utafiti wa kina tatizo hili na kutoa mapendekezo amilifu ya jinsi ya kutafsiri mambo haya katika michakato ya tafsiri za kifasihi.

### 1.3 Maswali ya Utafiti

Kutokana na uchanganuzi wa awali wa kiulinganishi tuliofanya kwa kuzirejelea matini za *Song of Songs* na tafsiri yake katika lugha ya Kiswahili *Wimbo Ulio Bora*, ilibainika kwamba matini hizi zinadhihirisha muachano mkubwa wa ujielezaji kijinsia, ukosefu wa ulinganifu wa kitamathali na kutokujitokeza kwa dhana mahususi za kitamaduni kati ya matini chanzi na matini lengwa. Hii ina maana kwamba kuna mambo ambayo hayajitokezi katika matini lengwa, matini hizi mbili zinapolinganishwa. Swala hili la ukosefu na kutokujitokeza kwa mambo yanayotarajiwa yajitokeze ndilo linalochochea utafiti huu kutaka kujibu maswali yafuatayo;

- 1) Je, ni kwa kiasi gani ujielezaji wa kijinsia unaobainika katika *Song of Songs* unajitokeza katika *Wimbo Ulio Bora*?
- 2) Ni kwa kiasi gani inaweza kusemwa kwamba kuna ulinganifu wa kitamathali kati ya matini lengwa *Wimbo Ulio Bora* ikilinganishwa na matini chanzi ya *Song of Songs*?
- 3) Je, ni kwa kiasi gani uhawilishaji wa dhana mahususi za kitamaduni unajitokeza katika *Wimbo Ulio Bora* inapolinganishwa na matini chanzi *Song of Songs*?

### 1.4 Madhumuni ya Utafiti

Utafiti huu ulinua kutekeleza malengo yafuatayo;

- 1) Kuchunguza ili kubaini kujitokeza au kutojitokeza kwa lugha inayoashiria ujielezaji wa kijinsia katika *Wimbo Ulio Bora* ikilinganishwa na matini chanzi *Song of Songs*.

- 2) Kuchunguza ni kwa kiasi gani kuna kutojitokeza kwa ulinganifu wa kitamathali kati ya matini lengwa *Wimbo Ulio Bora* ikilinganishwa na matini chanzi ya *Song of Songs*.
- 3) Kubainisha changamoto zinazohusiana na uhawilishaji wa dhana mahususi za kitamaduni kati ya matini chanzi na matini lengwa.

### 1.5 Sababu za Kuteua Mada hii

Kitabu cha *Song of Songs* kinapoangaliwa na kuchanganuliwa kwa mwelekeo wa kifasihi, kunadhihirika masuala mahususi ya kifasihi na kitafsiri yanayohitaji kifanyiwa utafiti sio tu kwa nia ya kutaka kupata ufahamu wa kina wa kitabu hiki, bali pia kwa kutaka kuibua masuala mapana yanayohusiana na michakato ya kutafsiri masuala mahususi ya kifasihi na kitamaduni. Kwanza, kitabu hiki cha *Song of Songs* tofauti na vitabu vingine katika Biblia ya Kikristo kama inavyofahamika kwa sasa katika matoleo yake mbalimbali ya Biblia, kimedhihirisha uwepo wa msukumo mkubwa wa lugha ya kitamathali. Aidha kuna ujitokezaji mkubwa wa ujielezaji wa kijinsia hivi kwamba lugha ya kitabu hiki inapoangaliwa katika misingi ya kijinsia, jinsia ya kike inaonekana kupewa kipaumbele na kukuzwa zaidi tofauti na ilivyo katika sehemu nyingine ya Biblia. Hii ni kwa sababu, miongoni wahusika au sauti tatu zinazonena katika kitabu hiki; yaani, sauti ya kike, sauti ya kiume na sauti ya kundi, sauti ya kike inaonekana kutawala zaidi. Mhusika huyu wa kike anazungumza mara nyingi na hata kuwa wa kwanza kuanzisha maongezi mara nyingi. Pamoja na haya, sauti ya tatu (kundi) pia ni ya wahusika wa kike wanaorejelewa kama Mabinti wa Yerusalemu. Fauka ya haya, kwa sababu ya wahusika hawa kudhibiti sehemu kubwa ya maongezi, kunaibuka lugha iliyo na mwegemeo mkubwa wa ujielezaji wa kijinsia hasa pale mhusika huyu anapojirelea, anapomrejelea mpenzi wake wa kiume na anaporejelewa na mpenzi huyu wa kiume. Si ajabu kwamba neno mama limejitokeza mara saba katika wimbo huu huku mzazi wa kiume (baba) akikosa kutajwa kabisa katika kitabu kizima. Kwa hali mbalimbali ujielezaji huu ni suala la kimsingi katika changanuzi za kifasihi na kitafsiri na ujitokezaji wake katika matini inayostahili kuangaliwa kwa misingi ya kidini, unazua mijadala mingi ya kiusomi.

Pamoja na haya, tamathali zilizotumika zinaisawiri jinsia ya kike kwa njia iliyo kinyume na chukulizi za kifeministi kuhusu jinsia hii. Hii ni kwa sababu wimbo huu unasheheni tamathali zinazodhihirisha jinsia ya kike kuwa na nguvu na hata hatari. Tulichochea zaidi na msukumo huu mkubwa wa ujielezaji wa kijinsia na wa kitamathali katika wimbo huu na ndiposa tulijitwika jukumu la kuchunguza jinsi ambavyo tamathali hizi tatu zilivyotasiriwa kutoka lugha ya Kiingereza hadi lugha ya Kiswahili. Kimsingi, kitabu *Song of Songs* kinadhihirisha



mwachano mkubwa na tafsiri yake katika lugha ya Kiswahili *Wimbo Ulio Bora*. Casagrande (1954) anasema kuwa mtu hatafsiri lugha bali hutafsiri utamaduni pia. Hivi ni kumaanisha kuwa tafsiri ni shughuli yenye uchangamano kwani inahusu kuhawilisha utamaduni wa lugha moja hadi ule wa lugha nyingine. Kwa hivyo, utafiti wetu ulichochea na kutaka kujua ni kwa nini *Wimbo Ulio Bora* katika Biblia ya Kiswahili unadhihirisha mwachano mkubwa wa ujielezaji wa kijinsia, ukosefu wa ulinganifu wa kitamathali na kutojitokeza kwa dhana mahususi za kitamaduni inapolinganishwa na matini chanzi ya Biblia? Ni kwa sababu ya mwachano huu kati ya matini chanzi na matini lengwa katika misingi ya ujielezaji, ukosefu wa ulinganifu wa kitamathali na utojitokezaji wa dhana mahususi za kitamaduni ambapo tulichochea kufanya utafiti wa kina kuhusu ujitokezaji au utojitokezaji wa mambo haya katika *Wimbo Ulio Bora* kwa misingi ya Nadharia ya Newmark (1988) ya Tafsiri ya Masuala Mahususi ya Kitamaduni. Tunatumaini kuwa utafiti huu uliweza kuziba pengo muhimu la maarifa katika uwanja mzima wa tafsiri na hata kuchochea tafiti zaidi hasa kwa yale maswala ambayo hayajakushuhulikiwa katika kazi hii.

## **1.6 Upeo na Mipaka**

Utafiti huu utashughulikia na kuangazia mambo matatu ya kimsingi kuhusiana na tafsiri ya lugha ya *Wimbo Ulio Bora* kutoka Kiingereza hadi Kiswahili. Kwanza, utafiti huu utaangazia changamoto za kutafsiri ujielezaji wa kijinsia kwa kadri unavyobainika katika lugha moja na kudidimia katika lugha lengwa. Pili utaangalia ujitokezaji wa ulinganifu wa kitamathali au kinyume chake, na tatu utaangazia kutafsirika au kutotafsiri kwa dhana mahususi za kitamaduni. Hata hivyo, kuhusiana na tafsiri za tamathali, ni muhimu kutahadharisha kwamba tamathali ziliko katika *Song of Songs* ni za aina nyingi lakini tutajikita katika tafsiri za tashihisi, sitiari na tashbihi. Matini zetu kuu zitakuwa Biblia katika lugha ya Kiingereza, hasa kitabu cha *Song of Songs* na tafsiri yake katika lugha ya Kiswahili *Wimbo Ulio Bora*. Tutazirejelea sauti tatu kuu katika wimbo huu (ya kike, ya kiume na ya kundi) ili kuzitalii tamathali hizi katika wimbo huu wote. Utafiti wetu vilevile utajikita katika mwanda wa nadharia ya Tafsiri ya Masuala Mahususi ya Kitamaduni ya Newmark (1988).

## **1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada**

Swala la tafsiri kama taaluma iliyoshughulikiwa kiusomi katika lugha ya Kiswahili, lina mawanda mapana hasa linapoangaliwa kwa misingi ya maswala yaliyowahi kutafitiwa na mahitimisho yaliyofikiwa. Kwa misingi hii, tunaweza kuhoji kwamba ziko tafiti zilizoliangalia swala la tafsiri kijumla na kuna nyingine zilizomega hoja mahususi na kuzikita hoja hizo katika

maeneo mahususi ya kiusomi, kama vile tafsiri zinazohusiana na maswala ya kifasihi. Sawia na ilivyo kuhusiana na uteuzi wa maswala ya kiutafiti ya tafsiri, mahitimisho na kauli zilizowahi kutolewa juu ya tafsiri hasa pale ambapo Kiswahili ni lugha lengwa ni nyingi tena za aina mbalimbali. Baadhi ya tafiti zilizofanywa zimefikia kutoa mahitimisho na kauli kwamba kuna tafsiri duni, ambapo uduni huo unahusishwa na mambo mengi au inahojiwa kwamba unatokana na sababu nyingi. Kwa mfano, Zaja (1986), akirejelea madai yaliyotolewa na Ryanga (1981), anasema kuwa maoni ya Ryanga kuwa tafsiri nyingi za kifasihi zilizofanywa kutoka Kiingereza hadi Kiswahili huwa duni zikilinganishwa na matini asilia za Kiingereza anahoji kuwa, wasomi wa fasihi tafsiri ni wepesi katika kutoa lawama kwamba pale panapotokea ukiushi katika kazi zinazotafsiriwa, wasomi na wahakiki wa tafsiri za kifasihi wanachukulia ukiushi katika matini zilizotafsiriwa kuwa makosa na kwamba makosa haya ndiyo hufanya tafsiri hizi kuwa duni.

Kauli na maoni kama haya yanatokana na chukulizi na mitazamo inayochukulia na kuiangalia tafsiri kama shughuli ya ulinganifu wa kiisimu ambayo hushurutisha kwamba pawepo na ulinganifu kiisimu kati ya matini chanzi na matini lengwa. Katika miktadha fulani ambapo tafsiri inaweza kuwa imechukua mitazamo ya kiisimu, kauli kama hizi za matini kulingana zinaweza kukubaliwa, kwa sababu kimsingi ni sharti matini yoyote inayotokana na michakato ya kutafsiri ijitosheleze kiisimu katika miktadha lengwa. Hili ni jambo ambalo liko wazi kwamba maswala ya kiisimu yana umuhimu mkubwa katika shughuli nzima ya tafsiri. Hata hivyo, isimu ni kijisehemu kidogo au ni eneo dogo katika usomi wa tafsiri kwa sababu yapo maswala mengine mengi yanayokitwa katika matini inayotafsiriwa hasa pale ambapo matini husika inakuwa ya kifasihi, kitamaduni au kiantropolojia, ambapo mtafsiri hushurutika kujali mivutano au uwiano wa kitamaduni, tofauti za kiutamaduni na kiusomi, mivutano kati ya kaida za utamaduni chanzi na utamaduni lengwa, mambo ambayo katika upekee wao au kuhusishwa na mambo mengine katika matini husika, huchangia kubainika kwa upekee wa matini lengwa. Tafiti hizi japo zimetoa mchango katika uwanja wa tafsiri, zinaacha pengo ambalo kazi hii itajitahidi kuchangia kuliziba. Kazi nyingi za awali zilijikita sana kwenye maswala ya kiisimu na kutochunguza masuala mahususi ya kitamaduni yanayoathiri tafsiri. Kazi hii itachunguza masuala hayo kwa kurejelea kitabu cha *Song of Songs* na tafsiri yake katika lugha ya Kiswahili; *Wimbo Ulio Bora*.

Mutie (1997) ameshughulikia matatizo yanayohusu kuhamisha sanaa katika kazi zilizotafsiriwa. Katika kazi yake amerejelea tamthilia ya *Mizigo* ambayo ni tafsiri ya *The*

*Burdens*. Katika utafiti huu, anatoa ufafanuzi wa jinsi sanaa hudhoofishwa katika kazi ya tafsiri hasa katika kipengele cha fani. Maoni haya ya Mutie kuwa tafsiri za sanaa hudhoofisha sanaa si ya kweli katika kila tafsiri. Hii ni kwa sababu tafsiri nyingine zinaweza kuwa bora hata kushinda matini chanzi na hata kuibua masuala ya manufaa ambayo hayakuwepo kwenye matini chanzi. Mutie pia anahoji kuwa tofauti za kimuundo za lugha zinazohusika katika tafsiri huwa kikwazo kikuu katika uhawilishaji wa fani. Kazi ya Mutie inaacha pengo ambalo kazi hii itajaribu kuliziba, yaani kuangazia ni kwa nini mambo fulani ya kifasihi yanakuwa ni changamoto kuhawilishwa kutoka miktadha chanzi hadi miktadha lengwa. Wakati kazi yake (Mutie) inaegemezwa kwenye tofauti katika muundo wa lugha husika na athari zinazosababishwa na tofauti hizo za kimuundo katika uhawilishaji wa fani, kazi hii itaegemezwa kwenye mahusiano kati ya tamathali zenye upekee wa kitamaduni na tamaduni zinazochochua kuibuka kwa tamathali hizo na jinsi zinavyodhihirika katika uhawilishaji wa tamathali zenye urejeleaji wa kijinsia kwa kujikita kwenye Kitabu cha *Song of Songs* na tafsiri yake katika lugha ya Kiswahili; *Wimbo Ulio Bora*.

Zaja (2002) anasema kuwa, utafiti katika fasihi tafsiri katika lugha ya Kiswahili umekuwa kwa kipindi kirefu ukiegemezwa kwenye maswala ya ulinganifu. Hata hivyo, tafiti nyingi za sampuli hiyo, zimedhihirisha hali za ujumlishaji na uwepo wa ukosefu wa mwongozo thabiti wa kinadharia; yaani wataalamu wengi hawajauliza swali, ni kwa jinsi gani tafsiri imetumika kama njia ya kuakisi mahusiano yaliyopo kati ya tamaduni mbalimbali, hasa kwa kuzingatia mitagusano ya tafsiri na miktadha tofauti, tamaduni tofauti...(TY). Mawazo haya ya Zaja, yanaibua mwelekeo muhimu sana katika taaluma ya tafsiri. Hii ni kwa sababu anapendekeza kazi za tafsiri kutochungwa kana kwamba ni zao la maswala ya kiisimu pekee bali zichunguzwe pia kwa kuzingatia na kuhusisha masuala mapana ya kitamaduni na mitagusano ya tamaduni husika.

Zaja (2002) anaongeza kwamba, “Utafiti huu umekusudia kuvuka mipaka ya misimamo finyu au banifu ya kiisimu ili kutumia tafsiri kama kigezo cha kuchimuza kile ambacho kinaweza kuelezeka kama uhalisia fiche kuhusu tafsiri, yaani kutambua kuwa kando na tafsiri kuwa ni swala la kiisimu, pia ni shughuli inayoangazia mitagusano ya kitamaduni, ni njia za kuelewa maneno katika udhahania wao na katika miktadha ya matumizi, ni njia ya kuangazia miundo ya kiisimu kama mbinu ya kuelewa vipengee vya kitamaduni... (TY). Mawazo haya yanasisitiza kuwa badala ya kupendelea ulinganifu kati ya matini chanzi na matini lengwa

kiisimu pekee, pana haja ya kuzingatia ufaafu wa tafsiri kwa kuangalia miktadha ya uamilifu kitamaduni na kihistoria.

Aidha, Mule (2002) akimrejelea Zaja anapopinga maoni ya King'ei kuwa tafsiri ya Kiswahili ya *Wimbo wa Lawino* ina makosa, anasema kuwa mchakato kama huu wa kutafuta makosa huweza kuathiri uelewekaji wa matini iliyotafsiriwa. Tunaunga mkono msimamo wa Zaja na tunaonelea kuwa pana haja ya kujiuliza ni kwa nini mtafsiri alitafsiri kwa jinsi alivyotafsiri na si vingine. Ni maoni yetu kwamba kujiuliza swali hili ni njia nzuri ya kiutobinasfi ya kukabili tafsiri yoyote, hasa katika lugha ya Kiswahili. Fauka ya hayo, mwelekeo huu wa kuchunguza tafsiri kwa vigezo vya kiisimu pekee, unaweza kudumaza ukuaji wa tafsiri za fasihi katika fasihi ya Kiswahili. Hii ni kwa sababu mwelekeo wa kuiona matini chanzi kuwa bora kuliko ile iliyotafsiriwa na kujishughulisha sana na jinsi ambavyo matini chanzi ilivyotofautiana na matini lengwa kiisimu huweza kumfanya mtafsiri kutopambanua maswala mengine muhimu yaliyomo katika hiyo matini moja husika. Mule (2002) akimrejelea Zaja anasema...Zaja anaona ni hatia kwa wataalamu wa Kiswahili ambao wamejikusisha sana na utafutaji wa makosa katika matini zilizotafsiriwa katika lugha ya Kiswahili, huku wakisawiri matini lengwa kama matini 'yatima' ya matini chanzi. Zaja anaongeza kuwa mielekeo kama hiyo katika tafsiri za fasihi ya Kiswahili zimesababisha udumavu katika uwanja huo. Tafiti hizi, japo zimetoa mchango mkubwa katika uwanja wa tafsiri, zimeacha pengo ambalo utafiti huu unakusudia kulijaza. Kazi hii itajikita katika uchunguzi wa masuala mahususi ya kitamaduni hasa yanayohusiana na ujielezaji kijinsia, kukosekana kwa ulinganifu wakitamathali na changamoto za kutokuhawilisha dhana mahususi za kitamaduni. Hili ndilo pengo ambalo utafiti huu unapania kuchangia kuziba kutokana na kazi hizi.

Nangira (2004) anasema kuwa...ipo mielekeo ambayo kimsingi huliona swala la tafsiri kama shughuli ya kuonyesha matatizo ya tafsiri na athari zake juu ya lugha na fasihi lengwa, japo mara nyingi athari hizo zinachukuliwa kimakosa kwamba ni lazima zijitokeze katika lugha na fasihi lengwa. Mielekeo hii hujishughulisha na kuonyesha makosa ya kiisimu yanayojitokeza katika tafsiri zilizokwishafanywa. Kwa mfano, kazi ya Wanza, A. (1981), Zaja, (1986), Ryanga C.W. (1986) na kadhalika. Kimsingi, utafiti wa Nangira ulipania kuibua mtazamo tofauti wa kutafiti tafsiri za kifasihi kwa kuangazia swala la usomekaji katika misingi miwili—usomekaji kama tunavyouzoea kwa maana kwamba kaida na miundo ya kisarufi na kisintaksia iliyo katika matini lengwa inawezesha kazi husika kusomeka; na kwa upande wa pili usomekaji kwa maana ya kwamba kaida na miundo hiyo ya kiisimu inawezesha kuibua uelewa wa aina mahususi au

uelewa mbadala. Kwa kujikita katika uchunguzi wa taratibu za ujielezaji kijinsia, matumizi ya tamathali zinazorejelea jinsia ya kike na uibukaji wa dhana mahususi za kitamaduni katika kitabu cha *Song of Songs* na tafsiri yake katika lugha ya Kiswahili, *Wimbo Ulio Bora* kama matini lengwa, kazi hii itajaza pengo lililoachwa na utafiti wa Nangira (2004) ambalo ni kuchunguza utojitokezaji wa lugha mahususi ya ujielezaji kijinsia katika *Wimbo Ulio Bora* ukilinganisha kitabu hicho na matini chanzi, *Song of Songs* na hasa pale ambapo ulinganifu wa kitamathali, ujielezaji wa kijinsia na ulinganifu wa kidhana ndio msingi wa data yetu katika matini rejelewa.

Zaja (2006) ameshuhulikia utathmini wa kinadharia wa fasihi tafsiri ya Kiswahili. Katika kazi hii, mtaalamu huyu anapendekeza kuwa kunastahili kuwe na mbinu mbadala ya kusoma, kufafanua na kutoa kauli juu ya matini zilizotafsiriwa kwa misingi iliyo nje ya mifumo na miundo ya kiisimu. Anaongezea kuwa yapo masuala mengine nje ya masuala ya kiisimu ya matini husika kama vile masuala ya kimuktadha na ya kitamaduni yanayochangia matini chanzi kufikia matarajio ya hadhira lengwa. Zaja anasisitiza kuwa kupatikana kwa ulinganifu si tokeo la usawa wa kiisimu bali ni matokeo ya kitamaduni na historia yanayochangia kuibuliwa kwa matini lengwa katika tafsiri za kifasihi. Zaja katika kazi hii anasema kuwa uchunguzi wa fasihi tafsiri katika lugha ya Kiswahili umejihusisha na uhawilishaji wa ulinganifu wa kiisimu kati ya matini chanzi na matini lengwa ambapo msisitizo unawekwa kwenye kanuni za kimuundo za kiisimu. Mtaalamu huyu anaongezea kuwa hali kama hii huchukua mitazamo inayodumisha na kupendelea matini chanzi pamoja na utamaduni wake huku ikipuuza matini lengwa na utamaduni wake. Anasema kuwa kwa kujifunga katika matini chanzi, umuhimu wa matini lengwa huishia kupuuzwa na aghalabu huizua hadhira lengwa kufikia matarajio yake. Mawazo yake Zaja yatatufaa katika utafiti wetu kwa kuwa yatatupa mwelekeo wa kuipa hadhi matini lengwa katika utafiti wa tafsiri. Hata hivyo, kazi ya Zaja imeacha pengo ambalo kazi hii itajitahidi kuliziba ambalo ni kuchimuza na kubaini sababu za muachano wa kitamathali, muachano katika urejelelaji wa kijinsia na muachano wa kidhana kati ya matini chanzi na matini lengwa.

Nzyoka (2014) kwa upande wake ameshughulikia tathmini ya tafsiri na mikakati ya kutafsiri tamathali za usemi katika tamthilia ya *Antigoni*. Katika kazi yake, Nzyoka amebaini mikakati mbalimbali ya kutafsiri tamathali tofauti tofauti za usemi kama vile utohozi, jazanda, tashbihi miongoni mwa tamathali nyingine. Kazi ya Nzyoka imeacha mapengo ya utafiti ambayo kazi hii inatazamia kuyaziba. Huku akijikita katika tamathali kwa jumla, kazi yetu imeshughulikia

tamathali mahususi (tashbihi, sitiari na tashihisi), urejeleaji wa kijinsia na masuala mahususi ya kitamaduni. Hili ni pengo mojawapo. Aidha, mtafiti huyu, ameongozwa katika kazi yake na nadharia ya ufasiri ambayo inasisitiza ujuzi kamili wa kutumia lugha zote mbili zinazotumiwa katika matini na tafsiri yake, ufahamu mwafaka wa mada inayotafsiriwa na mbinu faafu za kutafsiri matini huku kazi yetu ikiongozwa na nadharia ya tafsiri ya masuala mahususi. Kwa hivyo, pengo la pili ni haja ya kutathmini mchango wa maswala mahususi ya kitamaduni katika kuchangia muachano wa kitamathali kati ya matini chanzi na matini lengwa. Hata hivyo, licha ya mapengo haya ya kiutafiti, kazi ya Nzyoka itatufaa kwa kutupa maelezo muhimu kuhusu tashbihi pamoja na tafsiri yake.

Shiroko (2014) ameshughulikia tafsiri ya jazanda, mchezo wa maneno na takriri katika tamthilia ya *Amezidi*. Katika kazi hii (kazi ya Shiroko-2014), anasema kuwa changamoto katika tafsiri ya tamathali hizi hutokea kwa sababu watafsiri wanashindwa kudumisha ulinganifu wa yaliyomo kwenye matini chanzi wakati wanapoyahawilisha kwenda kwa lugha lengwa. Kazi yake inaacha pengo la utafiti kwani kwa kushuhulikia tamathali hizi katika ujumla wake, pengo linaibuka kuhusu uchunguzi wa masuala mahususi ya kitamaduni na urejeleaji wa kijinsia. Anataja kuwa changamoto mojawapo inayokumba tafsiri ya tamathali ni tofauti katika tamaduni za lugha zinazohusika katika tafsiri. Anaongeza kuwa mtafsiri havezi kupuuza tofauti za kitamaduni anapofanya kazi ya tafsiri. Maelezo yake yatatufaa katika kuchunguza masuala ya kitamaduni ambayo yamedhihirika katika tafsiri ya *Wimbo Ulio Bora* na athari ya maswala hayo ya kitamaduni.

Saberi (2015) ameshughulikia mikakati ya kutafsiri istilahi za kitamaduni akitumia lugha ya Kiingereza kama lugha chanzi na Kipasia kama lugha lengwa. Katika kazi hii, amedokeza kuwa istilahi za kitamaduni huibua changamoto katika tafsiri ya matini mbalimbali. Anapendekeza mikakati kama vile; pale ambapo hakuna changamoto za kisiasa au za kidini, mtafsiri anaweza kutafuta istilahi zinazoibua ulinganifu na dhana hizo katika matini chanzi. Aidha, anapendekeza mkakati wa kutoa maelezo pale ambapo hakuna istilahi katika lugha lengwa ya kuelezea dhana husika miongoni mwa mikakati mingine. Utafiti wa Saberi ni wa kidini kwani kazi yake ikijikita katika mikakati ya kutafsiri istilahi za kidini, kazi yetu ni ya kifasihi ambapo tutaangalia kutojitokeza kwa lugha inayodhihirisha urejeleaji wa kijinsia, ulinganifu wa kitamathali pamoja na kidhana *Wimbo Ulio Bora* kama matini lengwa, matini hiyo inapolinanihwa na matini chanzi, *Song of Songs*. Hili ndilo pengo ambalo tutaliziba katika utafiti huu.

Yegon (2016) ameandika kuhusu uwasilishaji wa ufeministi kinzani katika Kiswahili kupitia tafsiri akirejelea tathmini ya riwaya ya *Barua Ndefu Kama Hii*. Katika kazi yake anasema kwamba, “Uchanganuzi wa ufeministi kinzani katika riwaya tuliyoiteua umebainisha kwamba tafsiri ndiyo imewezesha ufeministi kinzani kuwepo katika fasihi ya Kiswahili”. Katika kazi yake pia ametumia nadharia ya ufeministi wa kiafrika katika uchunguzi wa masuala ya kifeministi na nadharia ya mawasiliano kuchunguza masuala ya uhawilishaji wa maana. Huku kazi yake ikijikita katika ufeministi kinzani, kazi yetu itachunguza jinsi ambavyo msukumo mkubwa wa lugha ya kijinsia ilivyoyeyushwa katika tafsiri ya tamathali ya tashihisi, tashbihi na sitiari. Kuchunguza ulinganifu wa kitamathali na urejeleaji wa kwa msingi wa tafsiri ya masuala mahususi ya kitamaduni ni pengo la maarifa ambalo linahitaji kufanyiwa utafiti ili kulijaza.

Omuya (2017) akirejelea hadithi ya “Samueli Asikia Sauti ya Mungu”, amechunguza usimilishwaji wa *Biblia* kama fasihi ya watoto. Katika kazi yake amejadili aina tisa za usilimisho ambazo ni pamoja na usimilisho wa kintindo, usimilisho wa kiitikadi, usimilisho wa kiuamilifu na usimilisho wa kusahilisha. Aidha, amejadili usimilisho wa kiutanzu, usimilisho huru, usimilisho wa kiutamaduni, usimilisho wa kisasa na usimilisho wa kufupisha. Kwa kujikita katika kuchunguza usilimishwaji wa *Biblia* kama fasihi ya watoto kwa msingi wa nadharia ya wingimifumo, panaibuka pengo la kiutafiti la kuchunguza ulinganifu wa kitamathali, urejeleahi wa kijinsia na ulinganifu wa kidhana katika kitabu cha *Wimbo Ulio Bora* kwa misingi ya nadharia ya tafsiri ya masuala mahususi ya kitamaduni.

### **1.8 Msingi wa Nadharia**

Kulingana na Bassnett (2002), tafsiri inahusu mambo mengi yasiyo ya kiisimu ambayo mara nyingi hayaangaziwi na watafsiri wanapotafsiri kazi mahususi na vilevile hayaangaziwi na watafiti na wachanganuzi wanapotathmini matokeo ya tafsiri fulani mahususi. Mara nyingi katika kutafsiri, wanaotafsiri hawashirikishi katika tafsiri zao ukweli kwamba matini yoyote ya kifasihi ni mkusanyiko wa mifumo tata inayotegemeana, inayochangiana na inayokuzana. Vilevile kuna ithibati kwamba mifumo hii tata iliyo ndani ya matini haihusiani na mifumo mingine tata iliyo nje ya matini husika lakini ambayo ina athari za aina nyingi juu ya mifumo iliyo ndani ya matini. Kwa sababu hizi, kuna usambamba wa kiutekelezi unaojibainisha kati ya watafsiri na wachanganuzi wa fasihi tafsiri. Kwa sababu ya kutotambua na kushirikisha utata huu wa kimfumo, mtafsiri anaweza kuangazia katika tafsiri yake moja kati ya mambo mengi, kwa mfano kuangazia uhawilishaji wa maudhui na kwa hivyo katika kutafisiri kwake akaweka

kipaumbele katika ukuzi wa tasnifu ya kimsingi katika kazi inayotafsiriwa. Pili, kuna uwezekano, hasa pale ambapo mtafsiri ni mtaalam wa fasihi, kubaini uwepo wa mifumo mingi katika matini moja na vilevile kubaini jinsi mifumo hiyo inavyoathiriana na kwa hivyo kuweza kuishirikisha katika tafsiri yake. Tatu, kuna hali ambapo mtafsiri anaweza kuangazia na kikishughulikia kipengele kimoja katika kazi inayotafsiriwa na aghalabu hili hufanyika pale mtafsiri anapokuwa na malengo mahususi. Nne, uwezekano wa mtafsiri kubaini kuwepo kwa wasifu fulani katika kazi inayotafsiri na akutumia kwa malengo mahususi. Kwa upande wa pili, hali hizi zinaakisika kwa malengo ya watafiti na wachanganuzi wa fasihi tafsiri. Hizi ni kauli za kimsingi kushirikishwa katika uelewa wa uchanganuzi wa fasihi tafsiri.

Hervey and Higgins (1992) nao wanasema kuwa katika mchakato wa tafsiri halisi au tafsiri sahihi, mtafsiri huziba pengo la kimawasiliano kati wazungumzaji wa lugha moja na wazungumzaji wa lugha nyingine tofauti. Umbali wa uelewa wa masuala ya kitamaduni kati ya hadhira ya matini chanzi na hadhira ya matini lengwa, huweza kusababisha mwachano kati ya athari za kitamaduni za matini chanzi na matini lengwa. Mwachano huu hudhihirika sana katika tafsiri za kifasihi kutokana na idadi kubwa ya masuala mahususi ya kitamaduni yanayoweza kujitokeza katika matini hizi. Kadri mtafsiri anavyokuwa na ufahamu wa uchanganuzi wa tofauti kati ya tamaduni ndivyo anavyoweza kutafsiri vizuri. Kwa hivyo, lugha na utamaduni ni mambo mawili yaliyo na uhusiano wa karibu sana na ambayo hayawezi kutenganishwa. Nord (1997) akirejelea msisitizo wa Agar (1991) kuhusu uhusiano kati ya lugha na utamaduni anasema kuwa, Agar anaona lugha na utamaduni kama kitu kimoja na kuongeza kuwa mpaka wa utamaduni unadhihirishwa na masuala kama vile tabia inayosababisha kutowiana kwa tamaduni tofauti na kuvuruwa kwa mawasiliano kati ya lugha mbili zinazopakana.

Kulingana na Venuti (2004), wakati ambapo lugha mbili hazijaachana kiisimu na kitamaduni, mtafsiri anakumbana na changamoto chache katika mchakato wa kutafsiri. Hivi ni kumaanisha kuwa kutafsiri masuala mahususi ya kitamaduni katika tafsiri za kifasihi ni mchakato wenye changamoto kwani unahusisha ugumu wa kuibusha matini iliyotafsiriwa vyema pamoja na kuwa mwaminifu kwa ujumbe kwenye matini husika. Ugumu huu wa kutafsiri masuala mahususi ya kitamaduni unatokana na hali kwamba utamaduni mahususi wa jamii ndiyo unaozaa lugha ya jamii husika, huzaa dhana, huekeza maana katika dhana hizo na kwamba lugha ya jamii huakisi utamaduni ulioizaa. Kwa sababu tutajikita katika masuala mahususi ya kitamaduni yanayohusiana na ujielezaji wa kijinsia, uibukaji wa tamathali mahususi za kifasihi



pamoja na uibukaji wa dhana mahususi za kitamaduni, ili tuweze kuyabaini masuala haya mahususi katika matini tafsiri na kuweza kuyachanganua kihalisi na kiyakinifu, inatujuzu tufasiri ni nini kinachomaanishwa na dhana ya utamaduni, dhana ya masuala mahususi ya kitamaduni, kategoria ya masuala mahususi ya kitamaduni ili kutoa mwelekeo utakaongoza utafiti huu pamoja na kuonyesha umuhimu wa masuala mahususi ya kitamaduni katika tafsiri ya kifasihi.

### **1.8.1 Dhana ya utamaduni**

Larson (1984) kwa upande wake anaufasiri utamaduni kama mkusanyiko wa imani, mitazamo, tabia na sheria miongoni mwa kikundi fulani cha watu. Larson anaashiria katika maelezo yake kuwa utamaduni unahusu kila kitengo cha maisha ya mwanajamii husika. Vermeer (1987) naye kwa upande wake anahoji kuwa utamaduni ni mfumo wa kaida na chukulizi ambazo mtu kama mwanajamii wa jamii yake anastahili kujua ili awe kama kila mtu, au awe tofauti na kila mtu. Nord (1997) akimnukuu Vermeer (1986) anasema kwamba utamaduni ni kile ambacho mtu anastahili kujua ili atende kwa jinsi inayokubaliana na matarajio ya kijumla ya jamii husika. Mtaalamu huyu anasisitiza utendaji na tabia kama mihimili mikuu katika ufasiri wake wa dhana ya utamaduni. Hivi ni kumaanisha kuwa mtaalamu huyu anauona utamaduni kama mfumo changamano unaoathiri matendo na tabia ya mtu. Sewell (2009) anasema kuwa dhana ya utamaduni ni bia na inatumika katika nyanja mbalimbali kama vile anthropolojia, sosiolojia, fasihi miongoni mwa nyanja nyingine. Ijapokuwa maelezo haya ya Sewell yanaakisi ubia wa dhana husika, ni muhimu kutaja kwamba nyanja mbalimbali huona utamaduni kwa mwegemeo na ufasiri ambao ni tofauti.

Fasiri hizi zinaeleza utamaduni kama dhana changamano iliyo na athari katika maisha ya kila siku ya binadamu na inayohusisha historia, miundo ya kijamii, dini na hata lugha. Hata hivyo, katika kazi hii utamaduni utafasiriwa kwa mujibu wa kauli za Newmark kwa sababu yeye hafasiri tu utamaduni bali pia anasisitiza uhusiano kati ya lugha na jamii na kwa hivyo uhusiano kati ya lugha na utamaduni (Newmark, 2010). Newmark anasema, “Ninaurejelea utamaduni kiantropolojia pekee; yaani, jinsi ya kuishi na mazingira yaliyo mahususi kwa wazawa na wakaaji wa eneo fulani la kijiografia, linalodhibitiwa na mipaka ya lugha na pia jinsi inavyodhihirika katika lugha moja”. Kama inavyodhihirika katika mawazo haya, Newmark anauona utamaduni kwa misingi ya kiantropolojia. Kwa kufuata mwelekeo huu wa kiantropolojia, Newmark anahusisha maswala mbalimbali ya kitamaduni akimakinikia karne ya 21 ambapo utandawazi umepiga hatua kubwa katika kusababisha miingiliano ya kitamaduni

na udhoofishaji wa utambulishaji wa kitamaduni. Mwelekeo huu wa Newmark wa kuweka msisitizo kwenye masuala ya kitamaduni utatufaa katika kazi hii kuchunguza masuala ya ujielezaji kijinsia tukiongozwa na migao yake mitano ya masuala mahususi ya kitamaduni.

### **1.8.2 Dhana ya Masuala Mahususi ya Kitamaduni**

Baker (1992), anasema kuwa “Maneno katika lugha chanzi yanaweza kuwasilisha dhana ambazo hazijulikani kabisa katika lugha lengwa”. Dhana hizi zinaweza kuwa za kidhahania au dhana thabiti; dhana hizi zinaweza kuhusiana na imani za kidini, utamaduni wa jamii au hata aina ya chakula. Dhana kama hizo hurejelewa kuwa zina umahususi wa kitamaduni. Kwa mujibu wa maelezo haya ya Baker, masuala mahususi ya kitamaduni huhusu lugha mbili zenye tamaduni tofauti ambapo dhana iliyopo katika lugha moja au utamaduni moja, hukosekana au huwa haijulikani katika lugha ya pili. Hivi ni kumaanisha kuwa kila wakati kunapotokea mtagusano kati ya lugha mbili au zaidi, masuala mahususi ya kitamaduni hudhihirika katika lugha, kimfumo, kimawasiliano na kiuamilifu. Tofauti zinaweza kuwa nyingi na anuwai hivi kwamba inaweza kuonekana kana kwamba watu wa utamaduni fulani wanaona mambo kwa mtazamo wao. Lewis (2006) anahoji kwamba inaweza kuonekana kana kwamba watu wa tamaduni mbalimbali wanaishi katika ulimwengu wao unaotofautina. Njia mojawapo ambayo kwayo utamaduni hudhihirika ni matumizi ya maneno au misamiati inayorejelea nyenzo, vyombo au vifaa vya kitamaduni, mipangilio ya kitamaduni, uhalisi wa kiikolojia wa mahali mahususi, n.k. Dhana ya masuala mahususi ya kitamaduni zimerejelewa na wataalamu mbalimbali kwa jinsi tofauti tofauti. Kwa mfano, Baker (1992) anairejelea kama dhana mahususi ya kitamaduni, Robinson (1997) anazirejelea kama fenomena funge ya kitamaduni naye Gambier (2004) akizirejelea kama marejeleo mahususi ya kitamaduni. Newmark (2010), kwa upande wake anazirejelea kama maneno ya kitamaduni. Hata hivyo, msamiati unaokubalika zaidi ni masuala mahususi ya kitamaduni. Katika kazi hii, masuala mahususi ya kitamaduni ndio msamiati utakaotumika kinadharia katika utafiti huu.

Tofauti au ukinzani kati ya lugha mbili unaweza kushuhudiwa sio tu katika istilahi za masuala mahususi ya kitamaduni bali pia katika ufasiri pia. Axiela (1996) anasema kuwa katika tafsiri, masuala mahususi ya kitamaduni ni tokeo la mgogoro unaotokana na uwasilishaji wa kiisimu katika matini chasili ambao unapohawilishwa katika lugha lengwa unaibua matatizo ya kitamaduni kutokana na maana tofauti ya dhana husika katika utamaduni lengwa. Nord (1997) anafasiri masuala mahususi ya kitamaduni kama fenomena ya kitamaduni iliyopo katika utamaduni X lakini haipo kwa jinsi hiyo katika utamaduni Y. Ingawa kuna fasiri nyingi kuhusu

dhana ya masuala mahususi ya kitamaduni, kazi hii itachukua mwelekeo wa kufasiri masuala haya mahususi ya kitamaduni kama maneno au kifungu cha maneno kilichobainishwa na tofauti za kitamaduni.

Ingawa lugha hujumuisha masuala mengi mahususi ya kitamaduni, ni vigumu hata hivyo kutoa ufasiri mahususi wa kile kinachoweza kurejelewa katika matini kuwa na umahususi wa kitamaduni. Kulingana na Aixela (1996), masuala mahususi ya kitamaduni ni elementi za matini zinazohusiana na dhana fulani katika tamaduni ambazo zinaweza kuwa hazijulikani kwa mtumiaji wa lugha lengwa. Hivi ni kumaanisha kuwa masuala mahususi ya kitamaduni yanaibua pengo la kitamaduni kati ya lugha chanzi na lugha lengwa. Pengo kama hilo linapatikana wakati ambapo suala katika matini chanzi halipatikani katika utamaduni lengwa ama lugha lengwa haina neno la kurejelea suala hilo. Ili kuziba tofauti kati ya lugha tofauti, na kuibusha tafsiri ya kina inayoakisi yaliyomo katika matini asilia, wataalamu wamependekeza mikakati na michakato tofauti. Miongoni mwa wataalamu hao waliopendekeza mikakati tofauti ya kutafsiri ni Newmark (1988) aliyependekeza makundi matano ya kuzigawa dhana mahususi za kitamaduni pamoja na mikakati 17 ya kukabiliana na dhana hizi mahususi wakati wa kuzihawilisha.

### **1.8.3 Migao ya Masuala Mahususi ya Kitamaduni**

Dhana ya utamaduni, sawa na masuala mahususi ya kitamaduni, inajumuisha vitengo mbalimbali vya maisha ya binadamu ambapo dhana au ujielezaji wa kitamaduni unaweza kubainika. Ili kuweza kufanya uchanganuzi wa tafsiri ya masuala mahususi ya kitamaduni, ni muhimu kuyagawa maeneo ya dhana za kitamaduni katika kategoria mbalimbali ili kufanya uchanganuzi unaofuata mpangilio mahususi. Newmark (1988), alipendekeza kategoria tano za kuainisha ujitokezaji wa dhana na maneno ya kitamaduni ya lugha ngeni. Kategoria hizi ni pamoja na utamaduni wa ikolojia (mazingira), utamaduni wa nyenzo au vifaa vya kijamii (material culture), utamaduni wa maisha ya kijamii (social culture), utamaduni wa asasi za kijamii na asasi rasmi (social and institutional culture) pamoja na utamaduni wa ishara na tabia.

#### **a) Ikolojia**

Katika kategoria ya ikolojia inajumuisha lugha na dhana zinazohusiana na masuala mahususi ya kitamaduni yanayohusu mazingira ya kiikolojia na ya kijiografia kwa mujibu wa lugha inayotumika katika hali hizo. Hii inajumuisha upana wa lugha na dhana zinazohusiana na

wanyama, mimea, pepo na hali ya nchi kwa kurejelea vitu kama milima, mabonde, nchi tambarare. Masuala haya yanayojumuishwa hapa ni masuala yanayodhihirika kwa msambao mpana katika *Song of Songs*, ndani ya masuala haya kunaibuka sio tu dhana bali pia uelewa wa istilahi mahususi katika utamaduni wa lugha chanzi na hivyo istilahi hizo zinapohawilishwa kutoka lugha chanzi hadi lugha lengwa, umuhimu wao katika lugha lengwa unaangaliwa ili kubaini ni kwa kiasi gani kuna kuwiana au kutofautiana kwa dhana hizi. Lakini zaidi ni kwamba kuwiana huku au tofauti zinazojitokeza ni sharti zitumike kukuza ufahamu wa aina fulani mahususi.

### **b) Vifaa vya Kitamaduni**

Kategoria hii inajumuisha lugha na dhana zinazohusiana na chakula, mavazi, majengo, makazi, usafiri, rangi na mawasiliano, miongoni mwa mambo mengine. Kwa mujibu wa Newmark (1988) chakula kwa mfano, kwa wengi ni kiwakilishi cha utamaduni wa taifa au wa lugha fulani. Istilahi za kurejelea mavazi mbalimbali hutofautiana kutoka lugha moja hadi nyingine kwani pia huakisi utamaduni ya jamii husika na pia hupewa umuhimu kutegemea utamaduni husika. Nyumba, miji na usafiri pia huakisi dhana ambazo ni mahususi katika utamaduni husika. Kwa mujibu wa maelezo haya, kuna msambao mkubwa wa utamaduni wa vifaa vya kijamii au vifaa vya kitamaduni katika *Song of Songs* ambapo tafsiri yake katika Kiswahili, *Wimbo Ulio Bora* inapofanyiwa uchanganuzi wa kiulinganishi, kunadhihirika mwachano mkubwa kuhusiana na uhawilishaji wa vifaa vya jamii.

### **c) Utamaduni wa asasi na taasisi za kijamii**

Newmark (1988) anazigawa asasi hizi katika kategoria tano. Kategoria hizi ni pamoja na siasa, dini, masuala ya kihistoria na istilahi za kijamii. Kila mojawapo ya asasi hizi hudhihirisha istilahi ambao zina upekee wa kitamaduni hivi kwamba wakati wa kuhawilisha kutoka lugha moja hadi nyingine, mtafsiri hana budi kutilia maanani. Kategoria hii, sawa na nyingine itatufaa katika kuyaainisha maswala ya aina hii katika *Song of Songs* na tafsiri yake kwa lugha ya Kiswahili; *Wimbo Ulio Bora*. Katika matini tulizoshughulikia, asasi mbalimbali zimerejelewa. Kwa mfano, kuna asasi ya ndoa pale ambapo tunaambiwa katika sura ya tatu mstari wa kumi na moja (3:11), “Go forth, O ye daughters of Zion, and behold king Solomon with the crown wherewith his mother crowned him in the day of his espousals, and in the day of the gladness of his heart.” ambapo tafsiri ni, “Tokeni, enyi binti za Sayuni, mtazameni Mfalme Sulemani, amevaa taji alilovikwa na mamaye, siku ya posa yake, siku ya furaha ya moyo wake”. Maelezo haya kuhusu posa ambayo huhusishwa na ndoa, inabainika kuwa asasi ya ndoa ni miongoni

mwa asasi ambazo zimeangaziwa. Hapa ndoa ya Mfalme Sulemani imerejelewa na mpenziwe Mshulemi. Katika ndoa hii tunaona wapenzi hawa wakionyesha mapenzi yao kwa njia mbalimbali. Asasi nyingine ambayo imeangaziwa ni ile ya kifalme. Solomoni amerejelewa kama mfalme aliyevikwa taji. Kundi hili la utamaduni wa asasi na taasisi za kijamii ni miongoni mwa makundi ambayo tutachunguza kuona jinsi ambavyo limetafsirirwa.

#### **d) Utamaduni wa kazi na burudani**

Newmark anaigawa kategoria hii katika makundi mawili makuu. Makundi haya ni pamoja na kazi na burudani. Kazi zinazofanywa na wanajamii fulani wenye utamaduni wao huweza kuakisi dhana ambazo hazipatikani katika utamaduni mwingine. Hivi ni kumaanisha kuwa kazi pia zina umahususi wa kiutamaduni ambao ni sharti utiliwe maanani wakati wa kuhawilisha matini fulani kutoka lugha chanzi hadi lugha lengwa. Kwa njia hiyo, jinsi ambavyo burudani hufasiriwa hutofautiana kutoka utamaduni mmoja hadi mwingine. Jambo hili hulifanya masuala ya burudani pia kuakisi umahususi wa kiutamaduni ambao huwa muhimu kutiliwa maanani. Katika *Wimbo Ulio Bora*, tunaona kazi kama vile uchungaji na ufugaji. Kwa mfano katika sura ya kwanza mstari wa saba (1:7) tunaambiwa, “Tell me, O thou whom my soul loveth, where thou feedest, where thou makest thy flock to rest at noon: for why should I be as one that turneth aside by the flocks of thy companions?” ambapo tafsiri ni “Nijulishe, ee mpendwa wa nafsi yangu, ni wapi utakapolisha kundi lako, ni wapi utakapolilaza adhuhuri. Kwa nini niwe kama aliyefungiwa shela, karibu na makundi ya wenzako?” na useremala katika sura ya tatu mstari wa tisa (3:9) “King Solomon made himself a chariot of the wood of Lebanon.” ambapo tafsiri ni “Mfalme Sulemani alijitengenezea machela ya miti ya Lebanoni;” miongoni mwa kazi nyingine.

#### **e) Ishara na tabia**

Ishara na tabia fulani huwa na upekee wa kiutamaduni ambao huweza kuathiri uhawilishaji wa matini kutoka lugha chanzi hadi lugha lengwa. Kwa mfano, watu wakitabasamu kidogo tu wakati mtu amefariki, wakipiga makofi kuashiria shukrani zao, wakitema mate kuashiria kubariki, wakitikisa kichwa kuashiria kukubali au kukataa jambo, wakibusu vidole vyao kusalimu au kusifu, wakitumia kidole cha gumba kuashiria kuridhia jambo; yote haya yanaakisi upekee wa kitamaduni kwani huweza kuwepo katika utamaduni mmoja na ukosekane kwa mwingine. Katika matini tulizozirejelea; yaani *Song of Songs* na tafsiri yake katika lugha ya Kiswahili, *Wimbo Ulio Bora*, tabia na ishara zimejitokeza. Kwa mfano, *Wimbo Ulio Bora* sura

ya kwanza mstariwa pili (1:2), tunaambiwa, “Let him kiss me with the kisses of his mouth: for thy love is better than wine.” ambapo tafsiri yake ni “Kubusu na anibusu kwa kinywa chake. Maana pendo lako lapita divai.” Katika mfano huu, tunaona ishara ya kuonyesha mapenzi kwa njia ya kubusu. Aidha, sura ya pili mstari wa saba (2:7) inasema, “I charge you, O ye daughters of Jerusalem, by the roes, and by the hinds of the field, that ye stir not up, nor awake my love, till he please.” ambapo tafsiri yake ni “Nawasihi, enyi binti za Yerusalemu, kwa paa na kwa ayala wa porini, msiyachochee mapenzi, wala kuyaamsha, hata yatakapoona vema yenyewe.” Fungu hili linaashiria tabia ya kutoa maagizo au kuapai kwa njia ya wanyama.

#### **1.8.4 Mikakati ya Kutafsiri masuala mahususi ya kitamaduni**

Newmark (1988) anapendekeza mikakati kumi na saba (17) ya kukabiliana na tafsiri ya masuala mahususi ya kitamaduni. Mikakati hii ni pamoja na uhawilishaji, uasiliaji, ulinganifu wa kitamaduni, ulinganifu tumikizi, ulinganifu fafanuzi, uchanganuzi kisehemu, matumizi ya visawe, tafsiri ya moja kwa moja, msongeo au mabadiliko, usawazishaji, tafsiri tambulishwa, ufidiaji, urejeleaji, ujumuishaji, maelezo ya ziada, upanuzi na ubanaji wa maana pamoja na tafsiri ya muda. Licha ya kwamba Newmark amependekeza mikakati hii 17 ya kukabiliana na masuala mahususi ya kitamaduni, tumehiari kutumia baadhi tu ya mbinu hizi katika kazi yetu. Kwa mfano, tutatumia mbinu ya upanuzi na ubanaji wa maana, maelezo ya ziada, uhawilishaji wa moja kwa moja, ulinganifu fafanuzi, matumizi ya visawe, udondoshaji pamoja na tafsiri ya moja kwa moja. Tunateua mbinu hizi kwa sababu kwa maoni yetu ndizo zimejitokeza katika mchakato wa kuhawilisha *Song of Songs* hadi *Wimbo Ulio Bora*. Kwa hivyo, katika kufanya uchunguzi wa masuala mahususi ya kitamaduni na jinsi ambavyo yametafsiriwa, mbinu hizi zitatumika katika kuchunguza masuala haya yanayodhihirisha upekee wa kitamaduni katika matini tulizorejelea. Aidha mbinu hizi zitatuwezesha kuafikia malengo yetu katika kazi hii na kufikia mahitimisho yatakayotusaidia kutatua tatizo la utafiti tinaloshughulikia. Kwa hivyo katika sehemu hii, tumejishughulisha kufafanua mbinu ambazo kwa maoni yetu zimetumikishwa katika matini tulizozirejelea kwa kuzijadili au kuzifafanua na kisha kuzitolea mifano kutoka kwenye matini husika kama hapa chini.

##### **a) Uhawilishaji**

Huu ni mchakato wa kuhawilisha neno katika lugha chanzi hadi lugha lengwa kama mkakati wa tafsiri. Mkakati huu kwanza huhusisha kulifanya neno la lugha chanzi kuwiana na lugha lengwa kimatamshi na kisha kuwiana kimofolojia ya lugha lengwa. Newmark (1988) anahoji kuwa vifaa vya kitamaduni au dhana za kitamaduni pekee ndizo zinastahili kuhawilishwa.

## **Mifano:**

Katika mchakato wa kuhawilisha *Song of Songs* hadi *Wimbo Ulio Bora*, mbinu hii imedhihirika. Tazama mifano ifuatayo:

### **Mfano 1**

#### *Song of Songs 1:14*

“My beloved is unto me as a cluster of camphire in the vineyards of **En-gedi**.”

#### *Wimbo Ulio Bora 1:14*

“Mpendwa wangu ni kama kishada cha hina, katika mizabibu huko **Engedi**.”

### **Mfano 2**

#### *Song of Songs 4:11*

“Thy lips, O my spouse, drop as the honeycomb: honey and milk are under thy tongue; and the smell of thy garments is like the smell of **Lebanon**.”

#### *Wimbo Ulio Bora 4:11*

“Bibi arusi, midomo yako yadondosha asali, asali na maziwa viko chini ya ulimi wako; na harufu ya mavazi yako ni kama harufu ya **Lebanoni**.”

Katika mifano hii miwili, maneno En-Gedi na Lebanon yamehawilishwa kutoka lugha chanzi ya Kiingereza hadi lugha lengwa ya Kiswahili.

## **b) Ulinganifu Fafanuzi**

Katika mkakati huu, mtafsiri anajaribu kufafanua maana au jukumu la neno katika lugha chanzi anapolihawilisha hadi lugha lengwa. Mkakati huu hutumika wakati ambapo neno la lugha chanzi linahusiana na utamaduni mahususi wa lugha chanzi na matumizi ya maneno ya kitamaduni yanayowiana nayo katika lugha lengwa yanaonekana hayawezi kuhawilisha dhana husika kwa ukamilifu. Kwa sababu hiyo, maana ya matini iliyo na upekee wa kitamaduni huelezwa kwa maneno mengi. Tazama mfano ufuatao:

#### *Song of Songs 1:6*

“Look not upon me, because I am black, because the sun hath looked upon me: my mother's children were angry with me; they made me the keeper of the **vineyards**; but mine own vineyard have I not kept.”

***Wimbo Ulio Bora 1:6***

“Msinichunguze kwa kuwa ni mweusi mweusi, kwa sababu jua limeniunguza. Wana wa mamangu walinikasirikia, waliniweka niwe mlinzi wa **mashamba ya mizabibu**; bali shamba langu mwenyewe sikulilinda.”

**d) Matumizi ya Visawe**

Matumizi ya visawe ni mkakati wa tafsiri unaotumiwa katika hali ambapo neno katika lugha chanzi linakosa neno lenye maana sawa katika lugha lengwa. Katika mkakati huu, neno la lugha lengwa litumiwalo kuhawilisha neno hilo la lugha chanzi ni lile linalokaribiana nalo.

Tazama mifano ifuatayo:

**Mfano 1**

***Song of Songs 1:13***

“A **bundle** of myrrh is my wellbeloved unto me; he shall lie all night betwixt my breasts.”

***Wimbo Ulio Bora 1:13***

“Mpendwa wangu ni kama **mfuko** wa manemane ukilazwa usiku maziwani mwangu.”

**Mfano 2**

***Song of Songs 6:11***

“I went down into the **garden** of nuts to see the fruits of the valley, and to see whether the vine flourished, and the pomegranates budded.”

***Wimbo Ulio Bora 6:11***

“Nilishukia katika **bustani** ya milozi, ili kuyatazama machipuko ya bondeni; nione kama mzabibu umechanua, kama mikomamanga imetoa maua.”

**e) Tafsiri ya Moja kwa Moja**

Mkakati huu pia hujulikana kama tafsiri kopa. Huhusisha kutafsiri maneno ya lugha chanzi moja kwa moja hadi lugha lengwa. Tazama mifano ifuatayo:

**Mfano 1**

***Song of Songs 7:4***

“Thy neck is as a **tower of ivory**; thine eyes like the fishpools in Heshbon, by the gate of Bath-rabbim: thy nose is as the tower of Lebanon which looketh toward Damascus.”

***Wimbo Ulio Bora 7:4***



“Shingo yako ni kama huo **mnara wa pembe**; macho yako kama viziwa vya Heshboni, karibu na mlango wa Beth-rabi; pua yako ni kama mnara wa Lebanoni, unaoelekea Dameski.”

## Mfano 2

*Song of Songs 4:5*

“**Thy two breasts** are like two young roes that are twins, which feed among the lilies.”

*Wimbo Ulio Bora 4:5*

“**Matiti yako mawili** ni kama wanapaa wawili, nyuma ya barakoa yako. Ambao ni mapacha ya paa; wakilisha penye nyinyoro.”

## f) Mabadiliko ya kimuundo

Kwa mujibu wa mkakati huu, mtafsiri anabadilisha muundo asilia wa sentensi katika lugha chanzi anapohawilisha matini husika hadi lugha lengwa ili kuafikia hali ya ulinganifu. Mabadiliko haya hufanywa ikiwa kuna tofauti kati ya miundo ya lugha chanzi na lugha lengwa. Mabadiliko haya yaweza kuhusisha kugeuza hali ya wingi hadi hali ya umoja, kubadili nafasi ya vivumishi na hata kuabadili muundo mzima wa sentensi wakati wa uhawilishaji wa matini husika kutoka lugha chanzi hadi lugha lengwa. Kimsingi, mkakati huu huhusisha mabadiliko katika sarufi ya lugha chanzi wakati wa kuhawilisha kutoka lugha chanzi hadi lugha lengwa kama vile kugeuza hali ya umoja kuwa hali ya wingi, kubadili kitenzi cha lugha chanzi kuwa kategoria tofauti katika lugha lengwa na hata kubadili kundi la nomino katika lugha chanzi hadi nomino katika lugha lengwa. Mabadiliko haya yanachochewa na kuwepo kwa muundo fulani katika lugha chanzi lakini muundo huo unakosekana katika lugha lengwa. Tazama mifano ifuatayo:

## Mfano 1

*Song of Songs 1:9*

“**I have compared thee, O my love**, to a company of horses in Pharaoh's chariots.”

*Wimbo Ulio Bora 1:9*

“**Mpenzi wangu, nimekulinganisha** na farasi katika magari ya Farao.”

## Mfano 2

*Song of Songs 2:2*

“As the lily among thorns, so is **my love** among the daughters.”

*Wimbo Ulio Bora 2:2*

“Kama fahirisi kati ya miiba, kadhalika **mpenzi wangu** kati ya binti.”

### g) Upanuzi na Ubanaji wa Maana

Mkakati wa ubanaji wa maana unahusisha kupunguzwa kwa sehemu za neno la lugha chanzi. Kwa mfano, mtafsiri anaweza kutumia neno gari kama neno tafsiri ya neno “*automobile*”. Kwa upande mwingine, upanuzi wa maana nao unahusisha kupanua elementi za neno linapohawilishwa hadi lugha lengwa. Kwa mfano mtafsiri kutumia neno samaki kama tafsiri ya neno “*whale*” katika lugha chanzi (lugha ya Kiingereza).

#### Mfano 1

##### *Song of Songs 3:3*

“The **watchmen** that go about the city found me: to whom I said, saw ye him whom my soul loveth?”

##### *Wimbo Ulio Bora 3:3*

“**Walinzi** wazungukao mjini waliniona; Je! Mmemwona mpendwa wa nafsi yangu?”

#### Mfano 2

##### *Song of Songs 6:12*

“Or ever I was aware, my soul made me like the **chariots** of Amminadib.”

##### *Wimbo Ulio Bora 6:12*

“Kabla sijajua, roho yangu ilinileta katikati ya **magari** ya wakuu wangu.”

### h) Udondoshi

Katika mchakato huu, neno, elementi au sehemu fulani katika matini ya lugha chanzi hudondoshwa wakati wa kutafsiri. Mkakati huu hutumika ili kuepuka uziada katika matini, miiko yenye misingi ya kitamaduni katika lugha husika, kuvuka vizingiti vya kitamaduni na wakati mtafsiri anapotaka kuwasilisha habari muhimu pekee. Tazama mfano ufuatao:

##### *Song of Songs 2:3*

“As the apple tree among the trees of the wood, so is my beloved among the sons. I sat down under his shadow with great delight, and his fruit was sweet **to my taste**.”

##### *Wimbo Ulio Bora 2:3*

“Kama mpera kati ya miti ya msituni, kadhalika mpendwa wangu kati ya vijana. Niliketi kivulini mwake kwa furaha, na matunda yake niliyaonja kuwa matamu. ”

##### *Song of Songs 3:3*

“The watchmen that go about the city found me: **to whom I said**, Saw ye him whom my soul loveth?”

### ***Wimbo Ulio Bora 3:3***

“Walinzi wazungukao mjini waliniona; Je! Mmemwona mpendwa wa nafsi yangu?”

Inadhihirika kuwa baadhi ya mikakati ya kitafsiri aliyopendekeza Newmark (1988) imedhihirika katika matini lengwa kutokana na jinsi ambavyo matini hiyo ilivyosawiriwa ikilinganishwa na matini chanzi. Mikakati hii itakuwa ya manufaa makubwa katika kati yetu kwa kufafanua ulinganifu au ukosefu wake matini lengwa inapolinganishwa na matini chanzi.

## **1.9 Mbinu ya Utafiti**

Katika sehemu hii, tuliangazia mbinu tulizotumia kuteua sampuli, zile zilizotumiwa kukusanya data, aina ya data iliyokusanywa, zile zilizotumiwa kuchanganua data au kutathmini matokeo ya uchunguzi pamoja na uwasilishaji wa data. Kwa sababu ya masuala haya, sehemu hii tuliigawa katika vijimada kama ifuatavyo:

### **1.9.1 Uteuzi wa Sampuli**

Utafiti wetu kimsingi ulikuwa wa maktabani. Kimsingi, katika kazi hii, sampuli lengwa iliyoteuliwa ni Biblia hasa kitabu cha *Song of Songs* na tafsiri yake katika lugha ya Kiswahili, *Wimbo Ulio Bora*. Matini hizi tulizidavua ili kupata mambo ya kimsingi pamoja na data muhimu zilizohitajika katika utafiti huu. Tulizisoma matini hizi na kudondoa lugha inayoashiria ujielezaji wa kijinsia, tamathali zinazojitokeza hususan tashihisi, tashbihi na sitiari, dhana mahususi za kitamaduni katika lugha ya Kiingereza na tafsiri yake katika lugha ya Kiswahili na kuziorodhesha. Aidha, tulidurusu matini tofauti tofauti ambazo kwa tamthmini yetu ziliufaidi uchunguzi wetu. Tulizidurusu zile zinazohusu tafsiri ya tamathali husika; tashihisi, tashbihi na sitiari. Pia, tulidurusu zile zinazohusu *Wimbo Ulio Bora* na tafsiri yake pamoja na zile zilizohusu nadharia ya tafsiri ya masuala mahususi ya kitamaduni. Tulisoma vitabu, majarida na tasnifu zilizohusu mijadala mbalimbali katika maswala ya tafsiri. Vilevile, tulitalii makala yaliyochapishwa na pia kuzama mitandaoni kutafuta kazi zilizoshughulikia tafsiri ya lugha ya kitamathali katika vitabu vingine katika Biblia kando na *Wimbo Ulio Bora*. Hii ni kwa sababu tuliamini kwamba kwa kufanya hivi tungepata maarifa ya kutosha ambayo yangetuwezesha kutimiza matakwa ya mada yetu ya utafiti.

### **1.9.2 Mbinu za ukusanyaji data**

Sehemu hii ilihusu mikakati tuliyoitumia kupata data zilizofaa utafiti wetu. Kimsingi, ukusanyaji wetu wa data ulihusu kukisoma kitabu cha *Song of Songs* na tafsiri yake ya *Wimbo*

**Ulio Bora.** Tuliorodhesha mifano mbalimbali ya lugha ya ujielezaji kijinsia, tamathali zinazojitokeza hasa tashihisi, sitiari na tashbihi. Hali kadhalika tulidondoa dhana mahususi za kitamaduni zinazojitokeza katika matini chanzi na tafsiri yake katika matini lengwa. Dhana hizi mahususi pia tulizigawa katika matapo mbalimbali yakiwemo: zile zinazohusiana na wanyama, zile zinazohusu mimea (ikolojia), viungo vya mwili, madini na hata zile zinazohusiana na masuala ya uhandisi (vifaa vya kitamaduni).

Baada ya kuzipanga tamathali hizi, tulihakiki jinsi ambavyo tafsiri ya tamathali hizi imefanywa katika lugha ya Kiswahili kwa kuzilinganisha na jinsi zilivyo katika lugha ya Kiingereza. Tulitumia data hii kuchunguza jinsi ambavyo lugha iliyo na msukumo mkubwa wa ujielezaji wa kijinsia katika *Song of Songs* ilivyotafsiri, maswala yanayojitokeza katika tafsiri yake kwa lugha ya Kiswahili pamoja na kubaini kama kuna ruwaza fulani katika tafsiri husika. Makundi aliyopendekeza Newmark (1988) ndiyo yaliongoza kazi hii.

Kihatua, utafiti huu ulifanywa katika hatua tatu. Hatua ya kwanza ilihusisha kusoma Kitabu cha *Song of Songs* kama matini chanzi ili kubaini masuala mahususi ya kitamaduni kwa kuzingatia zile nyanja 5 anazopendekeza Newmark (ikolojia, vifaa vya kitamaduni, utamaduni wa kijamii, asasi pamoja na ishara na tabia). Hatua ya pili ilihusisha kusoma matini lengwa; yaani, *Wimbo Ulio Bora* ili kubaini masuala mahususi ya kitamaduni katika tafsiri hiyo. Hatua ya mwisho ilikuwa kulinganisha masuala mahususi ya kitamaduni katika *Song of Songs* na tafsiri ya masuala hayo katika *Wimbo Ulio Bora* ili kubaini ulinganifu au utojitokezaji.

### **1.9.3 Uchanganuzi na uwasilishaji wa data**

Baada ya kukusanya data tulizohitaji, tulizichanganua kwa kutoa maelezo na ufafanuzi wa kina. Ufafanuzi huu uliongozwa na malengo yetu ya utafiti. Hivi ni kumaanisha kuwa tulitoa maelezo kuhusu jinsi ambavyo nafasi ya tafsiri na kaida za tafsiri katika lugha lengwa zilivyoathiri uhawilishaji wa tamathali kutoka lugha ya Kiingereza hadi ya Kiswahili. Uchanganuzi huu uliegemezwa kwenye misingi ya nadharia ya masuala mahususi ya kitamaduni ambayo inaweka msisitizo kwenye kuvigawa vipengee vinavyotafsiriwa katika makundi ya kitamaduni na kisha kuvihawilisha kwa kutumia mikakati ifaayo. Katika uchanganuzi wetu pia, tuliegemeza ithibati yetu kwenye ushahidi mwafaka kutoka kwenye kitabu cha *Song of Songs* na tafsiri yake kwa lugha ya Kiswahili; *Wimbo Ulio Bora*. Baada ya kuchanganua data hizi na kuzitolea ufafanuzi, tuliwasilisha matokeo ya uchanganuzi huu kwa njia ya maelezo pamoja na kutoa mapendekezo yetu.

## SURA YA PILI

### UJIELEZAJI WA KIJINSIA KATIKA *SONG OF SONGS*

#### 2.0 UTANGULIZI

Kudhihirika kwa makundi mbalimbali ya jamii, hususan yale yanayotokana na uana au jinsia ni suala ambalo hutokea katika matini mbalimbali, hasa pale ambapo masuala haya ya kijinsia yametiliwa maanani au mikabala ya kuichunguza matini husika inachimiza uana. Kama mojawapo ya malengo yetu, tulizingatia kujitokeza au kutojitokeza kwa lugha inayoakisi jinsia kati ya matini chanzi *Song of Songs* na matini lengwa *Wimbo Ulio Bora*. Ili kuafikia malengo haya, tuliigawa sehemu hii katika matapo matatu; kila tapo likidokeza masuala mahususi kuhusu lugha inayodhihirisha jinsia katika kitabu cha *Song of Songs*. Matapo haya ni pamoja na yale yanayohusu nomino zilizotajwa kwa jinsi zinavyobainisha jinsia, viwakilishi ambavyo vimedokezwa kwa kuhusishwa na jinsia mahususi pamoja na vivumishi vinavyoakisi jinsia. Tafsiri ya bibilia tuliyojikita kwayo ni ile ya *King James Version* katika lugha ya Kiingereza na *Swahili Standard Version* katika lugha ya Kiswahili. Udhihirikaji huu wa kijinsia tumeugawa katika makundi manne ambayo ni pamoja na nomino za kawaida, virai nomino, viwakilishi na vivumishi kama ifuatavyo:

#### 2.1 Nomino za kawaida

Waihiga (1999) anasema kuwa nomino za kawaida hazibainishi waziwazi vitu ambavyo habari zake zinatolewa. Mgullu (1999) kwa upande wake anasema kuwa nomino za kawaida ni nomino zinazotaja vitu vya kawaida ambavyo si vya pekee. Maoni haya ya Mgullu yanawiana na ya Matei (2014) ambaye anasema kuwa nomino ya kawaida au nomino jumla ni nomino ambayo hutaja mtu, mahali, au wazo ambalo si maalumu. Hutaja kitu kwa ujumla bila kukitambulisha zaidi kwa jina lake mahususi. Nomino za aina hii hazianzi kwa herufi kubwa isipokuwa pale zinapoanza sentensi. Nomino hizi, zimetumika katika kitabu cha *Song of Songs* kuakisi uana kwa binadamu na vilevile kwa wanyama. Nomino pamoja hizi zimedhihirisha jinsia mbalimbali kama ifuatayo:

##### 2.1.1 Wanyama

Katika kitabu cha *Song of Songs*, kuna wanyama ambao wametajwa kwa njia inayodhihirisha jinsia yao. Wanyama hawa wanajumuisha jinsia ya kike na ya kiume. Tazama mifano ifuatayo:

### **Mfano 1 (hart)**

Neno hili ‘hart’ ambalo linamaanisha ‘swara wa kiume’ limetumika katika matini chanzi mara tatu, yaani katika sura pili mstari wa tisa (2:9), sura ya pili mstari wa kumi na saba (2:17) na sura ya nane mstari wa kumi na nne (8:14). Katika mara zote hizi, neno hili limetafsiriwa katika matini lengwa kama ‘ayala’. Tazama mfano ufuatao:

#### ***Song of Songs 2:9***

“My beloved is like a roe or a young **hart**: behold, he standeth behind our wall, he looketh forth at the windows, shewing himself through the lattice.”

#### ***Wimbo Ulio Bora: 2:9***

“Mpendwa wangu ni kama paa, au **ayala**. Tazama, asimama nyuma ya ukuta wetu, achungulia dirishani, atazama kimiani.”

‘Hart’ ni swala wa kiume. Nomino hii imetafsiriwa katika katika matini lengwa kama ayala. Katika tafsiri hii, ubainishaji wa jinsia ya kiume inayoakisiwa katika matini chanzi inakosekana katika matini lengwa. Hali hii kwa mujibu wa nadharia tuliyoitumia huweza kuhusishwa na dhana hii kukosekana katika lugha lengwa, jambo linalomfanya mtafsiri kutafsiri kwa kutumia neno la kijumla ambalo haliakisi jinsia yoyote. Pamoja na mfano huu, ubainishaji wa jinsia ya kiume kwa kutumia neno hili (hart) umedhihirika kwingineko katika kitabu cha *Song of Songs*. Tazama mifano ifuatayo:

#### ***Song of Songs 2:17***

“Until the day break, and the shadows flee away, turn, my beloved, and be thou like a roe or a young **hart** upon the mountains of Bether.”

#### ***Wimbo Ulio Bora 2:17***

“Hata jua lipunge, na vivuli vikimbie, unigeukie, mpendwa wangu, nawe uwe kama paa, au **ayala**, juu ya milima ya Betheri.”

#### ***Song of Songs 8:14***

“Make haste, my beloved, and be thou like to a roe or to a young **hart** upon the mountains of spices.”

#### ***Wimbo Ulio Bora 8:14***

“Njoo, mpenzi wangu, uwe kama swala au kama **ayala** mdogo juu ya milima iliyojaa vikolezo.”

Katika mifano yote hii, uana haujitokezi katika matini lengwa *Wimbo Ulio Bora* kama ilivyoakisiwa katika *Song of Songs*.

### **Mfano wa 2 (hinds)**

Neno hili ‘hind’ ambalo linamaanisha ‘swara wa kike’ limetumika katika matini chanzi mara mbili, yaani katika sura pili mstari wa saba (2:7) na katika sura ya tatu mstari wa tano (3:5).

Katika mara zote hizi, neno hili limetafsiriwa katika matini lengwa kama ‘ayala’. Tazama mifano ifuatayo

***Song of Songs 2:7***

“I charge you, O ye daughters of Jerusalem, by the roes, and by the **hinds** of the field, that ye stir not up, nor awake my love, till he please.”

***Wimbo Ulio Bora 2:7***

“Nawasihi, enyi binti za Yerusalemu kwa paa na kwa **ayala** wa porini msiyachochee mapenzi, wala kuyaamsha, hata yatakapoona vema yenyewe.”

***Song of Songs 3:5***

“I charge you, O ye daughters of Jerusalem, by the roes, and by the **hinds** of the field, that ye stir not up, nor awake my love, till he please.”

***Wimbo Ulio Bora 3:5***

“Nawasihi, enyi binti za Yerusalemu, kwa paa na kwa **ayala** wa porini, msiyachochee mapenzi, wala kuyaamsha, hata yatakapoona vema yenyewe.”

Katika mfano huu, neno ‘hinds’ katika matini lengwa linaakisi jinsia ya kike katika lugha chanzi. Hata hivyo tafsiri yake ‘ayala’ katika matini lengwa inaleta hali ya ukosefu wa ulinganifu wa kati ya matini chanzi na matini lengwa. Hii ni kwa sababu mtafsiri ametafsiri kimaelezo kwa sababu ya dhana hii kukosekana katika lugha lengwa.

Katika mifano yote hii, uana haujitokezi katika matini lengwa **Wimbo Ulio Bora** kama ilivyoakisiwa katika **Song of Songs**. Wanyama hawa ambao wamebainishwa kijinsia katika kutajwa kwao, wamedhihirika katika jinsia ya kiume na ya kike. Kwa mfano neno ‘**hinds**’ ambalo ni nomino inayodokeza jinsia ya kike huku nomino ‘**harts**’ ikidhihirisha jinsia ya kiume. Katika hali zote, udhihirishaji wa kijinsia unakosekana; hali ambayo kwa mujibu wa nadharia tuliyoitumia, kutojitokeza kwa ulinganifu katika kuakisi jinsia kunatokana na dhana hizi kukosekana katika lugha lengwa.

### **2.1.2 Binadamu**

Kando na nomino jumla zinazohusu wanyama, kunazo nomino jumla pamoja ambazo zimetumika pia kuakisi jinsia ya mbalimbali. Mifano ifuatayo inadhihirisha ukweli huu.

### **Mfano wa 1 ( daughters)**

Nomino hii ‘daughters’ ambayo inadhihirisha jinsia ya kike imetumika mara mbili katika matini chasili; yaani sura ya pili mstari wa pili (2:2) na sura ya sita mstari wa tisa. Hata hivyo tafsiri yake katika maini lengwa kama ‘binti’ inadhihirisha ulinganifu kati ya matini husika katika kuakisi jinsia ya kike. Hali hii kwa mujibu wa nadharia tuliyoihusisha katika kazi hii inatokana na dhana husika kuwepo katika lugha mbili husika. Tazama mifano ifuatayo:

#### ***Song of Songs 2:2***

“As the lily among thorns, so is my love among the **daughters**.”

#### ***Wimbo Ulio Bora 2:2***

“Kama fahirisi kati ya miiba, kadhalika mpenzi wangu kati ya **binti**”

#### ***Song of Songs 6:9***

“My dove, my undefiled is but one; she is the only one of her mother, she is the choice one of her that bare her. The **daughters** saw her, and blessed her; yea, the queens and the concubines, and they praised her.”

#### ***Wimbo Ulio Bora 6:9***

“Hua wangu, mkamilifu wangu, ni mmoja tu, mtoto wa pekee wa mamaye. Ndiye kipenzi chake aliyemzaa, **binti** wakamwona wakamwita heri; malkia na masuria nao wakamwona, wakamsifu, wakisema,”

Katika mfano huu wa mwisho (6:9), japo jinsia katika matini asilia inadhihirika pia katika matini lengwa, kibainishi ‘the’ katika ‘the daughters’ linadondoshwa katika matini lengwa. Aidha, wingi unaoakisiwa na {s} katika matini chasili umeakisiwa katika matini lengwa kimuktadha tu. Hali hii kwa mujibu wa nadharia tuliyoitumia inatokana na tofauti kati ya lugha husika katika kuakisi wingi wa maneno.

### **Mfano wa 2 (sons)**

Nomino hii imetumika mara moja pekee katika matini chasili *Song of Songs* ambapo inadhihirisha jinsia ya kiume. Tazama mfano ufuatao:

#### ***Song of Songs 2:3***

“As the apple tree among the trees of the wood, so is my beloved among the **sons**. I sat down under his shadow with great delight, and his fruit was sweet to my taste.”

#### ***Wimbo Ulio Bora 2:3***

“Kama mpera kati ya miti ya msituni, kadhalika mpendwa wangu kati ya **vijana**. Niliketi kivulini mwake kwa furaha, ka matunda yake niliyaonja kuwa matamu.”



Katika mfano huu, neno ‘sons’ ambalo katika matini chasili linaakisia jinsia ya kiume limetafsiriwa katika matini lengwa kama ‘vijana’. Neno hili ‘vijana’ ambalo mtafsiri amehiari kulitumia haliakisi jinsia ya kiume inayoakisiwa katika matini chasili. Hii ni kwa sababu neno ‘vijana’ limeegemea zaidi upande wa kuakisi udogo wa kiumri kuliko kuakisi wazi jinsia ya kiume kama ilivyo katika matini chasili. Kwa mujibu wa nadharia ya tafsiri ya masuala mahususi ya Newmark (1988) tuliyoitumia katika kazi hii, hali hii inatokana na dhana ya ‘son’ kukosekana katika lugha lengwa.

### **Mfano wa 3 (queens)**

Nomino hii ‘queens’ imetumika mara mbili katika matini chasili; yaani, katika sura ya sita mstari wa nane (6:8) pamoja na sura ya sita mstari wa tisa (6:9). Katika mifano hiyo miwili, nomino hii inaakisi jinsia ya kike. Tazama mifano ifuatayo:

#### ***Song of Songs 6:8***

“There are threescore **queens**, and fourscore concubines, and virgins without number.”

#### ***Wimbo Ulio Bora 6:8***

“Wako **malkia** sitini, na masuria themanini, na wanawali wasiohesabika;”

#### ***Song of Songs 6:9***

“My dove, my undefiled is but one; she is the only one of her mother, she is the choice one of her that bare her. The daughters saw her, and blessed her; yea, the **queens** and the concubines, and they praised her.”

#### ***Wimbo Ulio Bora 6:9***

“Hua wangu, mkamilifu wangu, ni mmoja tu, mtoto wa pekee wa mamaye. Ndiye kipenzi chake aliyemzaa, binti wakamwona wakamwita heri; **malkia** na masuria nao wakamwona, wakamsifu, wakisema,”

Katika mfano hii, nomino ‘**queens**’ ambayo imetafsiriwa kuwa malkia inadhihirisha kujitokeza kwa masuala ya uana kati ya matini hizi mbili husika. Hali hii kwa mujibu wa nadharia tuliyoitumia katika kazi hii inatokana na hali kuwa dhana hii inapatikana katika lugha zote mbili. Hata hivyo, mpangilio wa kisintaksia wa maneno ‘sixty queens’ unabadilika kwa sababu mpangilio wa kisintaksia wa nomino na kivumishi katika lugha zote mbili husika unatofautiana.

#### **Mfano wa 4 (concubines)**

Neno hili ‘concubines’ limetumika mara mbili katika matini chanzi ikidhihirisha masuala mahususi ya kiafsiri. Tazama mifano ifuatayo:

*Song of Songs 6:8*

“There are threescore queens, and fourscore **concubines**, and virgins without number.”

*Wimbo Ulio Bora 6:8*

“Wako malkia sitini, na **masuria** themanini, na wanawali wasiohesabika;”

*Song of Songs 6:9*

“My dove, my undefiled is but one; she is the only one of her mother, she is the choice one of her that bare her. The daughters saw her, and blessed her; yea, the queens and the **concubines**, and they praised her.”

*Wimbo Ulio Bora 6:9*

“Hua wangu, mkamilifu wangu, ni mmoja tu, mtoto wa pekee wa mamaye. Ndiye kipenzi chake aliyemzaa, binti wakamwona wakamwita heri; malkia na **masuria** nao wakamwona, wakamsifu, wakisema,”

Katika mifano hii, nomino ‘**queens**’ ambayo imetafsiriwa kuwa malkia inadhihirisha kujitokeza kwa masuala ya uana kati ya matini hizi mbili husika. Hali hii kwa mujibu wa nadharia tuliyoitumia katika kazi hii inatokana na hali kuwa dhana hii inapatikana katika lugha zote mbili.

#### **Mfano wa 5 (sister)**

Nomino hii imetumika katika matini chasili mara saba; yaani katika sura ya nne mstari wa tisa (4:9), sura ya nne mstari wa kumi (4:10), sura ya nne mstari wa kumi na mbili (4:12), sura ya tano mstari wa kwanza (5:1), sura ya tano mstari wa pili (5:2) pamoja na sura ya nane mstari wa nane ambapo nomino hii imejitokeza mara mbili. Katika mar azote hizo saba, nomino hii imetafsiriwa kama ‘dada’ hali inayodhihirisha ulinganifu katika kuakisi uana katika matini zote. Hali hii kwa mujibu wa nadharia ya tafsiri ya masuala mahususi za kitamaduni inatokana na kuwepo kwa dhana husika katika lugha zote. Tazama mfano huu:

*Song of Songs 4:9*

“Thou hast ravished my heart, my **sister**, my spouse; thou hast ravished my heart with one of thine eyes, with one chain of thy neck.”

***Wimbo Ulio Bora 4:9***

“Umenishangaza moyo, **dada** yangu, bibi arusi, umenishangaza moyo, kwa mtupo mmoja wa macho yako, kwa mkufu mmoja wa shingo yako.”

**Mfano wa 6 (brother)**

Nomino hii imetumika mara moja pekee katika matini chasili; yaani katika sura ya nane mstari wa kwanza (8:1). Katika mfano huu, nomino hii inadhihirisha jinsia ya kiume. Tazama mfano ufuatao:

***Song of Songs 8:1***

“O that thou wert as my **brother**, that sucked the breasts of my mother! when I should find thee without, I would kiss thee; yea, I should not be despised.”

***Wimbo Ulio Bora 8:1***

“Laiti ungekuwa kama **ndugu** yangu, aliyeyanyonya matiti ya mamangu! Kama ningekukuta huko nje, ningekubusu, asinidharau mtu.”

Katika matini lengwa nomino hii imetafsiriwa kama ndugu, hali inayoifanya nomino hii kutoakisi jinsia ya kiume kama ilivyo kwenye matini chasili. Hali hii kwa mujibu wa nadharia ya tafsiri ya masuala mahususi za kitamaduni inatokana na uhalisia kwamba, japo neno kaka linaweza kutumika katika mukatdha husika na kuakisi jinsia ya kiume kama ilivyo kwenye matini lengwa, mtafsiri anaonekana kushawishiwa na kani kuwa busu kati ya maumbu ni tendo ambalo utamaduni lengwa haukubali. Kwa sababu hiyo, mtafsiri akahiari kutumia neno ‘ndugu’ ambalo haliakisi uhusiano wa karibu kama ‘kaka’.

**2.2 Virai nomino**

Virai nomino kwa mujibu wa Matei (2011), ni aina ya kirai ambacho kichwa chake ni nomino. Katika kitabu cha Song of Songs, virai nomino mbalimbali vimetumika kuashiria jinsia mbalimbali. Tazama mifano ifuatayo:

**Mfano wa 1 (daughters of Jerusalem)**

Kirai ‘Daughters of Jerusalem’ kimetumika saba katika *Song of Songs*; yaani katika sura ya kwanza mstari wa tano (1:5), sura ya pili msari was aba (2:7), sura ya tatu mstari wa tano (3:5), sura ya tatu mstari wa kumi (3:10), sura ya tano mstari wa nane (5:8), sura ya tano mstari wa kumi na sita (5:16) pamoja na sura ya nane mstari wa nne (8:4). Kirai hiki katika matini chasili kinadokeza jinsia ya kike. Aidha tafsiri yake katika matini lengwa ‘binti za Yerusalemu’ pia

inaashiria jinsia ya kike. Ulinganifu huu wa kirai hiki katika matini chanzi na matini lengwa katika uashiriaji wa masuala ya uana, hasa jinsia ya kike kwa mujibu wa nadharia ya tafsiri ya masuala mahususi ya kitamaduni unatoka na dhana ‘daughter’ kuwepo katika lugha zote husika (Kiswahili na Kiingereza). Tazama mifano ifuatayo:

***Song of Songs 1:5***

“I am black, but comely, O ye **daughters of Jerusalem**, as the tents of Kedar, as the curtains of Solomon.”

***Wimbo Ulio Bora 1:5***

“Mimi ni mweusi mweusi, lakini napendeza, enyi **binti za Yerusalemu**, mfano wa hema za Kedari, kama mapazia yake Sulemani.”

***Song of Songs 5:8***

“I charge you, O **daughters of Jerusalem**, if ye find my beloved, that ye tell him, that I am sick of love.”

***Wimbo Ulio Bora 5:8***

“Nawasihi, enyi **binti za Yerusalemu**, ninyi mkimwona mpendwa wangu, ni nini mtakayomwambia? Ya kwamba nazimia kwa mapenzi!”

***Song of Songs 8:4***

“I charge you, O **daughters of Jerusalem**, that ye stir not up, nor awake my love, until he please.”

***Wimbo Ulio Bora 8:4***

“Nawasihi, enyi **binti za Yerusalemu**, msiyachochee mapenzi, au kuyaamsha, hadi yatakapokuwa tayari.”

***Song of Songs 3:10***

“He made the pillars thereof of silver, the bottom thereof of gold, the covering of it of purple, the midst thereof being paved with love, for the **daughters of Jerusalem**.”

***Wimbo Ulio Bora 3:10***

“Nguzo zake alizitengeneza za fedha, na mgongo wake wa dhahabu, kiti chake kimepambwa urujuani, gari lake limenakishiwa njumu, hiba ya **binti za Yerusalemu**.”

**Mfano wa 2 (mother’s children)**

Kirai hiki kimetumika mara moja pekee katika matini chasili; katika sura ya kwanza mstari wa sita (1:6). Tazama mfano ufuatao:

***Song of Songs 1:6***

“Look not upon me, because I am black, because the sun hath looked upon me: my **mother's children** were angry with me;

they made me the keeper of the vineyards; but mine own vineyard have I not kept.”

**Wimbo Ulio Bora 1:6**

“Msinichunguze kwa kuwa ni mweusi mweusi, kwa sababu jua limeniunguza. **Wana wa mamangu** walinikasirikia, waliniweka niwe mlinzi wa mashamba ya mizabibu; bali shamba langu mwenyewe sikulilinda.”

Katika kirai hiki ‘mother’s children’ katika matini chasili, jinsia ya kike inadokezwa. Tafsiri ya kirai hiki katika lugha ya Kiswahili, ‘wana wa mama’ pia inadhihirisha ulinganifu katika urejeaji wa kijinsia kati ya matini mbili husika. Kwa mujibu wa nadharia ya tafsiri ya masuala mahususi ya kitamaduni, ulinganifu huu unatokea kwa sababu dhana hii inapatikana katika lugha zote.

**Mfano wa 3 (mother’s house)**

Kirai hiki ‘mother’s house’ kimejitokeza mara mbili kwenye kitabu *Song Of Songs* kikitafiriisha jinsia ya kike; sura ya tatu mstari wa nne (3:4) pamoja na sura ya nane mstari wa pili (8:2). Tazama mifano ifuatayo:

**Song of Songs 3:4**

“It was but a little that I passed from them, but I found him whom my soul loveth: I held him, and would not let him go, until I had brought him into my **mother's house**, and into the chamber of her that conceived me.”

**Wimbo Ulio Bora 3:4**

“Kitambo kidogo tu nilipoachana nao, nikamwona mpendwa wa nafsi yangu; nikamshika, nisimwache tena, hata nilipomleta **nyumbani mwa mamangu**, chumbani mwake aliyenizaa.”

**Song of Songs 8:2**

“I would lead thee, and bring thee into my **mother's house**, who would instruct me: I would cause thee to drink of spiced wine of the juice of my pomegranate.”

**Wimbo Ulio Bora 8:2**

“Ningekuongoza **nyumbani mwa mamangu**, naye angenifundisha; ningekunyweshwa divai iliyokolea, divai mpya ya mkomamanga wangu.”

Katika mifano hii miwili, kirai ‘mother’s house’ kinaakisi jinsia ya kike. Kirai hiki kinapohawilishwa hadi lugha ya Kiswahili katika *Wimbo Ulio Bora*, kunadhihirika ulinganifu katika kuakisi jinsia ya kike. Hali hii kwa mujibu wa nadharia tafsiri ya masuala mahususi ya kitamaduni inatokana na lugha mbili husika kuwa na dhana husika na hivyo uhawilishaji huo

ukadhihirisha uana katika matini zote. Hata hivyo mpangilia wa kisintaksia katika kirai hiki kati ya matini mbili husika unatofautiana kwa sababu ya tofauti za kisintaksia kati ya lugha mbili husika ambapo kivumishi kinatangulia nomino katika lugha chanzi huku kivumishi kikija baada ya nomino katika lugha lengwa.

#### **Mfano wa 4 (her mother)**

Kirai hiki kimetumika mara moja pekee katika matini chasili; katika sura ya sita mstari wa tisa.

Tazama mfano huu:

##### ***Song of Songs 6:9***

“My dove, my undefiled is but one; she is the only one of **her mother**, she is the choice one of her that bare her. The daughters saw her, and blessed her; yea, the queens and the concubines, and they praised her.”

##### ***Wimbo Ulio Bora 6:9***

“Hua wangu, mkamilifu wangu, ni mmoja tu, mtoto wa pekee wa **mamaye**. Ndiye kipenzi chake aliyemzaa, binti wakamwona wakamwita heri; malkia na masuria nao wakamwona, wakamsifu, wakisema,”

Katika mfano huu, kirai the only one of ‘**her mother**’ kinaakisi jinsia ya kike. Hata hivyo, katika matini lengwa kirai hiki kimetafsiriwa kama mtoto wa pekee wa ‘**mamaye**’. Japo tafsiri hii inadhihirisha jinsia ya kike kama ilivyo kwenye matini chasili, inadhihirika kama tafsiri iliyofanywa kwa kufupisha maneno mawili ya kirai husika kuwa neno moja.

#### **Mfano wa 5 (my brother)**

Kirai hiki kimetumika mara moja pekee katika matini chasili; yaani katika sura ya nane mstari wa kwanza (8:1). Tazama mfano ufuatao:

##### ***Song of Songs 8:1***

“O that thou wert as **my brother**, that sucked the breasts of my mother! when I should find thee without, I would kiss thee; yea, I should not be despised.”

##### ***Wimbo Ulio Bora 8:1***

“Laiti ungekuwa kama **ndugu yangu**, aliyeyanyonya matiti ya mamangu! Kama ningekukuta huko nje, ningekubusu, asinidharau mtu.”

Katika mfano huu, kirai nomino ‘**my brother**’ ambacho kimetafsiriwa katika matini lengwa kama ‘**ngugu yangu**, kinadhihirisha ukosefu wa ulinganifu katika uakisiaji wa masuala ya uana katika matini zote. Hii ni kwa sababu kirai ‘ndugu yangu’ hakiakisi jinsia ya kiume kama ilivyo katika matini lchanzi. Kwa mujibu wa nadharia ya tafsiri ya masuala mahususi ya

kitamaduni, hali hii inatokana na uhalisia kuwa urejeleaji huu wa kijinsia, japo unapatikana katika lugha zote, utamaduni lengwa haukubali tendo la busu kati ya maumbu.

### **Mfano wa 6 ( little sister)**

Kirai hiki kimetumika mara moja tu katika matini chasili; katika sura ya nane mstari wa nane (8:8)

#### *Song of Songs 8:8*

“We have a **little sister**, and she hath no breasts: what shall we do for our sister in the day when she shall be spoken for?”

#### *Wimbo Ulio Bora 8:8*

“Kwetu sisi tuna **dada mdogo**, wala hana matiti; tumfanyieje dada yetu, siku atakapoposwa?”

Kirai nomino ‘**little sister**’ ambacho kimetafsiriwa kama ‘**dada mdogo**’ katika matini lengwa kinadhihirisha kujitokeza kwa lugha ya kijinsia kati ya matini mbili husika. Hali hii kwa mujibu wa nadharia ya Newmark ya tafsiri ya masuala mahususi ya kitamaduni inatokana na uhalisia kuwa dhana husika zipo katika lugha chanzi na pia lugha lengwa.

### **Mfano wa 7 (prince’s daughter)**

Kirai hiki kimetumika mara moja pekee katika matini chasili *Song of Songs*; yaani, katika sura ya saba mstari wa kwanza (7:1).

#### *Song of Songs 7:1*

“How beautiful are thy feet with shoes, O **prince's daughter!** the joints of thy thighs are like jewels, the work of the hands of a cunning workman.”

#### *Wimbo Ulio Bora 7:1*

“**Binti wa kimalkia**, jinsi ulivyo mzuri hatua zako katika mitarawanda. Mapaja yako ya mviringo ni kama johari, kazi ya mikono ya fundi stadi;”

Katika mfano huu, urejeleaji wa jinsia ya kike umejitokeza katika matini chanzi na vilevile katika matini lengwa. Hata hivyo, kirai hiki kina maana ya ‘binti wa mtoto wa mfalme’ na hivyo kutafsiriwa kama ‘binti wa kifalme’ kumejumuisha maana husika sana. Pamoja na masuala haya, tafsiri hii inaibua masuala zaidi ya kitafsiri. Kwa mfano, mpangilio wa kisintaksia katika kirai hiki katika matini chanzi ambapo kivumishi kinakuja kabla ya nomino unatofautiana na ule wa matini lengwa ambapo kivumishi kinakuja baada ya nomino.

Kimsingi, mjadala wetu hapa juu unadhihirisha kuwa nomino na virai nomino katika kitabu cha *Song of Songs*, ni kiunzi muhimu cha kuakisi jinsia. Hii ni kwa sababu nomino na virai hivyo vimeakisi jinsia ya kiume na vilevile ya kike. Hata hivyo katika michakato ya kuhawilisha nomino na virai hivi kutoka *Song of Songs* hadi *Wimbo Ulio Bora*, kumbainika kuwepo kwa kiasi kikubwa cha hali ya kutojitokeza kwa ujielezaji kijinsia katika *Wimbo Ulio Bora*. Hali hii kwa mujibu wa nadharia ya tafsiri ya masuala mahususi ya kitamaduni huhusishwa na tofauti kati ya lugha mbili husika katika kuakisi masuala ya kijinsia kupitia kwa baadhi ya nomino jumla na baadhi ya virai nomino.

### 2.3 Viwakilishi

Mgullu (1999) anaeleza viwakilishi kama “Maneno ambayo yanatumiwa badala ya nomino” . Mawazo haya yanawiana na ya Matei (2014) anaeleza kiwakilishi kama, “neni au fungu la maneno au kiambishi ambacho hutumiwa badala ya nomino. Anaongeza kuwa kiwakilishi huchukua nafasi ya nomino au kirai nomino katika sentensi.” Vilevile, mtaalamu huyu anahoji kuwa kiwakilishi hufanya kazi ya nomino, na kinapotumiwa nomino haitumiwi hapo. Hivi ni kumaanisha ya kuwa kiwakilishi ni kibadala cha nomino kinachotumiwa wakati nomino inayowakilishwa haipo katika sentensi husika. Mtaalamu huyu anaainisha aina kumi na moja za viwakilishi. Hata hivyo, kwa ajili ya kazi hii, tutajikita katika aina tatu pekee za viwakilishi na kuonyesha jinsi ambavyo aina hizo zimejitokeza katika kitabu cha *Song of Songs*.

#### 2.3.1 Viwakilishi vya nafsi

Kulingana na Matei (2014), hivi ni viwakilishi ambavyo husimamia nomino ambazo ni majina ya watu au wanyama. Anahoji kuwa viwakilishi hivi hudhihirika katika aina mbili; viwakilishi vya nafsi huru na viwakilishi vya nafsi viambata. Anaeleza (Matei, 2014) kuwa viwakilishi vya nafsi huru ni maneno mazima ambayo yanatumiwa badala ya watu au wanyama. Kwa upande mwingine, mtaalamu huyu anaeleza viwakilishi vya nafsi viambata kama viambishi vinavyoambikwa kwenye mzizi wa kitenzi kuwakilisha nomino ama kiwakilishi huru kilichotajwa awali, ama ambacho hakikutajwa awali. Anasema kuwa viwakilishi hivi vinaweza kuashiria mtenda au yambwa. Kwa mfano:

Ninasoma kitabu cha fasihi. (**ni** – kiwakilishi cha mtenda)

Amempikia mtoto chai. (**m**- kiwakilishi cha yambwa)



### 2.3.1.1 Viwakilishi vya nafsi mtenda

Viwakilishi hivi huwakilisha kwa kudokeza nafsi. Viwakilishi hivi pia huweza kuakisi jinsia katika matumizi yake. Tazama mifano ifuatayo.

#### Mfano wa 1 (he)

Kiwakilishi hiki 'he' kimedhihirika mara kumi na moja katika kitabu hiki cha *Song of Songs* ambapo kimeibua masuala mbalimbali ya kitafsiri, hali zote hizo zikidhihirisha jinsia ya kiume. Mifano hiyo ni kama vile katika sura ya kwanza mstari wa kumi na tatu (1:13), sura ya pili mstari wa nne (2:4), sura ya pili mstari wa nane (2:8), sura ya pili mstari wa tisa (2:9), sura ya pili mstari wa kumi na sita (2:16), sura ya tatu mstari wa kumi (3:10), sura ya tano mstari wa sita (5:6), sura ya sita mstari wa tatu (6:3) pamoja na sura ya nane mstari wa kumi na moja (8:11). Tazama mifano ifuatayo:

#### *Song of Songs 2:8*

“The voice of my beloved! behold, he cometh leaping upon the mountains, skipping upon the hills.”

#### *Wimbo Ulio Bora 2:8*

“Sikiliza! Ni mpendwa wangu! Tazama, anakuja, akiruka milimani, akichachawa vilimani.”

#### *Song of Songs 5:6*

“I opened to my beloved; but my beloved had withdrawn himself, and was gone: my soul failed when he spake: I sought him, but I could not find him; I called him, but he gave me no answer.”

#### *Wimbo Ulio Bora 5:6*

“Nilimfungulia mpendwa wangu, lakini mpendwa wangu amegeuka amepita; (Nimezimia nafsi yangu aliponena), nikamtafuta, nisimpate, nikamwita, asiniitikie.”

#### *Song of Songs 2:9*

“My beloved is like a roe or a young hart: behold, he standeth behind our wall, he looketh forth at the windows, shewing himself through the lattice.”

#### *Wimbo Ulio Bora 2:9*

“Mpendwa wangu ni kama paa, au ayala. Tazama, asimama nyuma ya ukuta wetu, achungulia dirishani, atazama kimiani.”

#### *Song of Songs 3:10*

“He made the pillars thereof of silver, the bottom thereof of gold, the covering of it of purple, the midst thereof being paved with love, for the daughters of Jerusalem.”

***Wimbo Ulio Bora 3:10***

“Nguzo zake alizitengeneza za fedha, na mgongo wake wa dhahabu, kiti chake kimepambwa urujuani, gari lake limenakishiwa njumu, hiba ya binti za Yerusalemu.”

Katika mifano hii, mambo mawili yanadhihirika. Kwanza kiwakilishi hiki ambacho ni neno zima ‘he’ katika matini chanzi, kimechukua umbo la kiambishi {a-} katika matini lengwa. Jambo la pili ni kuwa, jinsia ya kiume inayoakisiwa na kiwakilishi hiki katika matini chanzi haidhihiriki katika matini lengwa. Kutodhihirika huku kwa masuala ya uana katika matini lengwa kwa mujibu wa nadharia ya tafsiri ya masuala mahususi ya kitamaduni huweza kuhusishwa na lugha lengwa kutokuwa na viwakilishi vya sampuli hii, vinavyodokeza jinsia katika lugha lengwa.

**Mfano wa 2 (she)**

Kiwakilishi hiki (she) kimejitokeza katika matini chanzi mara nane ambazo ni katika sura ya sita mstari wa tisa (6:9) mara mbili, dura ya sita mstari wa kumi (6:10), sura ya nane mstari wa tano (8:5), sura ya nane mstari wa nane (8:8) mara mbili pamoja na sura ya nane mstari wa tisa (8:9). Katika mifano yote hii, kiwakilishi hiki kinadokeza jinsia ya kike katika matini chanzi. Hata hivyo, japo hali hii inadhihirika katika matini chanzi, kinapohawilishwa hadi matini lengwa, masuala mbalimbali ya kitafsiri huibuka Tazama mfano ufuatao:

***Song of Songs 8:8***

“We have a little sister, and she hath no breasts: what shall we do for our sister in the day when she shall be spoken for?”

***Wimbo Ulio Bora 8:8***

“Kwetu sisi tuna dada mdogo, wala **hana** matiti; tumfanyieje dada yetu, siku atakapoposwa?”

Katika mfano huu, kiwakilishi ‘she’ kinaakisi jinsia ya kike. Hata hivyo, katika matini lengwa, jinsia hiyo haijitokezi. Hali hii kwa mujibu wa nadharia ya tafsiri ya masuala mahususi ya kitamaduni ni kwa sababu lugha lengwa haina uashiriaji wa kijinsia kutumia viwakilishi husika. Pamoja na haya, kiwakilishi hiki kimeambatanishwa na ukanushaji unaojitokeza kwenye muktadha wa kutokea kwake katika matini asilia, ambapo fungu ‘she has no breasts’ limetafsiriwa kama ‘hana matini’. Hali hii inaondosha katika matini lengwa uashiriaji wa kijinsia unaojitokeza katika matini chasili. Pamoja na mfano huu, kuna mifano mingine ambapo kiwakilishi hiki kimetafsiriwa kwa kiambishi {a}. Tazama mifano ifuatayo.

***Song of Songs 8:9***

“If **she** be a wall, we will build upon her a palace of silver: and if **she** be a door, we will inclose her with boards of cedar.”

***Wimbo Ulio Bora 8:9***

“Kama **a**kiwa tu ukuta, tumjengee buruji za fedha; na kama **a**kiwa ni mlango, tumhifadhi kwa mbao za mierezi.”

***Song of Songs 8:5***

“Who is this that cometh up from the wilderness, leaning upon her beloved? I raised thee up under the apple tree: there thy mother brought thee forth: there **she** brought thee forth that bare thee.”

***Wimbo Ulio Bora 8:5***

“Ni nani huyu apandaye kutoka nyikani, akimtegemea mpendwa wake? Nilikuamsha chini ya huo mpera; huko mama yako alikuonea uchungu, **a**liona uchungu aliyekuzaa.”

***Song of Songs 6:10***

“Who is **she** that looketh forth as the morning, fair as the moon, clear as the sun, and terrible as an army with banners?”

***Wimbo Ulio Bora 6:10***

“Ni nani huyu **a**tazamaye kama alfajiri, mzuri kama mwezi, safi kama jua, wa kutisha kama wenye bendera?”

Katika mifano yote hii, kiwakilishi hiki ‘**she**’ kimetumika katika matini asilia kuakisi jinsia ya kike. Ijapokuwa jinsia ya kike inadhihirika wazi katika *Song of Songs*, suala hili la uana linakosekana kabisa katika tafsiri ya *Song of Songs* katika lugha ya Kiswahili, *Wimbo Ulio Bora* ambapo kiwakilishi hiki kmetafsiriwa kwa kiambishi {a}. Sawa na kiwakilishi ‘**he**’ ambacho kinaakisi jinsia ya kiume, kiwakilishi ‘**she**’ pia kinakosekana katika *Wimbo Ulio Bora* kwa sababu kwa mujibu wa unadharia ya tafsiri ya masuala mahususi ya kitamaduni, lugha lengwa, yaani Kiswahili hakina uashiriaji wa kijinsia kwa kutumia viwakilishi husika.

Katika kitabu cha *Song of Songs*, viwakilishi hivi vimechukua maumbo mawili, ambayo ni ‘**he**’ na ‘**she**’, vyote vikiwa vinadokeza jinsia ya kiume na ya kike mtawalia. Uchunguzi wetu uliweza kubaini kuwa jinsia zote mbili; ya kike na ya kiume ambazo zinaakisiwa na viwakilishi hivi katika matini chasili *Song of Songs*, hazidhihiriki katika matini lengwa, *Wimbo Ulio Bora*. Hivi ni kumaanisha kuwa viwakilishi vya mtenda vinavyoakisi jinsia vinakosekana katika lugha ya Kiswahili na badala ya maneno haya mazima, viwakilishi hivi vinadhihirika kupitia kwa kiambishi {a}.

### 2.3.1.2 Viwakilishi vya nafsi yambwa

Kuna viwakilishi ambavyo vinawakilisha kwa kudokeza yambwa. Kulingana na Matei (2011), ni nomino katika au kiwakilishi ambao hupoke kitendo katika sentensi. Katika kitabu cha *Song of Songs*, viwakilishi hivi vimedokeza jinsia kupitia maumbo mawili ambayo ni ‘him’ pamoja na ‘her’ vyote vikiashiria jinsia ya kiume na ya kike mtawalia. Tazama mifano ifuatayo:

#### Mfano wa 1 (him)

Kiwakilishi hiki ‘**him**’ kimetumika katika kitabu cha *Song of Songs* kikidokeza yambwa na vilevile kuashiria jinsia ya kiume. Kiwakilishi hiki kimejitokeza katika matini chanzi mara kumi na saba ambapo ni mara tatu katika sura ya tatu mstari wa kwanza (3:1), mara tatu katika sura ya tatu mstari wa pili (3:2), sura ya tatu mstari wa tatu (3:3), mara nne katika sura ya tau mstari wa nne (3:4), sura ta tatu mstari wa kumi na moja (3:11), mara tatu katika sura ya tano mstari wa sita (5:6), sura ya tano mstari wa nane (5:8) pamoja na sura ya sita mstari wa kwanza (6:1). Katika kujitokeza huku, kiwakilishi hiki kimeibua masuala mbalimbali ya kitafsiri. Kwa mfano, kuna zile hali ambazo kiwakilishi hiki kimetafsiriwa kwa kiambishi {m}. Tazama mifano ifuatayo:

#### *Song of Songs 3:1*

“By night on my bed I sought **him** whom my soul loveth: I sought **him**, but I found **him** not.”

#### *Wimbo Ulio Bora 3:1*

“Usiku kitandani nili**mt**afuta mpendwa wa nafsi yangu, nili**mt**afuta, nisi**mp**ate.”

#### *Song of Songs 5:8*

“I charge you, O daughters of Jerusalem, if ye find my beloved, that ye tell **him**, that I am sick of love.”

#### *Wimbo Ulio Bora 5:8*

“Nawasihi, enyi binti za Yerusalemu, ninyi mkimwona mpendwa wangu, ni nini mtakayo**m**wambia? Ya kwamba nazimia kwa mapenzi.”

#### *Song of Songs 3:2*

“I will rise now, and go about the city in the streets, and in the broad ways I will seek **him** whom my soul loveth: I sought **him**, but I found **him** not.”

#### *Wimbo Ulio Bora 3:2*

“Nikasema, Haya, niondoke nizunguke mjini, katika njia zake na viwanjani, ni**mt**afute mpendwa wa nafsi yangu. Ni**ka****mt**afuta, nisi**mp**ate.”

Kiwakilishi hiki (him) ambacho ni neno zima na ambacho kinaakisi jinsia ya kiume, kinachukua umbo la kiambishi [-m-] tu katika matini lengwa. Ruwaza hii ya kutafsiri kiwakilishi hiki cha yambwa kwa umbo la kiambishi kwa mujibu wa nadharia ya tafsiri ya masuala mahususi za kitamaduni kinatokana na uhalisia kuwa lugha lengwa inakosa uashiriaji wa kijinsia kupitia kwa kiambishi husika.

Pamoja na ruwaza iliyoshuhudiwa katika mifano ya hapo juu, kuna hali ambapo kiwakilishi hiki kimedondoshwa katika matini lengwa. Tazama mfano ufuatao:

***Song of Songs 3:11***

“Go forth, O ye daughters of Zion, and behold king Solomon with the crown wherewith his mother crowned **him** in the day of his espousals, and in the day of the gladness of his heart.”

***Wimbo Ulio Bora 3:11***

“Tokeni, enyi binti za Sayuni, mtazameni Mfalme Sulemani, amevaa taji alilovikwa na mamaye, siku ya posa yake, siku ya furaha ya moyo wake.”

**Mfano wa 2 (her)**

Kiwakilishi hiki ‘**her**’ kimejitokeza mara nne katika kitabu cha *Song of Songs* ambapo ni mra tatu katika sura ya sita mstari wa tisa (6:9) pamoja na sura ya nane mstari wa tisa (8:9) . Tazama mifano ifuatayo:

***Song of Songs 6:9***

“My dove, my undefiled is but one; she is the only one of her mother, she is the choice one of her that bare **her**. The daughters saw **her**, and blessed **her**; yea, the queens and the concubines, and they praised **her**.”

***Wimbo Ulio Bora 6:9***

“Hua wangu, mkamilifu wangu, ni mmoja tu, Mtoto wa pekee wa mamaye. Ndiye kipenzi chake aliyem<sub>u</sub>zaa, binti wakam<sub>w</sub>wona wakam<sub>w</sub>wita heri; malkia na masuria nao wakam<sub>w</sub>wona, wakam<sub>s</sub>sifu, wakisema,”

***Song of Songs 8:9***

“If she be a wall, we will build upon **her** a palace of silver: and if she be a door, we will inclose **her** with boards of cedar.”

***Wimbo Ulio Bora 8:9***

“Kama akiwa tu ukuta, tum<sub>j</sub>jengee buruji za fedha; na kama akiwa ni mlango, tum<sub>h</sub>hifadhi kwa mbao za mierezi.”

Katika mifano hii yote, kiwakilishi hiki ‘her’ kimetumika katika matini chanzi kikiashiria jinsia ya kike. Hata hivyo katika matini lengwa, kiwakilishi hiki ambacho katika matini chanzi ni neno zima, kinachukua umbo la kiambishi [-m-]. Pamoja na haya, uashiriaji wa uana unaojitokeza wazi katika matini chanzi kupitia kiwakilishi hiki unapotea kabisa katika matini lengwa. Ukosefu huu wa ulinganifu wa uashiriaji wa kijinsia kwa mujibu wa nadharia ya tafsiri ya masuala mahususi ya kitamaduni unatokana na uhalisia kuwa lugha lengwa inakosa uashiriaji wa kijinsia kupitia kiwakilishi cha yambwa ‘her’.

### 2.3.2 Viwakilishi vimilikishi

Matei (2014) anasema kuwa viwakilishi vimilikishi ni viwakilishi ambavyo husimama mahali pa nomino ambayo imemilikiwa na mtu. Kwa mfano:

**Chake** kimevunjika.

Katika mfano huu, neno **chake** ni kiwakilishi kimilikishi. Katika kitabu tulichokirejelea cha *Song of Songs*, viwakilishi hivi vimetumika kudhihirisha uana. Vimilikishi hivi vimedhihirisha jinsia ya kike na ya kiume.

#### 2.3.2.1 Vimilikishi vinavyodokeza jinsia ya kike

Kimilikishi ‘her’ kimetumika mara tatu katika kitabu cha *Song of Songs* kikidokeza jinsia ya kike. Kimejitokeza katika sura ya sita mstari wa tisa (6:9), sura ya nane mstari wa tano (8:5) pamoja na sura ya pili mstari wa kumi na tatu (2:13). Tazama mifano ifuatayo:

##### *Song of Songs 6:9*

“My dove, my undefiled is but one; she is the only one of **her** mother, she is the choice one of her that bare her. The daughters saw her, and blessed her; yea, the queens and the concubines, and they praised her.”

##### *Wimbo Ulio Bora 6:9*

“Hua wangu, mkamilifu wangu, ni mmoja tu, mtoto wa pekee wa mamaye. Ndiye kipenzi chake aliyemzaa, binti wakamwona wakamwita heri; malkia na masuria nao wakamwona, makamsifu, wakisema,”

##### *Song of Songs 8:5*

“Who is this that cometh up from the wilderness, leaning upon **her** beloved? I raised thee up under the apple tree: there thy mother brought thee forth: there she brought thee forth that bare thee.”

***Wimbo Ulio Bora 8:5***

“Ni nani huyu apandaye kutoka nyikani, akimtegemea mpendwa wake? Nilikuamsha chini ya huo mpera; huko mama yako alikuonea uchungu, aliona uchungu aliyekuzaa.”

***Song of Songs 2:13***

“The fig tree putteth forth her green figs, and the vines with the tender grape give a good.”

***Wimbo Ulio Bora 2:13***

“Mtini wapevusha tini zake, na mizabibu inachanua, inatoa harufu yake nzuri; ondoka, mpenzi wangu, mzuri wangu, uje zako.”

Katika mifano hii, kimilikishi ‘her’ kinadhihirisha jinsia ya kike katika matini chanzi. Hata hivyo, mfano wa kwanza (6:9) katika matini lengwa, kiwakilishi hiki kimechukua umbo [-ye] ambacho ni kifupisho cha ‘yake’ kama vile katika mfano ‘mama yake’ (mamaye). Hali hii inasababisha kutojitokeza kwa ulinganifu wa uashiraji wa kijinsia kati ya matini mbili husika. Katika mifano inayosalia kimilikishi hiki kimetafsiriwa kwa {-ake} katika matini lengwa. Tafsiri ya kiwakilishi hiki kinadhihirisha ukosefu wa uashiraji wa kijinsia katika matini mbili husika. Hali hii kwa mujibu wa nadharia ya tafsiri ya masuala mahususi ya kitamaduni inatokana na lugha lengwa kukosa uashiraji wa kijinsia kupitia kiwakilishi hiki.

### **2.3.2.2 Vimilikishi vinavyodokeza jinsia ya kiume**

Vimilikishi vilevile vimetumika katika kitabu cha *Song of Songs* kudhihirisha jinsia ya kiume. Kiwakilishi hiki ‘his’ ambacho kinadokeza jinsia ya kiume kimejitokeza mara nyingi katika matini chanzi kuliko kiwakilishi [her] ambacho kinadokeza jinsia ya kike. Kwa mfano kimejitokeza mara thelathini na nne (34) kama vile katika sura ya kwanza mtari wa pili (1:2), sura ya kwanza mstari wa nne (1:4), sura ya kwanza mstari wa kumi na mbili (1:12), mara mbili katika sura ya pili mstari wa tatu (2:3), sura ya pili mstari wa nne (1:4), mara mbili katika sura ya pili mstari wa sita (2:6), sura ya pili mstari wa kumi na sita (2:16), sura ya tatu msatri wa saba (3:7), mara mbili katika sura ya tatu mstari wa nane (3:8), mara tatu katika sura ya tatu mstari wa kumi na moja (3:11), mara mbili katika sura ya nne mstari wa kumi na sita (4:16), sura ya tano mstari wa nne (5:4), mara mbili katika sura ya tano mstari wa kumi na moja (5:11), sura ya tano mstari wa kumi na mbili (5:12), mara mbili katika sura ya tano mstari wa kumi na tatu (5:13), mara mbili katika sura ya tano mstari wa kumi na nne (5:14), mara mbili katika sura ya tano mstari wa kumi na tano (5:15), sura ya tano mstari wa kumi na sita (5:16), sura ya sita mstari wa pili (6:2), sura ya saba mstari wa kumi (7:10), mara mbili katika sura ya

nane mstari wa tatu (8:3), sura ya nane mstari wa saba (8:7) pamoja na sura ya nane mstari wa kumi (8:10). Hii inaweza kusemekana kuwa inatokana na ukweli kwamba wahusika wa jinsia ya kike ambao ni mpenziwe mfalme pamoja na mabinti wa Yerusalemu wameshamiri katika mazungumzo yanayoendelea katika kitabu cha *Song of Songs* kuliko mhusika wa kiume. Kimilikishi hiki kimetafsiriwa katika matini lengwa kikidhihirisha masuala mbalimbali ya kitafsiri. Kwa mfano, kuna hali ambapo kiwakilishi hiki kinadondoshwa katika matini lengwa. Tazama mfano ufuatao:

*Song of Songs 1:12*

“While the king sitteth at **his** table, my spikenard sendeth forth the smell thereof.”

*Wimbo Ulio Bora 1:12*

“Muda mfalme alipoketi juu ya kochi, nardo yangu ilitoa harufu yake.”

Katika mfano huu, kimilikishi ‘**his**’ kinadokeza jinsia ya kiume katika matini chasili. Hata hivyo, katika matini lengwa, kimilikishi hiki kimedondoshwa kabisa na hivyo kusababisha ukosefu wa ulinganifu wa uashiriaji wa kijinsia kati ya matini lengwa na matini chasili. Katika mifano inayosalia, kiwakilishi hiki kimetafsiriwa kupitia kwa umbo {-ake-}. Tazama mifano ifuatayo:

*Song of Songs 2:6*

“**His** left hand is under my head, and his right hand doth embrace me.”

*Wimbo Ulio Bora 2:6*

“Mkono **wake** wa kushoto uko chini ya kichwa changu, nao wa kulia unanikumbatia!”

*Song of Songs 2:16*

“My beloved is mine, and I am **his**: he feedeth among the lilies.”

*Wimbo Ulio Bora 2:16*

“Mpendwa wangu ni wangu, na mimi ni **wake**; hulisha kundi lake penye nyinyoro.”

Katika mifano yote hii, ambapo panadhahirika mwelekeo wa kutafsiri kiwakilishi [his] kupitia kwa umbo [-ake] panajitokeza ukosefu wa ulinganifu wa uashiriaji wa kijinsia kupitia kwa kimilikishi hiki. Hali hii kwa mujibu wa nadharia ya tafsiri ya masuala mahususi ya kitamaduni inatokana na lugha lengwa kukosa uashiriaji wa jinsia ya kiume kupitia kwa kimilikishi husika.



### 2.3.2.3 Viwakilishi virejeshi

Kiwakilishi kirejeshi ‘himself’ kimetumika mara tatu katika kitabu cha *Song of Songs*. Kwa mfano katika sura ya pili mstari wa tisa (2:9), sura ya tatu mstari wa tisa (3:9) pamoja na sura tano mstari wa sita (5:6). Katika mifano hii, kuna hali ambapo kiwakilishi hiki kimedondoshwa. Tazama mifano ifuatayo:

#### *Song of Songs 2:9*

“My beloved is like a roe or a young hart: behold, he standeth behind our wall, he looketh forth at the windows, shewing himself through the lattice.”

#### *Wimbo Ulio Bora 2:9*

“Mpendwa wangu ni kama paa, au ayala. Tazama, asimama nyuma ya ukuta wetu, achungulia dirishani, atazama kimiani.”

#### *Song of Songs 5:6*

“I opened to my beloved; but my beloved had withdrawn himself, and was gone: my soul failed when he spake: I sought him, but I could not find him; I called him, but he gave me no answer.”

#### *Wimbo Ulio Bora 5:6*

“Nilimfungulia mpendwa wangu, lakini mpendwa wangu amegeuka amepita; (Nimezimia nafsi yangu aliponena), nikamtafuta, nisimpate, nikamwita, asiniitikie.”

Pamoja na mifano hii inayodhihirisha kudondoshwa kwa kiwakilishi hiki katika matini lengwa, kuna hali ambapo kiwakilishi hiki kimetafsiriwa kwa kutmia kiambishi {ji}. Tazama mfano huu:

#### *Song of Songs 3:9*

“King Solomon made himself a chariot of the wood of Lebanon.”

#### *Wimbo Ulio Bora 3:9*

“Mfalme Sulemani alijiitengenezea machela ya miti ya Lebanoni;”

Kutafsiriwa kwa kiwakilishi hiki kupitia kwa kiambishi {ji} katika matini lengwa kwa mujibu wa nadharia ya tafsiri ya masuala mahususi ya kitamaduni kunatokana na uhalisia kuwa lugha lengwa haina uashiriaji wa kijinsia kupitia kiwakilishi husika.

## 2.4 Vivumishi vinavyoashiria jinsia

Katika matini tuliyoirejelea; *Song of Songs*, kuna vivumishi ambavyo vimetumika vikidhihirisha jinsia. Kwa mujibu wa tafsiri ya King James, kivumishi kinachodhihirika ni kimoja tu ambacho ni ‘beautiful’. Kivumishi hiki kimejitokeza katika matini asilia mara mbili tu ambapo ni katika sura ya sita mstari wa nne (6:4) pamoja na sura ya saba msatri wa kwanza (7:1). Katika mifano hii, kivumishi hiki kinaashiria jinsia ya kike. Tazama mifano ifuatayo:

### *Song of Songs 6:4*

“Thou art **beautiful**, O my love, as Tirzah, comely as Jerusalem, terrible as an army with banners.”

### *Wimbo Ulio Bora 6:4*

“Mpenzi wangu, u **mzuri** kama Tirza, mwenye kupendeza kama Yerusalemu, wa kutisha kama jeshi lenye bendera.”

### *Song of Songs 7:1*

“How **beautiful** are thy feet with shoes, O prince's daughter! the joints of thy thighs are like jewels, the work of the hands of a cunning workman.”

### *Song of Songs 7:1*

“Binti wa kimalkia, jinsi ulivyo **mzuri**, hatua zako katika mitarawanda. Mapaja yako ya mviringo ni kama johari, kazi ya mikono ya fundi stadi;”

Katika kitabu kizima cha Song of Songs, kivumishi hiki beautiful ambacho kinadokeza jinsia ya kike kimejitokeza mara mbili. Katika mara zote hizo, kivumishi hiki kimetafsiriwa katika lugha lengwa kama ‘mzuri’, kivumishi ambacho hakidokezi jinsia yoyote. Katika tafsiri husika, mtafsiri amehiari kutotumia kivumishi **mrembo** ambacho kinahawilisha kivumishi hiki katika lugha lengwa na pia kuakisi jinsia ya kike kama iliyo katika matini chanzi na badala yake kutumia kivumishi **mzuri** ambacho hakihusishwi na jinsia yoyote. Matumizi haya ya neno ‘**mzuri**’ katika tafsiri hii yanaweza kuhusishwa na sababu za kidini ambapo mtafiri alilenga kuashiria uzuri wa kitabia badala ya uzuri wa kimaumbile (urembo). Tafsiri hii kwa hivyo inasababisha hali ya ukosefu wa ulinganifu wa uashiraji wa kijinsia kati ya matini mbili husika.

## 2.5 Mahitimisho

Katika sura hii, tumeshughulika ujitokezaji wa lugha ya kijinsia ambapo tumefanikiwa kudhihirisha kuwa kitabu cha *Song of Songs* ni kitabu ambacho kina msukumo mkubwa wa kujitokeza kwa lugha inayobainisha jinsia ambapo jinsia ya kike na ile ya kiume imebainika wazi. Masuala haya ya kijinsia yamejitokeza katika vitengo mbalimbali kama vile kitengo cha

nomino (wanyama na vilevile watu), viwakilishi na vivumishi. Huku tukiwa tumejikita katika kujitokeza au kutojitokeza kwa lugha inayoakisi uana katika matini lengwa tukiilinganisha na matini chanzi, mambo yafuatayo yamedhihirika. Kwanza, kitabu cha *Wimbo Ulio Bora*, kikilinganishwa na matini yake asilia *Song of Songs* kinadhihirisha kiasi kikubwa cha kutojitokeza kwa lugha inayoashiria jinsia ya kiume na ya kike. Hali hii kwa mujibu wa nadharia ya tafsiri ya masuala mahususi ya kitamaduni inatokana na uhalisia kuwa lugha lengwa inakosa uashiriaji wa kijinsia kupitia vitengo husika tulivyovirejela. Pili, kitengo ambacho kimedhihirisha kiwango kikubwa cha kutojitokeza kwa lugha ya uana ni kile cha viwakilishi ambapo takriban viwakilishi vyote vilivyotumika katika matini chanzi vikichukua umbo tofauti au hata kudondoshwa. Nomino ambazo zinataja wanyama na hata binadamu kijinsia ndizo ambazo zimemeelekea kudhihirisha ulinganifu katika uashiriaji wa masuala uana japo kwa kiwango cha chini au kiwango kidogo tu. Hata hivyo nomino hizo ni chache mno huku hata virai vinavyoelekea kudhihirisha mfanano kati ya matini chanzi na matini lengwa vikidhihirisha mpangilio tofauti kabisa wa kisintaksia. Pamoja na haya, vivumishi vyote vilivyotumika katika matini chanzi vinaonyesha kutojitokeza kwa lugha ya uana kati ya matini mbili husika.

Pamoja na uchanganuzi huu wa masuala ya uana katika matini mbili tulizozirejelea, nadharia ya masuala mahususi ya kitamaduni imetufaa sana katika uchanganuzi huu kwa njia mbili kuu. Kwanza ni kwamba nadharia hii inadai kuwa lugha mbili tofauti zinapotagusana katika miktadha ya tafsiri panaweza kudhihirika kutojitokeza kwa masuala fulani ya kitafsiri, matini mbili husika zinapolinganishwa kwa sababu masuala hayo yanapatikana katika lugha chanzi lakini yanakosekana katika lugha lengwa au mismiati ya kuyatajia masuala hayo yanakosekana katika lugha lengwa. Kwa msingi wa madai haya, tuliweza kung'amua kuwa kutojitokeza kwa kiasi kikubwa kwa lugha ya uana katika matini lengwa *Wimbo Ulio Bora* tukiilinganisha matini hii na matini chanzi *Song of Songs* kunatokana na uhalisia kuwa lugha lengwa ya Kiswahili haibainishi jinsia kama ilivyo lugha chanzi ya Kiingereza. Pili, nadharia pia iliweza kutusaidia kubaini pale ambapo panadhihirika udhaifu katika tafsiri hasa pale ambapo pana istilahi za kudokeza jinsia katika lugha lengwa naye mtafsiri akahiari kutumia misamiati ambayo haiakisi uana bila sababu za kitafsiri.

## SURA YA TATU

### ULINGANIFU WA KITAMATHALI KATIKA *SONG OF SONGS* NA *WIMBO ULIO BORA*

#### 3.0 Utangulizi

Wamitila (2003) anasema kuwa, “Tamathali za usemi ni fungu la maneno au hata neno ambalo limegeuzwa maana yake ya kiurejelezi au asilia na kuwa na maana nyingine”. Maelezo haya ya Wamitila yanaashiria kuwa lugha ya kitamathali ni ile lugha ambayo inadhihirisha ukiushi katika kiwango cha kisemantiki. Maelezo haya ya Wamitila yanawiana na ya Mbatia (2001) ambaye akichukua mwelekeo huo huo wa kueleza tamathali za usemi anasema, “Tamathali ni ukiushi wa kimakusudi wa matumizi ya lugha katika viwango vya maana na mpangilio wa maneno ili kuleta maana mpya au msisitizo”. Maoni haya ya Mbatia yanaashiria kuwa tamathali za usemi ni ukiushi unaodhihirika katika kiwango cha kisintaksia na vilevile kiwango cha kisemantiki. Hata hivyo mtaalamu huyu anaashiria katika maelezo yake kuwa ukiushi huu hata ukidhihirika katika kiwango cha kisemantiki au kisintaksia, malengo yake makuu ni kuibua maana mpya au kuleta msisitizo katika usemi. Maoni ya wataalamu hawa ambayo tunakubaliana nayo yanatupa mwelekeo wa kufasiri lugha ya kitamathali ambao tutautumia katika kazi hii kwamba, lugha ya kitamathali ni lugha ambayo inadhihirisha ukiushi katika viwango vya kisemantiki au vya kisintaksia au vyote na katika katika ukiushi huu, neno au kifungu fulani hutumiwa kwa maana ambayo ni tofauti na maana ya kimsingi.

Ukiushi huu unaodhihirika katika lugha ya kitamathali, huweza kuibua mijadala ya kitafsiri, hasa pale ambapo matini katika lugha moja inapohawilishwa hadi lugha nyingine. Mijadala hii huweza kuibuka kwa kuwa pamoja na ukweli kwamba tamathali hizi huhitaji uelewa wa kimuktadha, pia hukitwa kwenye utamaduni wa lugha chanzi. Tofauti hizi za kimuktadha na kiutamaduni huweza kusababisha hali ambapo matini chanzi inapolinganishwa na matini lengwa, kunadhihirika kujitokeza au kutojitokeza kwa tamathali husika matini mbili ambapo moja ni tafsiri ya nyingine zinapolinganishwa.

Katika sura hii, tulichunguza kujitokeza na vilevile kutojitokeza kwa lugha ya kitamathali katika kitabu cha *Song of Songs* kikilinganishwa na tafsiri yake katika lugha ya Kiswahili, *Wimbo Ulio Bora*. Katika kazi hii tutajifunga katika uchunguzi wa tamathali tatu ambazo ni tashihisi, sitiari pamoja na tashbihi. Ili kuafikia malengo haya, tulitoa ufafanuzi wa kina kuhusu tamathali hizi tatu, kuzitolea mifano maridhawa na kisha kuzilinganisha tamathali hizo katika matini zetu mbili tulizojikita kwazo; *Song of Songs* na *Wimbo Ulio Bora*.

### **3.1 Tashihisi, Tashbihi na Sitiari**

Hapa tulikusudia kutoa maelezo ya tamathali hizi tatu; tashbihi, tashihisi pamoja na sitiari kwa lengo la kutoa mwelekeo utakaotumika kutazama tamathali hizi. Aidha, tulijadili tamathali hizi kwa kutoa mifano ya kijumla pamoja na mifano kutoka kwenye matini tulizorejelea.

#### **3.1.1 Tashbihi**

Istilahi tashbihi imeweza kufasiriwa na wataalamu mbalimbali. Miongoni mwa wataalamu hawa ni Matei (2011) anayefasiri tashbihi kwamba, "... tashbihi ni tamathali ya usemi inayolinganisha vitu kwa kutumia maneno ya kulinganisha kama vile mfano wa, kama na mithili ya". Matei anatoa mifano ifuatayo ya tashbihi:

*Kawaida ni kama sheria.* Anaelezea mfano huu kwa kusema, 'Kawaida imefananishwa na sheria kuonyesha kuwa la kawaida ni kaida.' Yaani jambo analolifanya mtu kwa kawaida huwa kwake kama sheria.

*Jambo usilolijua ni kama usiku wa kiza.* Anafafanua tashbihi hii kwa kusema kwamba, 'Lisilolulikana linalinganishwa na kiza' Yaani, usilokuwa na habari yake kwako halifahamiki wala kueleweka kama giza

Mtaalamu mwingine ambaye amatoa ufasiri wa tashbihi ni Wamitila (2003) anayesema kuwa, "Hii ni tamathali ya usemi ambapo vitu viwili hulinganishwa kwa njia waziwazi. Tashbihi hutambulishwa kwa matumizi ya viungo kama vile kama, mfano wa, mithili ya, tamthili ya, ja, kama vile, sawa n.k"

Msokile (1993) asema, "Tashbihi ni tamathali ya usemi ambayo huhusisha vitu au sehemu tatu ambazo ni pamoja na; kizungumziwa, kifananishi na kiungo". Kwa mfano, "Alivaa shati lililokuwa jeupe kama pamba". Katika mfano huu, kizungumziwa ni shati, kifananishi ni pamba nacho kiungo ni weupe. Maelezo ya wataalu hawa watatu yanadhihirisha mambo fulani ya kimsingi kusuhu tashbihi. Kwanza ni kwamba tashbihi huweza kutambulishwa kupitia viungo au vilinganishi kama vile: mithili ya, tamthili ya, ja, kama, sawa na, mfano wa n.k. Pili ni kuwa tashbihi hulinganisha tabia au sifa za vitu viwili.

Wamitila (2004) pia anasema kuwa tashbihi ni msemo wa kiulinganishi ambao hukieleza kitu au sifa zake kwa kukilinganisha na kingine ili kukuza sifa zake. Maelezo haya ya Wamitila yanaashiria kuwa ulinganisho huu huchangia kukuza sifa za kile kizungumziwa ambazo zimeegemezwa kwenye uelewa wa sifa au tabia za kifananishi. Wamitila anaongeza kuwa,

“Tashbihi inaweza kuangaliwa kitaalamu kwa njia mbili kuu. Njia hizi ni pamoja na kuangalia tashbihi kama usemi wa kiulinganishi ambapo vitu viwili hulinganishwa. Njia ya pili ambayo kwayo tashbihi huangaliwa ni kuichukulia tashbihi kama usemi wa kiulinganishi ambao unafumbata maana fulani”. Katika kazi yetu, mikabala hii miwili itatufaa katika kuafikia malengo ya kuchunguza ulinganifu wa tashbihi katika kitabu cha *Song of Songs* na tafsiri zake katika *Wimbo Ulio Bora*. Katika mfano, ‘amevaa shati lililokuwa jeupe kama pamba,’ kilinganishi pamba kinatokana na uzoefu wa jamii husika kama inavyodhihirika katika lugha yake. Hii ni kwa sababu katika utamaduni mwingine, kilinganishi kinaweza kuwa theluji, na hata maziwa miongoni mwa vilinganishi vingine.

Katika kitabu cha *Song of Songs*, matumizi ya tashbihi yamedhihirika. Kwa mfano, katika sura ya kwanza mstari wa tisa tunaambiwa:

***Song of Songs 1:9***

“I have compared thee, O my love, to a company of horses in Pharaoh's chariots.”

***Wimbo Ulio Bora 1:9***

“Mpenzi wangu, nimekulinganisha na farasi katika magari ya Farao.”

Tashbihi hii inaashiria kuwa farasi waliokuwa kenye gari la Farao walikuwa wa kiume na hii ndiyo inayodhihirisha upekee wa farasi jike huyu. Tashbihi hii, pamoja na kuhitaji uelewa ulioegemezwa kwenye muktadha wa jamii husika, pia imedhihirisha masuala mahususi ya kitamaduni. Mwelekeo huu wa tashbihi kuchota kwenye utamaduni wa lugha chanzi huku zikidokeza masuala mahususi ya kijamii ndio unaotupelekea kuchunguza jinsi ambavyo tashbihi hizi zimehawilishwa kutoka *Song of Songs* hadi *Wimbo Ulio Bora*.

### **3.1.2 Sitiari**

Kwa mujibu wa Kuhenga (1977) sitiari ni neno linaloibuka kutokana na neno sitiri lenye maana ya ficha au funika. Maoni haya ya Kuhenga yanadhihirisha suala muhimu kuhusu sitiari kuwa zina maana fiche. Maana hiyo fiche au hali hiyo ya kuficha maana inatokana na uhalisia kuwa sitiari hurejelea tamathali ya usemi inayohusisha ulinganishaji wa moja kwa moja wa vitu viwili au watu wawili. Ulinganishaji huu humwacha msomaji akiwazia maana inayoibuliwa na ulinganishaji huu. Kwa mfano, katika sura ya pili mstari wa kwanza tunapata mfano:

***Song of Songs 2:1***

“I am the rose of Sharon, and the lily of the valleys.”

### ***Wimbo Ulio Bora 2:1***

“Mimi ni ua la uwandani, ni fahirisi ya mabondeni.”

Katika mfano huu, bibi arusi (mwanamwali, mpenziwe mfalme) anajilinganisha moja kwa moja na ua kushiria urembo wake.

Wa Mutiso (2005) anasema, “Istiari ni mbinu ya kulinganisha vitu kwa kuhusisha vitu viwili tofauti kimaumbile na kitabia. Mlinganisho huu hauhusishi maneno kama vile ja, mithili ya, kama na visawe vyake”. Maelezo ya mtaalamu huyu yanatuashiria kuwa tofauti na tashbihi ambazo hutumia vilinganishi kama vile ja, mithili ya n.k, sitiari hulinganisha bila kutumi vilinganishi hivi. Maoni haya ya wa Mutiso yanawiana na ya wataalamu wengine ambao pia wanaifasiri istiari kwa mwelekeo uu huu. Kwa mfano, Matei (2011) anasema, “Istiari ni mbinu ya kulinganisha kitu na kingine bila kutumia maneno ya kulinganisha kama vile kama, mfano wa na mithili ya”. Anatoa mfano ufuatao wa istiari, “*Mgeni ni kuku mweupe*” ambayo anaeleza kwa kusema kuwa hapa, mgeni anafananishwa moja kwa moja na kuku mweupe kuonyesha kuwa mgeni hutambulika haraka akiwa kundini. Wamitila (2003) kwa upande wake anaeleza istiari kwa kusema kuwa ni tamathali ya usemi ielezeayo sifa za kitu fulani kwa kusema kuwa ni kingine. Hii ni mbinu ya kiulinganishi kama tashbihi lakini ulinganishi huo haujitokezi waziwazi. Hapana matumizi ya viungio kama mithili ya, mfano wa, kama n.k

Mwakio (2016), akirejelea maoni ya wataalamu mbalimbali anaeleza istiari kwa kusema, “Sitiari ni mlinganisho wa moja kwa moja ambao hutokea kwa kuhamisha maana ya sifa, tabia, sura, muundo au umbo fulani kutoka kwa kitu kimoja kwenda kwa kitu kingine... vitu au watu hulinganishwa na vitu au watu wengine kana kwamba vitu au watu hao ni sawa kabisa”. Anahoji vilevile kuwa, “Lengo kuu la kutumia istiari ni kuonyesha uhusiano au ulinganisho wa vitu na watu tofauti tofauti katika kujenga uzito wa maana”. Kuhusu muundo wa istiari, Mwakio anasema, “Sitiari huundwa kwa sehemu tatu ambazo ni pamoja na kilinganishi, kilinganishwa na mwisho msingi wa ulinganishi .... mambo haya matatu ni sharti yawepo katika fungu na yaweze kuhusiana ndiposa ujumbe uliokusudiwa uweze kufasiriwa vyema”. Katika kazi hii, sitiari ilichukuliwa kuwa ni ulinganishaji wa moja kwa moja bila kutumia vilinganishi na ambao unahusisha kulinganisha tabia, sifa, umbo n.k

### 3.1.3 Tashihisi

Wataalamu mbalimbali wametoa fasiri mbalimbali kuhusu istilahi tashihisi. Kwa mfano, Matei (2011) anaeleza kuwa, “Tashihisi ni mbinu ya kukipa kitu sifa za kibinadamu au kitu kisicho hai kupewa sifa za kitu kilicho hai”. Maelezo haya ya Matei yanaashiria kuwa tashihisi kama tamathali ya usemi huhusisha kitu kisichokuwa hai kupewa sifa za viumbe wenye uhai. Japo maelezo haya yanaokosa kutaja viumbe hawa wenye uhai ambao tabia zao zinaakisiwa katika vitu ambavyo havina uhai, yanatupa msingi mzuri wa uelewa wa mbinu hii, kwamba tashihisi huhusu uhaishaji wa vitu visivyokuwa na uhai.

Wamitila (2003) kwa upande wake anasema, “ tashihisi ni tamathali ya usemi ambapo vitu visivyokuwa hai au vitu visivyokuwa na uhai huwasilishwa au husawiriwa kwa namna ilivyo sawa na binadamu ya kuweza kufikiri na kuhisi”. Mtaalamu huyu anaendelea kuhoji kuwa, “... aghalabu tamathali hii hutumiwa pia kurejelea sifa ya kuwapa wanyama sifa za kibinadamu”. Wamitila vilevile anadai kuwa, “Tashihisi haipatikani tu katika lugha ya kifasihi bali pia katika lugha ya kawaida”. Aidha akirejelea majukumu ya tashihisi, Wamitila (khj) nasema, “Tashihisi ina uwezo mkubwa wa kuigusa hisi ya msikilizaji au msomaji”. Maelezo haya ya Wamitila yanatuashiria kuwa tashihisi huhusisha vitu visivyokuwa na uhai pamoja na wanyama kupewa sifa za kibinadamu kwa lengo la kuleta mvuto katika kazi ya fulani.

Harris (2003) naye kwa upande wake anadai kuwa, “Tashihisi ni mbinu inayohusisha vitu, wanyama na hata mawazo kupewa sifa za kibinadamu.... sifa au tabia hizi za kibinadamu zinaweza kuhusu umbo, tabia, hisia, mielekeo, ushawishi n.k”. Harris katika maelezo haya anabainisha sifa za kibinadamu ambazo wanyama, vitu na hata mawazo hupewa katika uhuishi. Pamoja na haya, mtaalamu huyu anasema kuwa tashihisi hufanya mahusiano yetu na vitu au viumbe hivyo kuwa rahisi kwa kuwa yameelezwa kwa tabia au mienendo ya binadamu. Tazama mfano ufuatao:

Meli ililalamikia mawimbi makali yaliyoipiga.

Katika mfano huu, meli huwa haina uwezo wa kulalamika kwa kuwa ni kiumbe kisichokuwa na uhai. Hata hivyo, kwa kuhuisha meli, mwandishi anapata nafasi ya kuyapa matendo yake katika mawimbi tabia au sifa ambazo zinaweza kueleweka kwa urahisi kwa sababu yameelezwa kwa njia ya tabia za kibinadamu. Maelezo ya wataalamu hawa yanaashiria kuwa tashihisi ni mbinu inayohusisha wanyama na vitu visivyo na uhai kupewa sifa au tabia ya binadamu. Huu ndio mwelekeo ambao ulitumiwa katika kazi hii. Japo wataalamu mbalimbali wametoa majukumu tofauti ya tashihisi, katika kazi hii tuliichunguza tashihisi kwa kugemea



kudhihirika kwake katika *Song of Songs* na jinsi ambavyo zimehawilishwa hadi *Wimbo Ulio Bora* ili kutathmini ulinganifu au kutokuwepo kwa ulinganifu wa tamathali hii kati ya matini mbili husika.

### **3.2 Tashbihi, tashihisi na sitiari katika *Song of Songs* na *Wimbo Ulio Bora***

Katika sehemu hii, tulionyesha jinsi tamathali hizi tatu zilivyojitokeza katika *Song of Songs* na jinsi ambavyo zilitafsiriwa hadi *Wimbo Ulio Bora*.

#### **3.2.1 Tashbihi**

Tashbihi katika matini asilia imedhihirisha ruwaza mbalimbali ambapo kila mojawapo ya ruwazo hizo, inaibua masuala tofauti tofauti ya kitafsiri. Ruwaza hizi ni pamoja na pale ambapo tashbihi katika matini chasili zimetumia kilinganishi ‘as’, nyingine ambazo zimetumia kilinganishi ‘like’ na nyingine ambazo zimetumia kilinganishi ‘compared’. Makundi haya matatu yamedhihirisha masuala tofauti ya kitafsiri kama ifuatavyo:

#### **Tashbihi zilizotumia kilinganishi ‘as’**

Katika matini chanzi, *Song of Songs*, tashbihi ambazo zimetumia kilinganishi ‘as’ zimejitokeza mara thelathini na saba (37). Mifano hii imedhihirika katika sura ya kwanza mstari wa tatu (1:3), sura ya kwanza mstari wa tano (1:5), sura ya kwanza mstari wa saba (1:7), sura ya kwanza mstari wa kumi na nne (1:14), sura ya pili mstari wa pili (2:2), sura ya pili mstari wa tatu (2:3), sura ya nne mstari wa kwanza (4:1), sura ya nne mstari wa kumi na moja (4:11), sura ya tano mstari wa kumi na moja (5:11), sura ya tano mstari wa kumi na mbili (5:12), sura ya tano mstari wa kumi na tatu (5:13), sura ya tano mstari wa kumi na nne (5:14), sura ya tano mstari wa kumi na tano (5:15), sura ya sita mstari wa nne (6:4), sura ya sita mstari wa tano (6:5), sura ya sita mstari wa sita (6:6), sura ya sita mstari wa saba (6:7), sura ya sita mstari wa kumi (6:10), sura ya saba mstari wa nne (7:4), sura ya saba mstari wa nane (7:8), sura ya nane mstari wa sita (8:6) pamoja na sura ya nane mstari wa kumi (8:10).

Katika kundi hili la kwanza, kilinganishi hiki kimetafsiriwa katika matini lengwa kama ‘mfano’. Mwelekeo huu umajitokeza mara mbili pekee katika matini chanzi; yaani katika sura ya kwanza mstari wa tano (1:5) pamoja na sura ya tano mstari wa kumi na tano (5:15). Tazama mifano ifuatayo:

#### ***Song of Songs 1:5***

“I am black, but comely, O ye daughters of Jerusalem, as the tents of Kedar, as the curtains of Solomon.”

***Wimbo Ulio Bora 1:5***

“Mimi ni mweusi mweusi, lakini napendeza, enyi binti za Yerusalemu, **mfano** wa hema za Kedari, kama mapazia yake Sulemani.”

***Song of Songs 5:15***

“His legs are as pillars of marble, set upon sockets of fine gold: his countenance is **as** Lebanon, excellent as the cedars.”

***Wimbo Ulio Bora 5:15***

“Miguu yake ni kama nguzo za marimari, zilizowekwa juu ya misingi ya dhahabu; sura yake ni kama Lebanoni, ni bora **mfano** wa mierezi;”

Aidha, katika kundi hili la kwanza, kuna zile tashbihi ambazo kilinganishi ‘as’ kimetafsiriwa kama ‘kama’. Mwalekeo huu wa kilinganishi ‘as’ kutafsiriwa kama ‘kama’ umedhihirika mara nyingi katika matini chanzi. Tazama mifano miwili ifuatayo:

***Song of Songs 1:3***

“Because of the savour of thy good ointments thy name is **as** ointment poured forth, therefore do the virgins love thee.”

***Wimbo Ulio Bora 1:3***

“Manukato yako yanukia vizuri; jina lako ni **kama** marhamu iliyomiminwa; kwa hiyo wanawali hukupenda.”

***Song of Songs 4:1***

“Behold, thou art fair, my love; behold, thou art fair; thou hast doves' eyes within thy locks: thy hair is **as** a flock of goats, that appear from mount Gilead.”

***Wimbo Ulio Bora 4:1***

“Tazama, u mzuri, mpenzi wangu, u mzuri, macho yako ni kama ya hua, nyuma ya barakoa yako. Nywele zako ni **kama** kundi la mbuzi, wakijilaza mbavuni pa mlima Gileadi.”

Pamoja na kilinganishi hiki ‘as’ kutafsiriwa katika matini lengwa kama tulivyoonyesha hapo juu, kundi hili la kwanza linadhihirisha tashbihi ambazo matini chanzi *Song of Songs* inapolinganishwa na matini lengwa *Wimbo Ulio Bora*, kunabainika ulinganifu wa kitamathali. Ulinganifu huu umedhihirika katika mifano ifuatayo:

***Song of Songs 1:5***

“I am black, but comely, O ye daughters of Jerusalem, as the tents of Kedar, as the curtains of Solomon.”

***Wimbo Ulio Bora 1:5***

“Mimi ni mweusi mweusi, lakini napendeza, enyi binti za Yerusalemu, mfano wa hema za Kedari, kama mapazia yake Sulemani.”

Tashbihi inajitokeza pale ambapo mwanamwali analinganisha weusi wake na mahema ya Kedari. Aidha, analinganisha urembo wake na mapazia ya Solomoni. Mifano hii hata hivyo, inadhihirisha hali ambapo kuna kujitokeza kwa ulinganifu wa kitamathali katika tashbihi hii kati ya matini chanzi na matini lengwa. Hii ni kwa mujibu wa nadharia ya tafsiri ya masuala mahususi ya kitamaduni ni kwa sababu dhana husika zipo katika lugha chanzi na vilevile lugha lengwa. Mfano mwingine wa tashbihi ambao imedhihirisha ulinganifu wa kitamathali kati ya matini mbili husika kwa sababu dhana kwenye tashbihi husika katika matini chanzi zinapatikana pia katika matini lengwa ni sura ya sita mstari wa sita (6:6). Tazama mfano ufuatao:

***Song of Songs 6:6***

“Thy teeth are as a flock of sheep which go up from the washing, whereof every one beareth twins, and there is not one barren among them.”

***Wimbo Ulio Bora 6:6***

“Meno yako kama kundi la kondoo, wakipanda kutoka kuoshwa; ambao kila mmoja amezaa mapacha, wala hakuna aliyefiwa kati yao.”

Kando na hali hii ambapo tashbihi zinadhihirisha ulinganifu wa kitamathali kati ya matini mbili husika, kunayo mifano ambapo tashbihi husika katika matini chanzi zinapolinganishwa na jinsi zilivyotafsiriwa katika matini lengwa, panadhihirika ukosefu wa ulinganifu wa kitamathali. Hali hii, kwa mujibu wa utafiti wetu ilitokana na sababu mbalimbali. Kwanza kuna zile tashbihi ambazo kukosekana kwa ulinganifu katika matini mbili husika kulitokana na masuala ya uana. Hii ni kwa sababu uashiriaji wa kijinsia unabainika katika lugha chanzi unakosekana katika lugha lengwa na kwa sababu hiyo kuibua ukosefu wa ulinganifu wa kitamathali katika tashbihi husika. Tazama mifano ifuatayo:

***Song of Songs 5:12***

“**His** eyes are as the eyes of doves by the rivers of waters, washed with milk, and fitly set.”

***Wimbo Ulio Bora 5:12***

“Macho **yake** ni kama hua penye vijito, wakioga kwa maziwa, wakiikalia mito iliyojaa;”

***Song of Songs 5:13***

“**His** cheeks are as a bed of spices, as sweet flowers: his lips like lilies, dropping sweet smelling myrrh.”

***Wimbo Ulio Bora 5:13***

“Mashavu **yake** ni kama matuta ya rihani ambayo hufanyizwa manukato; midomo yake ni kama nyinyoro, inadondosha matone ya manemane;”

***Song of Songs 5:14***

“**His** hands are as gold rings set with the beryl: his belly is as bright ivory overlaid with sapphires.”

***Wimbo Ulio Bora 5:14***

“Mikono **yake** ni kama mianzi ya dhahabu, iliyopambwa kwa zabarajadi; kiwiliwili chake kama kazi ya pembe, iliyonakishiwa kwa yakuti samawi;”

***Song of Songs 5:15***

“**His** legs are as pillars of marble, set upon sockets of fine gold: his countenance is as Lebanon, excellent as the cedars.”

***Wimbo Ulio Bora 5:15***

“Miguu **yake** ni kama nguzo za marimari, zilizowekwa juu ya misingi ya dhahabu; sura yake ni kama Lebanoni, ni bora mfano wa mierezi;”

Katika mifano hii, tashbihi husika zinakosa ulinganifu kwa sababu kiwakilishi ‘his’ ambacho kinaakisi jinsia ya kiume hakijatafsiriwa kwa jinsi ya kuakisi jinsia hiyo katika matini lengwa. Hii ni kwa sababu matini tafsiri katika matini lengwa ni {-ake} kutegememea ngeli ya nomino husika. Kwa mujibu wa nadharia ya Newmark (1988) ya tafsiri ya masuala mahususi za kitamaduni, hali hii inasababishwa na kiwakilishi hiki kinachoakisi jinsia ya kiume kukosekana katika lugha lengwa.

Kando na tashbihi husika kukosa ulinganifu kwa sababu ya kiwakilishi kinachoakisi jinsia kukosekana katika lugha lengwa, kunayo mifano ya tashbihi katika matini lengwa ambazo pia zinadhahirisha ukosefu wa ulinganifu kwa sababu kivumishi kwenye tashbihi husika katika

matini lengwa hakijatafsiriwa kwa jinsi ya kushiria jinsia kama kilivyo kwenye matini chanzi.

Tazama mfano ufuatao:

*Song of Songs 6:4*

“Thou art **beautiful**, O my love, as Tirzah, comely as Jerusalem, terrible as an army with banners.”

*Wimbo Ulio Bora 6:4*

“Mpenzi wangu, u **mzuri** kama Tirza, mwenye kupendeza kama Yerusalemu, wa kutisha kama jeshi lenye bendera.”

Katika tashbihi hii, ‘**thou art beautiful, O my love, as Tirzah**, neno **beautiful** ambalo linaashiria jinsia ya kike limetafsiriwa katika matini lengwa kama ‘mzuri’ hali ambayo uana unaoakisiwa katika matini chanzi haudhihiriki katika matini lengwa. Kufanya hivi kumeibua ukosefu wa ulinganifu katika tamathali hii kati ya matini mbili husika. Hata hivyo, katika tashbihi ya pili na ya tatu zinadhihirisha ulinganifu wa kitamathali. Kwa mujibu wa nadharia tuliyoitumia kwenye kazi hii ya tafsiri ya masuala mahususi ya kitamaduni, kukosekana kwa ulinganifu wa kitamathali katika tashbihi ya kwanza kwenye kifungu hiki kunatokana na sababu za kidini za kuakisi uzuri wa kitabia na wala si wa kimaumbile.

Katika kundi hili la tashbihi vilevile kunazo tashbihi ambazo zimekosa ulinganifu wa kitamathali matini mbili husika zinapolinganishwa kwa sababu baadhi ya masuala katika matini chasili yamedondoshwa katika matini lengwa. Tazama mifano ifuatayo:

*Song of Songs 1:14*

“My beloved is **unto me** as a cluster of camphire in the vineyards of En-gedi”

*Wimbo Ulio Bora 1:14*

“Mpendwa wangu ni kama kishada cha hina, katika mizabibu huko Engedi.”

*Song of 5:12*

“His eyes are as **the eyes of** doves by the rivers of waters, washed with milk, and fitly set.”

*Wimbo Ulio Bora 5:12*

“Macho yake ni kama hua penye vijito, wakioga kwa maziwa, wakiikalia mito iliyojaa.”

*Song of Songs 6:10*

“Who is she that looketh forth as the morning, fair as the moon, clear as the sun, and terrible as **an army** with banners?”

***Wimbo Ulio Bora 6:10***

“Ni nani huyu atazamaye kama alfajiri, mzuri kama mwezi, safi kama jua, wa kutisha kama wenye bendera?”

Katika mifano hii, maneno ‘unto me’, ‘the eyes of’ pamoja na ‘an army’ katika matini chanzi yamedondoshwa katika matini lengwa. Udondoshaji huu kwa mujibu wa nadharia ya tafsiri ya masuala mahususi ya kitamaduni unasababisha ukosefu wa ulinganifu wa kitamathali katika tashbihi husika. Kwingineko, ukosefu wa ulinganifu umesababishwa na mtafsiri kutumia maelezo katika matini lengwa. Tazama mfano ufuatao:

***Song of Songs 1:14***

“My beloved is unto me as a cluster of camphire in the vineyards of En-gedi”

***Wimbo Ulio Bora 1:14***

“Mpendwa wangu ni kama kishada cha hina, katika mizabibu **huko** Engedi.”

Katika mfano huu, neno ‘huko’ katika matini lengwa linajitokeza kama maelezo ya ziada ambayo hayapo katika matini chanzi. Mkakati huu wa kutumia maelezo ya ziada katika matini lengwa kwa mujibu wa nadharia ya masuala mahususi ya kitamaduni huchangia ukosefu wa ulinganifu wa kitamathali katika tashbihi husika.

Katika mifano mingine, kutojitokeza kwa ulinganifu wa kitamathali kumedhihirika katika matini lengwa kwa sababu ya kile tulichokirejelea kama udhaifu wa kitafsiri. Tazama mfano ufuatao:

***Song of Songs 2:2***

“As the lily among thorns, so is my love among the daughters.”

***Wimbo Ulio Bora 2:2***

“Kama fahirisi kati ya miiba, kadhalika mpenzi wangu kati ya binti.”

Katika tashbihi hii, kunadhihirika pia kutojitokeza kwa ulinganifu wa kitamathali kwa sababu neno la matini chasili ‘among’ limetafsiriwa katika matini lengwa kama ‘kati ya’ badala ya ‘miongoni mwa’. Pamoja na kwamba nadharia tuliyoitumia inasisitiza kuwa kutojitokeza kwa tamathali hizi, kama dhana mojawapo ya kitafsiri kunatokana na kutokuwepo kwa masuala husika katika lugha mojawapo kati ya lugha husika katika tafsiri, mfano huu unadhihirika udhaifu wa kitafsiri kwa sababu baadhi ya istilahi zinazoiunda tashbihi husika zipo katika lugha lengwa, wala muktadha husika haushawishi tafsiri iliyofanywa.

Pamoja na mifano hii, kuna hali ambapo ukosefu wa ulinganifu wa kitamathali umesababishwa na mtafsiri kutumia tafsiri ambayo inaweza kuchochea fasiri nyingi tofauti na ilivyo katika matini chasili. Tazama mfano ufuatao:

***Song of Songs 1:3***

“Because of the savour of thy good ointments thy name is as ointment poured forth, therefore do the virgins love thee.”

***Wimbo Ulio Bora 1:3***

“Manukato yako yanukia vizuri; jina lako ni kama marhamu iliyomiminwa; kwa hiyo wanawali hukupenda.”

Tashbihi inajitokeza pale ambapo jina linafananishwa na manukato yaliyomiminwa. Mfano huu hata hivyo, unadhihirisha hali ambapo kuna kutojitokeza kwa ulinganifu wa kitamathali katika tashbihi hii kati ya matini chanzi na matini lengwa kwa kuwa fungu ‘poured forth’ ambalo limetafsiriwa kama miminwa linaweza kueleweka kuwa na maana zaidi ya kumimina kama vile ‘kumwaga nje ya’.

Kundi hili la tashbihi pia lilidhihirisha tashbihi ambazo kutojitokeza kwa ulinganifu wa kitamathali kunatokana na mtafsiri kutozingatia masuala ya kipragmatiki. Tazama mfano ufuatao:

***Song of Songs 7:8***

“I said, I will go up to the palm tree, I will take hold of the boughs thereof: now also thy breasts shall be as clusters of the vine, and the smell of thy nose like apples;”

***Wimbo Ulio Bora 7:8***

“**Matiti yako mawili** ni kama wanapaa wawili, nyuma ya barakoa yako. Ambao ni mapacha ya paa; wakilisha penye nyinyoro.

Ukosefu wa ulinganifu wa kitamathali katika mfano huu unatokana na neno ‘breasts’ katika matini chanzi kutafsiriwa kama ‘matiti’ katika matini lengwa. Katika kufanya hivi, mtafsiri ameegemea masuala ya kisemantiki na kupuuzwa masuala ya kipragmatiki kwani neno ambalo lingefaa zaidi ni ‘maziwa’ au ‘kifua’ kwa sababu limetasfidiwa.

**Tashbihi zilizotumia kilinganishi ‘like’**

Tashbihi zilizotumia kilinganishi ‘like’ zimejitokeza mara ishirini (20). Kwa mfano katika sura ya pili mstari wa tisa (2:9), sura ya pili mstari wa kumi na saba (2:17), sura ya tatu mstari wa

sita (3:6), sura ya nne mstari wa pili (4:2), sura ya nne mstari wa tatu (4:3), sura ya nne mstari wa nne (4:4), sura ya nne mstari wa tano (4:5), sura ya nne mstari wa kumi na moja (4:11), sura ya tano mstari wa kumi na tatu (5:13), sura wa sita mstari wa kumi na mbili (6:12), sura ya saba msatri wa kwanza (7:1), sura ya saba mstari wa pili (7:2), sura ya saba mstari wa tatu (7:3), sura ya saba mstari wa nne (7:4), sura ya saba mstari wa tano (7:5), sura ya saba mstari wa saba (7:7), sura ya saba mstari wa nane (7:8), sura ya saba mstari wa tisa (7:9), sura ya nane mstari wa kumi (8:10) pamoja na sura ya nane mstari wa kumi na nne (8:14). Katika mifano hii, ruwaza zifuatazo zimejitokeza:

Kwanza, kuna zile tashbihi zilizopo katika matini chasili *Song of Songs*, ambazo zinakosa ulinganifu zikilinganishwa katika matini mbili husika kwa sababu ya masuala ya kijinsia. Hii ni kwa kuwa wanyama waliotajwa kijinsia katika matini chanzi, hawarejelewi kwa njia inayoakisi jinsia katika matini lengwa. Tazama mifano ifuatayo:

***Song of Songs 2:9***

“My beloved is like a roe or a young **hart**: behold, he standeth behind our wall, he looketh forth at the windows, shewing himself through the lattice.”

***Wimbo Ulio Bora 2:9***

“Mpendwa wangu ni kama paa, au **ayala**. Tazama, asimama nyuma ya ukuta wetu, achungulia dirishani, atazama kimiani.”

***Song of Songs 2:17***

“Until the day break, and the shadows flee away, turn, my beloved, and be thou like a roe or a young **hart** upon the mountains of Bether.”

***Wimbo Ulio Bora 2:17***

“Hata jua lipunge, na vivuli vikimbie, unigeukie, mpendwa wangu, nawe uwe kama paa, au **ayala**, juu ya milima ya Betheri.”

***Song of Songs 8:14***

“Make haste, my beloved, and be thou like to a roe or to a young **hart** upon the mountains of spices.”

***Wimbo Ulio Bora 8:14***

“Ukimbie, mpendwa wangu, nawe uwe kama paa, au **ayala**, juu ya milima ya manukato.”

Katika mifano hii ya tashbihi, panadhihirisha ukosefu wa ulinganifu wa kitamathali kwa sababu jinsia ya kiume inayoakisiwa na neno ‘**hart**’ haidhihiriki katika matini lengwa. Jambo hili linafanya tashbihi hii katika matini lengwa kutokuwa na msukumo sawa katika kufasiriwa



kwake, matini mbili husika zinapolinganishwa. Hali hii kwa mujibu wa nadharia ya tafsiri ya masuala mahususi ya kitamaduni inatokana na lugha lengwa kukosa uashiraji wa kijinsia katika kuwataja wanyama husika.

Aidha kuna hali ambapo ukosefu wa ulinganifu wa kitamathali katika tashbihi husika umetokana na masuala ya kijinsia ambapo kiwakilishi kinachodokeza jinsia katika matini chanzi kimetafsiriwa katika matini lengwa kwa njia ambayo uana unaoakisiwa katika matini chanzi haujitokezi. Tazama mfano ufuatao:

***Song of Songs 4:5***

“His cheeks are as a bed of spices, as sweet flowers: his lips like lilies, dropping sweet smelling myrrh.”

***Wimbo Ulio Bora 4:5***

“Mashavu yake ni kama matuta ya rihani ambayo hufanyizwa manukato; midomo yake ni kama nyinyoro, inadondosha matone ya manemane;”

Katika kundi hili la tashbihi vilevile kunazo tashbihi ambazo zimekosa ulinganifu wa kitamathali matini mbili husika zinapolinganishwa kwa sababu baadhi ya masuala katika matini chasili yamedondoshwa katika matini lengwa. Tazama mifano ifuatayo:

***Song of Songs 4:5***

“Thy two breasts are like two **young** roes that are twins, which feed among the lilies.”

***Wimbo Ulio Bora 4:5***

“Matiti yako mawili ni kama wanapaa wawili, nyuma ya barakoa yako. Ambao ni mapacha ya paa; wakilisha penye nyinyoro.”

***Song of Songs 4:2***

“Thy teeth are like a flock of **sheep** that are even shorn, which came up from the washing; whereof every one bear twins, and none is barren among them.”

***Wimbo Ulio Bora 4:2***

“Meno yako ni kama kundi waliokatwa manyoya, wakipanda kutoka kuoshwa, ambao kila mmoja amezaa mapacha, wala hakuna aliyefiwa kati yao.”

Katika mifano hii, kutojitokeza kwa ulinganifu wa kitamathali katika tashbihi hizi kumesababishwa na udondoshaji wa dhana ‘young’ na ‘sheep’ katika mfano wa kwanza na wa pili mtawalia. Hii ni kwa sababu masuala haya ambayo ni muhimu katika kukeza maana katika matini chasili hayapo katika matini lengwa. Udondoshi huu ambao unasababisha kutokuwepo kwa ulinganifu wa kitamathali kati ya matini mbili husika unajitokeza kama udhaifu wa

kitafsiri kwa mujibu wa nadhari ya tafsiri ya masuala mahususi ya kitamaduni. Udondoshaji huu pia umejitokeza katika sura ya tano mstari wa kumi na tatu (5:13) pamoja na sura ya saba mstari wa tisa (7:9). Aidha, ukosefu wa ulinganifu wa kitamathali umesababishwa na mtafsiri kutafsiri baadhi ya masuala katika matini chanzi kwa njia ya kifasiri. Tazama mfano ufuatao:

***Song of Songs 6:12***

“Or ever I was aware, **my soul made me like the chariots of Amminadib.**”

***Wimbo Ulio Bora 6:12***

“Kabla sijajua, **roho yangu ilinileta katikati ya magari ya wakuu wangu.**”

Katika mfano huu, fungu ‘my soul made me like the chariots of Amminadib’ ambalo limetafsiriwa kifasiri kama ‘roho yangu ilinileta katikati ya magari ya wakuu wangu’. Kwa mujibu wa nadharia ya tafsiri ya masuala mahususi ya kitamaduni mkakati huu wa kutafsiri kifasiri unachangia kutokuwepo kwa ulinganifu kati ya tashbihi husika. Mkakati huu umedhihirika katika sura ya saba mstari wa kwanza (7:1) pamoja na sura ya saba mstari wa pili (7:2). Aidha, ukosefu wa ulinganifu wa kitamathali umesababishwa na mtafsiri kutafsiri baadhi ya masuala katika matini chanzi kwa njia ya kupamua maana ya baadhi ya masuala hayo. Tazama mfano ufuatao:

***Song of Songs 6:12***

“Or ever I was aware, my soul made me like the **chariots** of Amminadib.”

***Wimbo Ulio Bora 6:12***

“Kabla sijajua, roho yangu ilinileta katikati ya **magari** ya wakuu wangu.”

Katika mfano huu, neno ‘chariots’ katika matini chanzi linadokeza aina mahususi ya vyombo vya usafiri. Hata hivyo, mtafsiri amepanua maana ya neno hili katika matini lengwa kwa kutumia neno ‘gari’ ambalo linajumuisha aina mbalimbali ya vyombo hivi vya usafiri. Mkakati huu wa kupanua maana ya dhana katika matini lengwa kwa mujibu wa nadharia ya tafsiri ya masuala mahususi ya kitamaduni ndio unaosababisha ukosefu wa ulinganifu wa maana katika tashbihi husika.

Pamoja na ruwaza hizi tulizozijadili hapa juu kuhusu kundi hili la tashbihi, kuna zile tashbihi ambazo zimedhihirisha ukosefu wa ulinganifu wa kitamathali kati ya matini mbili husika kwa sababu ya tafsiri kufanywa kimaelezo. Tazama mifano ifuatayo:

***Song of Songs 3:6***

“Who is this that cometh out of the wilderness like pillars of smoke, perfumed with myrrh and frankincense, **with all powders of the merchant?**”

***Wimbo Ulio Bora 3:6***

“Ni nani huyu apandaye kutoka nyikani, mfano wake ni nguzo za moshi; afukizwa manemane na ubani, **na mavumbi ya manukato yote ya mchuuzi?**”

***Song of Songs 4:3***

“Thy lips are like a thread of scarlet, and thy speech is comely: thy temples are like a **piece of a pomegranate** within thy locks.”

***Wimbo Ulio Bora 4:3***

“Midomo yako ni kama uzi mwekundu, na kinywa chako ni kizuri; mashavu yako ni **kama nusu kipande cha komamanga**, nyuma ya barakoa yako.”

Katika mifano hii, fungu ‘with all powders of the merchant’ ambalo limetafsiriwa kwa njia ya kuongeza maelezo ya ziada kama ‘na mavumbi ya manukato yote ya mchuuzi’ katika mfano wa kwanza pamoja na fungu ‘piece of a pomegranate’ ambalo limetafsiriwa kama ‘kama nusu ya kipande cha komamanga’ yanadhihirisha kutojitokeza kwa ulinganifu wa kitamathali kwa sababu ya tafsiri ya kutoa maelezo ambayo hayapo katika matini chanzi. Aidha, katika mfano wa kwanza (3:6), tashbihi hii vilevile inadhihirisha ukoefu wa ulinganifu kati ya matini mbili husika. Hii ni kwa sababu maneno ‘**cometh out of the wilderness**’ ambayo yametafsiriwa kama ‘apandaye kutoka nyikani’ kinafanya maana ya tashbihi hii kutolingana na maana katika matini chasili kwa kuwa dhana zinazoibuliwa katika matini chasili na zile za matini lengwa ni tofauti. Kwa mujibu wa nadharia tuliyoitumia ya tafsiri ya masuala mahususi ya kitamaduni, tafsiri hii inadhihirisha udhaifu katika tafsiri kwa sababu lugha lengwa ina misamiati ifaavyo ya kurejelea dhana husika wala muktadha husika hauhalisi tafsiri iliyotumika.

**Tashbihi iliyotumia kilinganishi ‘compared’**

Kundi hili la tashbihi limedhihirika mara moja tu katika sura ya kwanza, mstari wa tisa kama ilivyo kwenye mfano ufuatao:

***Song of Songs 1:9***

“I have compared thee, O my love, to a company of horses in Pharaoh's chariots.”

### ***Wimbo Ulio Bora 1:9***

“Mpenzi wangu, nimekulinganisha na farasi katika magari ya Farao.”

Tashbihi hii inadhihirisha kutojitokeza kwa ulinganifu wa kitamathali kwa njia mbalimbali. Kwanza, kutafsiri ‘a company of horses’ kama ‘farasi’ kunaibua dhana katika matini lengwa ambayo ni tofauti na ile iliyoko katika matini chanzi. Aidha fungu ‘**Pharaoh’s chariots**’ ambalo limetafsiriwa kama ‘magari ya Farao’ pia linasababisha ukosefu wa ulinganifu wa kitamathali kwani ‘magari ya Farao’ ni istilahi ya kijumla ilhali neno ‘**chariot**’ linadokeza gari mahususi. Maelezo haya muhimu yanakosekana katika matini lengwa, hali inayosababisha ukosefu wa ulinganifu wa kitamathali katika tashbihi husika katika matini mbili tulizorejelea. Hali hii kwa mujibu wa nadharia tafsiri ya masuala mahususi ya kitamaduni katika kazi hii ni kwa sababu dhana kama vile ‘chariots’ inakosekana katika lugha lengwa.

### **3.2.2 Sitiari**

Katika kukichunguza kitabu cha *Song of Songs* kwa kukilinganisha na kile cha *Wimbo Ulio Bora* ambacho ni tafsiri yake katika lugha ya Kiswahili, masuala mbalimbali ya kitafsiri yanadhihirika. Hata hivyo, katika sehemu hii, tulimakinikia zaidi ulinganifu wa kitamathali katika kuangazia jinsi unavyoakisika katika sitiari husika au ukosefu wake kati ya matini hizi mbili tulizorejelea. Tafsiri ya sitiari kutoka matini chanzi hadi matini lengwa imedhihirisha masuala mbalimbali ya kitafsiri.

Kwa kulinganisha matini chanzi na matini lengwa, ruwaza ya kwanza ambayo imedhihirika katika tafsiri ya sitiari ni pale ambapo sitiari katika matini chanzi inabadilika kuwa tashbihi katika matini lengwa. Tazama mfano ufuatao:

### ***Song of Songs 1:13***

“**A bundle of myrrh is my wellbeloved unto me; he shall lie all night betwixt my breasts.**”

### ***Wimbo Ulio Bora 1:13***

“**Mpendwa wangu ni kama mfuko wa manemane** ukilazwa usiku maziwani mwangu.”

Katika sitiari hii, ulinganifu wa kitamathali unakosekana tamathali hii inapolinganishwa katika matini mbili husika. Hii ni kwa sababu tamathali hii ambayo ni sitiari katika matini chanzi inageuka kuwa tashbihi katika matini lengwa. Kufanya hivi kunadhoofisha nguvu za ulinganishaji ambao unadhihirishwa na sitiari. Hivi ni kumaanisha kuwa mpendwa wa mrejelewa si mfuko wa manemane hasa bali ni kama mfuko wa manemane. Kwa mujibu wa

nadharia ya tafsiri ya masuala mahususi ya kitamaduni, huu unajitokeza kama udhaifu katika tafsiri kwa kuwa muktadha husika hauhalisi tafsiri ya sampuli hii.

Pamoja na ruwaza hii ya sitiari katika matini chanzi kubadilishwa kuwa tashbihi katika matini lengwa, kuna zile sitiari ambazo zimekosa ulinganifu wa kitamathali kwa sababu ya kutafsiriwa kifasiri. Tazama mfano ufuatao:

***Song of Songs 2:1***

“I am the rose of Sharon, and the lily of the valleys.”

***Wimbo Ulio Bora 2:1***

“Mimi ni ua la uwandani, ni fahirisi ya mabondeni.”

Katika mfano huu, fungu ‘rose of Sharon’ ambalo limetafsiriwa kama ‘ua la uwandani’ limetafsiriwa kwa kutoa maana ya fungu husika katika matini asilia. Jambo hili linasababisha ukosefu wa ulinganifu wa kitamathali katika tamathali husika kati ya matini mbili husika. Aidha kuna sitiari nyingine ambazo ukosefu wa ulinganifu wa kitamathali umesababishwa na hali ya tafsiri kufanywa kwa kutoa maelezo ya ziada ambayo hayapo kwenye matini chanzi. Tazama mfano ufuatao:

***Song of Songs 8:9***

“If she be a wall, we will build upon her a palace of silver: and if she be a door, we will inclose her with boards of cedar.”

***Wimbo Ulio Bora 8:9***

“Kama akiwa tu ukuta, tumjengee buruji za fedha; na kama akiwa ni mlango, tumhifadhi kwa mbao za mierezi.”

Katika sitiari ‘if she be a wall’ ambayo imetafsiriwa kama ‘kama akiwa tu ukuta’, neno ‘tu’ katika matini lengwa ni maelezo ya ziada ambayo hayapo kwenye matini chanzi. Maelezo haya kwa mujibuwa nadharia ya tafsiri ya masuala mahususi ya kitamaduni yanasababisha ukosefu wa uliganifu wa kitamathali kati ya matini husika. Katika mifano mingine, ukosefu wa ulinganifu wa kitamathali unakosekana kwa kuwa metafsiri hajazinganitia wakati katika matini chanzi. Tazama mfano ufuatao:

***Song of Songs 8:10***

“I am a wall, and my breasts like towers: then was I in his eyes as one that found favour.”

***Wimbo Ulio Bora 8:10***

“Mimi nilikuwa ukuta, na matiti yangu kama minara; ndipo nikawa machoni pake kama mtu aliyeipata amani.”

Sitiari hii ‘**I am a wall**’ katika matini chanzi ambayo imetafsiriwa kama ‘**mimi nilikuwa ukuta**’ katika matini lengwa inadhihirisha hali ya ukosefu wa ulinganifu wa kitamathali kati ya matini mbili husika. Hii ni kwa sababu mtafsiri ametumia wakati uliopita ‘nilikuwa’ badala ya wakati uliopo unaoakisiwa na neno ‘am’ katika matini chanzi. Hali hii inaleta tofauti katika sitiari hii kwa kulinganisha matini husika. Hata hivyo kwa kuwa muktadha husika unahashawishi tafsiri kwa kutumia wakati uliopita, inadhihirika kuwa mtafsiri alitumia tafsiri kuafikia sitiari hii katika matini lengwa.

Aidha, kunayo mifano ambapo ukosefu wa ulinganifu wa kitamathali umetokana na mtafsiri kutafsiri kwa njia ya kutoa maelezo ya ziada ambayo hayapo katika matini chanzi. Tazama mfano ufuatao:

***Song of Songs 4:12***

“A garden inclosed is my sister, my spouse; a spring shut up, a fountain sealed;”

***Wimbo Ulio Bora 4:12***

“Bustani iliyofungwa ni dada yangu, bibi arusi, kijito kilichofungwa, chemchemi iliyotiwa mhuri.”

Katika mfano huu, tofauti inaibuka kati ya sitiari husika katika matini chanzi na matini lengwa. Kwa mfano, sitiari ‘**A garden inclosed is my sister, my spouse**’ imetafsiriwa kama ‘**Bustani iliyofungwa ni dada yangu, bibi arusi,**’. Katika tafsiri hii, neno ‘my’ katika kirai ‘my spouse’ limedondoshwa katika matini lengwa, jambo linalosababisha kutokuwepo kwa ulinganifu kati ya matini mbili husika. Hatua hii ya kudondosha umilikaji katika matini chanzi kwa mujibu wa nadharia ya tafsiri ya masuala mahususi ya kitamaduni huweza kusemekana kuwa ilikusudiwa kuondoa uziada katika sitiari husika kwa kuwa umilikaji umedokezwa katika sehemu ya kwanza ya tashbihi husika.

Sitiari nyingine ilidhihirisha ruwaza ambayo ilionyesha ukosefu wa ulinganifu wa kitamathali kwa sababu ya tofauti katika mpangilio wa kisintaksia katika baadhi ya virai nomino. Tazama mfano ufuatao:

***Song of Songs 4:13***

“Thy plants are an orchard of pomegranates, with pleasant fruits; camphire, with spikenard,”

***Wimbo Ulio Bora 4:13***

“Machipuko yako ni bustani ya komamanga, yenye matunda mazuri, hina na nardo,”

Sitiari hii inadhihirisha tofauti katika kiwango cha kisintaksia ambapo kivumishi na nomino katika matini chanzi zinapishana nafasi katika matini lengwa kama ilivyo katika mfano (**thy plants- machipuko yako**) na vilevile (**pleasing fruits – matunda mazuri**). Kwa mujibu wa nadharia ya tafsiri ya masuala mahususi ya kitamaduni, tofauti hii inatokana na tofauti kwenye muundo wa kisintaksia kati ya lugha mbili husika.

### 3.2.3 Tashihisi

Tashihisi katika matini chanzi zimejitokeza mara kumi na mbili. Tashihisi hizi zimejitokeza katika sura ya kwanza mstari wa kumi na mbili (1:12), sura ya pili mstari wa sita (2:6), sura ya pili mstari wa saba (2:7), sura ya pili mstari wa kumi na tatu (2:13), sura ya pili mstari wa kumi na nne (2:14), sura ya tatu mstari wa tano (3:5), sura ya nne mstari wa sita (4:6), sura ya nne mstari wa kumi na sita (4:16), sura ya tano mstari wa pili (5:2), sura ya saba mstari wa kumi na tatu (7:13), sura ya nane mstari wa nne (8:4) pamoja na sura ya nane mstari wa sita (8:6). Mifano hii inadhihirisha masuala mbalimbali ya kitafsiri. Kwa mfano, kuna tashihisi ambazo zimedhihirisha ulinganifu wa kitamathali kwa sababu dhana husika katika tashihisi husika zinapatikana katika lugha zote mbili husika. Tazama mfano ufuatao:

#### *Song of Songs 2:17*

“Until the day breaks and the shadows flee, turn, my beloved, and be like a gazelle or like a young stag on the rugged hills.”

#### *Wimbo Ulio Bora 2:17*

“Mpaka jua linapochomoza, na vivuli vikimbie, rudi, mpenzi wangu, na uwe kama paa, au kama ayala kijana juu ya vilima vya Betheri.”

Tashihisi hii katika matini chanzi ‘**shadows flee**’ imetafsiriwa katika matini lengwa kama ‘**vivuli vikimbie**’, hali inayodhihirisha ulinganifu wa kitamathali. Tashihisi hii ‘**shadows flee**’ imejitokeza pia katika sura ya nne mstari wa sita (4:6) ambapo pia imeibua masuala haya haya ya kitafsiri kuhusu ulinganifu wa kitamathali. Tazama mfano ufuatao;

#### *Song of Songs 4:6*

“Until the day breaks and the shadows flee, I will go to the mountain of myrrh and to the hill of incense.”

#### *Wimbo Ulio Bora 4:6*

“Hata papambazuke na vivuli vikimbie, nitakwenda kwenye mlima wa manemane na kwenye kilima cha uvumba.”

Ulinganifu huu wa kitamathali kwa mujibu wa nadharia tuliyoitumia ya tafsiri ya masuala mahususi ya kitamaduni, unatokana na lugha zote mbili kusheheni dhana zinazohusika katika tashihisi husika. Ulinganifu wa kitamathali pia umejitokeza katika tashihisi inayojitokeza katika sura ya nne mstari wa kumi na sita (4:16). Tazama mfano ufuatao:

***Song of Songs 4:16***

“Awake, north wind, and come, south wind! Blow on my garden, that its fragrance may spread everywhere. Let my beloved come into his garden and taste its choice fruits.”

***Wimbo Ulio Bora 4:16***

“Amka, upepo wa kaskazi, na uje, upepo wa kusi! Vuma juu ya bustani yangu, ili harufu yake nzuri iweze kuenea mpaka ng’ambo. Mpendwa wangu na aje bustanini mwake na kuonja matunda mazuri sana.”

Tafsiri ya tashihisi ‘**awake, north wind, and come, south wind**’ katika lugha chanzi hadi ‘**amka, upepo wa kaskazi, na uje, upepo wa kusi**’ pia inadhihirisha ulinganifu wa kitamathali. Hii ni kwa sababu dhana husika zinapatikana katika lugha zote mbili husika.

Pamoja na ulinganifu wa kitamathali ambao umejitokeza katika mifano ya hapo juu, kunayo mifano ya tashihisi ambazo zinadhihirisha ukosefu wa ulinganifu wa kitamathali kwa sababu mbalimbali. Tazama mifano ifuatayo:

***Song of Songs 1:12***

“While the king sitteth at his table, my spikenard sendeth forth the smell thereof.”

***Wimbo Ulio Bora 1:12***

“Muda mfalme alipoketi juu ya kochi, nardo yangu ilitoa harufu yake.”

Kwa kulinganisha tashihisi katika matini lengwa, ‘**my spikenard sendeth forth the smell thereof**’, ambayo imetafsiriwa katika lugha lengwa kama ‘**nardo yangu ilitoa harufu yake**’ inadhihirisha hali ya ukosefu wa ulinganifu kati ya matini mbili husika. Hii ni kwa sababu ya nomino na kivumishi katika matini chanzi zimepushana nafasi matini chanzi inapolinganishwa na matini lengwa. Kwa mujibu wa nadharia ya tafsiri ya masuala mahususi ya kitamaduni, hali hii inatokana na tofauti katika miundo ya kisintaksia ya lugha mbili zinazohusika.

Aidha, kunazo tashihisi ambazo zinapolinanishwa katika matini mbili husika, zinadhihirisha ukosefu wa ulinganifu wa kitamathali kwa sababu ya tofauti kati ya lugha mbili husika katika kuakisi wingi. Tazama mfano ufuatao:



***Song of Songs 2:7***

“I charge you, O ye daughters of Jerusalem, by the roes, and by the hinds of the field, that ye stir not up, nor awake my love, till he please.”

***Wimbo Ulio Bora 2:7***

“Nawasihi, enyi binti za Yerusalemu, kwa paa na kwa ayala wa porini, msiyachochee mapenzi, wala kuyaamsha, hata yatakapoona vema yenyewe.”

Katika tashihisi hii, “**ye stir not up, nor awake my love, till he please**”, ambayo imetafsiriwa katika matini lengwa kama “**msiyachochee mapenzi, wala kuyaamsha, hata yatakapoona vema yenyewe.**” kumedhihirika ukosefu wa ulinganifu wa kitamathali kwani hali ya wingi katika matini chanzi inajitokeza katika muktadha wa fungu zima ilhali katika matini lengwa hali ya wingi imejitokeza kupitia kiambishi cha wingi {m} katika neno ‘msichochee’. Kwa mujibu wa nadharia tuliyoitumia katika kazi hii, tofauti kati ya lugha mbili husika huchangia tofauti hii. Vilevile, neno ‘yenyewe’ pia ni maelezo ya ziada ambayo hayapo katika matini chanzi. Tashihisi hii vilevile imejitokea katika sura ya tatu mstari wa tano (3:5) ambapo imetafsiriwa kwa njia sawa na kuibua masuala sawa kuhusu ulinganifu wa kitamathali. Tazama mifano ifuatayo:

***Song of Songs 3:5***

“I charge you, O ye daughters of Jerusalem, by the roes, and by the hinds of the field, that ye stir not up, nor awake my love, till he please.”

***Wimbo Ulio Bora 3:5***

“Nawasihi, enyi binti za Yerusalemu, kwa paa na kwa ayala wa porini, msiyachochee mapenzi, wala kuyaamsha, hata yatakapoona vema yenyewe.”

***Song of Songs 8:4***

“I charge you, O daughters of Jerusalem, that ye stir not up, nor awake my love, until he please.”

***Wimbo Ulio Bora 8:4***

“Nawasihi, enyi binti za Yerusalemu, msiyachochee mapenzi, au kuyaamsha, hadi yatakapokuwa tayari.”

Katika mifano hii, ukosefu wa ulinganifu wa kitamathali pia unatokana na masuala ya kijinsia. Hii ni kwa sababu tashihisi hii imejengwa kwenye msingi wa kurejelea mapenzi kama ‘he’ ambacho ni kiwakilishi kinachoakisi jinsia ya kiume. Hata hivyo tafsiri yake katika matini lengwa haiakisi jinsia husika kama ilivyo katika matini chanzi. Kwa mujibu wa nadharia ya

tafsiri ya masuala masusi ya kitamaduni, hali hii inatokana na tofauti kati ya lugha husika katika kuakisi jinsia kupitia kwa viwakilishi.

Tashihisi nyingine zimedhihirisha ukosefu wa ulinganifu wa kitamathali kwa sababu ya tafsiri kufanywa kwa kudondosha baadhi ya masuala katika matini chanzi uhawilishaji unapofanywa hadi matini lengwa. Tazama mfano ufuatao:

***Song of Songs 2:13***

“The fig tree putteth forth her green figs, and the vines with the tender grape give a good smell. Arise, my love, my fair one, and come away.”

***Wimbo Ulio Bora 2:13***

“Mtini wapevusha tini zake, na mizabibu inachanua, inatoa harufu yake nzuri; ondoka, mpenzi wangu, mzuri wangu, uje zako.”

Kutafsiriwa kwa tashihisi katika matini chanzi ‘**the vines with the tender grape give a good smell**’ kama ‘**na mizabibu inachanua, inatoa harufu yake nzuri**’ katika matini lengwa kunadhihirisha hali ya kutokuwepo kwa ulinganifu kati ya tashihisi hii katika matini chanzi na matini lengwa. Hii ni kwa sababu kibainishi ‘**the**’ katika matini chanzi kimedondoshwa katika matini lengwa. Hali hii kwa mujibu wa nadharia ya tafsiri ya masuala mahususi ya kitamaduni inatokana na lugha lengwa kukosa kipashio husika. Kiwakilishi kingine ambacho kinapolinanishwa katika matini chanzi na matini lengwa katika tashihisi husika kinasababisha ukosefu wa ulinganifu wa kitamathali kati ya matini mbili husika ni kiwakilishi ‘I’. Tazama mfano ufuatao:

***Song of Songs 5:2***

“I slept but my heart was awake. Listen! My beloved is knocking: “Open to me, my sister, my darling, my dove, my flawless one. My head is drenched with dew, my hair with the dampness of the night.”

***Wimbo Ulio Bora 5:2***

“Nililala lakini moyo wangu ulikuwa macho. Sikiliza! Mpenzi wangu anabisha: “Nifungulie, dada yangu, mpenzi wangu, hua wangu, asiye na hitilafu. Kichwa changu kimeloa umande, na nywele zangu manyunyuni ya usiku.”

Tashihisi ‘**I slept but my heart was awake**’ katika matini chanzi imejitokeza katika matini lengwa kwa jinsi ambayo inadhihirisa ukosefu wa ulinganifu wa kitamathali. Hii ni kwa sababu kiwakilishi ambacho ni neno zima ‘I’ katika matini chanzi kimetafsiriwa kwa njia ya kiambishi

{ni-} kwenye neno ‘**nililala**’ katika matini lengwa. Tashihisi nyingine zimeonyesha ukosefu wa ulinganifu wa kitamathali kwa sababu ya tofauti ya kisintaksia kati ya lugha mbili zilizohusika katika matini tulizozirejelea. Tazama mfano ufuftao:

*Song of Songs 7:5*

“Your head crowns you like Mount Carmel. Your hair is like royal tapestry; the king is held captive by its tresses.”

*Wimbo Ulio Bora 7:5*

“Kichwa chako kinakuvika taji kama mlima Karmeli. Nywele zako ni kama zulia nene la kutundika ukutani, mfalme ametekwa na mashungi yake.”

Tofauti ya kitamathali inayojitokeza katika tashihisi husika kama inavyojitokeza katika matini chanzi ‘**your head crowns you**’ na matini lengwa, ‘**kichwa chako kinakuvika taji**’ inatokana na muundo tofauti ya kisintaksia kati ya lugha chanzi na lugha lengwa. Kwa mfano, kirai ‘**your head**’ (kivumishi kisha nomino) kinabadilika na kuwa ‘kichwa chako’ ambacho ni nomno kisha kivumishi.

Kwa upande mwingine, kunazo tashihisi ambazo zimeonyesha ukosefu wa ulinganifu wa kitamathali kati ya matini mbili husika kwa sababu ya matini lengwa kudhihirisha tafsiri ya kimaelezo. Tazama mfano ufuatao:

*Song of Songs 7:13*

“The mandrakes send out their fragrance, and at our door is every delicacy, both new and old, that I have stored up for you, my beloved.”

*Wimbo Ulio Bora 7:13*

“Mitunguja hutoa harufu zake nzuri, kwenye milango yetu kuna matunda mazuri, mapya na ya zamani, ambayo nimekuhifadhia wewe, mpenzi wangu.”

Kwa kulinganisha matini chanzi na matini lengwa kwa msingi wa tashihisi hii, tofauti zifuatazo huibuka. Kwanza, kibainishi ‘**the**’ kimedondoshwa huku neno ‘**fragrance**’ likitafsiriwa kwa njia ya kutoa maelezo kama ‘harufu nzuri’. Kwa mujibu wa nadharia ya tafsiri ya masuala mahususi ya kitamaduni, mkakati huu wa kutoa maelezo ndio unaosababisha ukosefu wa ulinganifu wa kitamathali.

### 3.3 Mahitimisho

Uchunguzi wetu kuhusu ulinganifu wa kitamathali (tamathali ya tashbihi, sitiari na tashihisi) kati ya *Wimbo Ulio Bora* na *Song of Songs* umedhihirisha kuwa kitabu cha *Wimbo Ulio Bora* kikilinganishwa na matini asilia *Song of Songs* kinadhihirisha kwa kiasi kikubwa kutojitokeza kwa lugha ya kitamathali. Njia ambazo hali hii zimejitokeza kwazo katika *Wimbo Ulio Bora* ni kama vile mabadiliko ya kisintaksia yaliyoshuhudiwa katika matini lengwa ikilinganishwa na matini chanzi. Mabadiliko haya hususan yalihusu vivumishi na nomino ambapo kutokana na tofauti za kimuundo kati ya lugha mbili husika ambapo katika lugha ya Kiingereza kivumishi huja kabla ya nomino, tofauti za kisintaksia zilidhihirika kwani katika lugha ya Kiswahili, nomino huja kabla ya kivumishi. Tofauti hizi zilidhihirika katika tamathali zote tatu; tashbihi, sitiari pamoja na tashihisi.

Kutojitokeza kwa lugha ya kitamathali kati ya matini husika pia kulitokana na lugha lengwa kukosa ubainishaji wa kijinsia katika vitengo vya kisarufi kama vile baadhi ya nomino, viwakilishi na hata vivumishi vinavyoakisi jinsia. Sababu nyingine iliyodhihirika katika tamathali zote tatu ni kutafsiri katika matini lengwa kwa kutumia maelezo. Hii vilevile ilitokana na hali kwamba mtagusano kati ya lugha ya Kiingereza na lugha ya Kiswahili kupitia kwa matini mbili tulizorejelea uliibua hali ambapo dhana fulani zinapatikana katika lugha ya Kiingereza lakini hazipo katika lugha ya Kiswahili. Hali kama hii inamlazimu mtafsiri kutumia lugha ya maelezo kuakisi dhana ambazo hazipo moja kwa moja katika matini lengwa.

Sababu nyingine iliyochangia hali ya kutojitokeza kwa lugha ya kitamathali katika matini lengwa ni pale ambapo mtafsiri alitumia misamiati ambayo ama inabana au inapanua katika matini lengwa maana ya dhana husika katika matini chanzi. Hali hii ilidhihirika sana katika mbinu ya sitiari ambapo kulingana na maoni yetu katika baadhi ya mifano ilidhihirika kama udhaifu wa kitafsiri. Udondoshaji vilevile ulidhihirika katika tamathali zote tatu ambapo maneno yaliyodondoshwa ni kibainishi na kiwakilishi kirejeshi kwa kile ambacho kwa maoni yetu kinatokana na lugha lengwa kukosa dhana husika.

Pamoja na haya, nadharia yetu ya tafsiri ya masuala mahususi ya kitamaduni ilitufaa sana katika sura hii. Kwanza, ilitusaidia kuelewa kuwa lugha mbili zinapotagusana katika miktadha ya tafsiri panaibuka masuala ambayo yapo katika lugha chanzi lakini hayapo katika lugha lengwa. Kwa sababu hiyo, nadharia hii ilituelekeza kung'amua kuwa kutojitokeza kwa lugha ya kitamathali kunatokana na tofauti kati ya lugha mbili tulizojikita kwazo; Kiingereza na

Kiswahili kupitia kwa matini *Song of Songs* na *Wimbo Ulio Bora* mtawalia. Aidha nadharia hii ilituwezesha kubaini pale ambapo kulidhihirika udhaifu katika tafsiri hasa pale ambapo mtafsiri alitumia misamiati isiyofaa katika hali ambapo kuna misamiati katika lugha lengwa ya kurejelea dhana husika.

## SURA YA NNE

### MASUALA MAHUSUSI YA KITAMADUNI

#### 4.0 Utangulizi

Katika mchakato wa kutafsiri, mtafsiri anaweza kukumbana na maneno au dhana ambazo zinafungamana na lugha au utamaduni fulani na ambazo hazipo katika lugha nyingine (lengwa). Kwa mujibu wa Axiela (1996), masuala mahususi ya kitamaduni hayajitokezi tu yenyewe, bali ni tokeo la kuhawilisha matini chasili hadi matini lengwa, mchakato unaoibua ugumu kutokana na kutokuwepo kwa masuala au dhana hizo katika utamaduni lengwa. Maelezo haya ya Axiela, yanaashiria kuwa masuala mahususi ya kitamaduni yanadhihirika katika miktadha ya tafsiri na huchochewa na tofauti za kitamaduni kati ya lugha mbili zinazohusika katika tafsiri. Hivi ni kumaanisha kuwa, masuala mahususi ya kitamaduni ni yale ambayo yana umahususi katika utamaduni husika kwa sababu kwa kuchunguza tamaduni mbili zinazohusika katika tafsiri, dhana hizo hazipo au zimepewa hadhi tofauti katika lugha au utamaduni lengwa.

Inaweza kusemwa vilevile kuwa dhana mahususi za kitamaduni huibuka pale ambapo panadhihirika pengo la kiutamaduni katika lugha chanzi na lugha lengwa . Pengo kama hilo hutokea pale ambapo suala katika matini chanzi halipo katika utamaduni lengwa au lugha lengwa inakosa msamiati wa kulirejelea suala hilo. Ili kuliziba pengo kama hili la kitamaduni kati ya lugha husika, na kuibua matini lengwa inayoakisi yaliyomo katika matini chanzi wataalamu mbalimbali wamependekeza kikakati mbalimbali ya kitafsiri. Miongoni mwao ni Newmark (1988) ambaye kwanza anapendekaza makundi matano ya kuainisha masuala haya ya kitamaduni. Mkundi haya ni pamoja na lile linalohusu ikolojia au mazingira, vifaa vya kitamaduni, utamaduni wa asai na taasisi za kijamii, utamaduni wa kazi na burudani pamoja na utamaduni wa ishara na tabia za jamii.

Kwa mujibu wa Newmark (1988), masuala haya yanayodhihirisha upekee katika lugha chanzi; yaani masuala yanayopatikana katika katika lugha chanzi lakini hayapo katika lugha lengwa , huibua changamoto au ugumu kwa mtafsiri katika harakati za kuhawilisha masuala haya kwa lugha lengwa. Ugumu au changamoto hizi huibua haja ya kutumia mikakati mbalimbali ili kuvuka kizingiti hiki cha tafsiri na kufanikisha uhawilishaji huu. Hivi ni kumaanisha kuwa katika kuhawilisha masuala haya mahususi ya kitamaduni kutoka matini chanzi hadi matini lengwa, kwa sababu ya mkakati uliotumika kuhawilisha swala husika, panaweza kudhihirika hali ya kutojitokeza kwa masuala haya, matini chanzi na matini lengwa zinapolinganisha.

Utafiti umeonyesha kuwa kuna masuala mbalimbali mahususi ya kitamaduni ambayo yamedhihirisha ulinganifu na vilevile yale ambayo hayakuonyesha ulinganifu katika masuala haya, matini husika zinapolinganishwa. Kwa hivyo katika sura hii tumeonyesha ulinganifu au kutojitokeza kwa ulinganifu kwa misingi ya nadharia ya Newmark (1988) hasa kuegemea mikakati ya kitafsiri ambayo huweza kuibua tofauti katika masuala husika matini chanzi na matini lengwa zinapolinganishwa.

#### **4.1 Ikolojia**

Kategoria hii ya ikolojia inajumuisha lugha na dhana zinazohusiana na masuala mahususi ya kitamaduni yanayohusu mazingiria ya kiikolojia na ya kijiografia kwa mujibu wa lugha inayotumika katika hali hizo. Hivi ni kumaanisha kuwa kundi hili linajumuisha upana wa lugha na dhana zinazohusiana na wanyama, mimea, pepo pamoja na hali ya nchi kwa kurejelea vitu kama vile milima, mabonde na hata nchi tambarare. Katika sehemu hii, tumeyachunguza masuala haya ili kubaini kuwiana au kutofautiana kwa dhana hizi pamoja na kuhoji ni kwa nini kuna kutojitokeza au kujitokeza kwa dhana hizi mahusi za kitamaduni zinazohusu ikolojia. Kutokana na sababu za kiuchunguzi, tumegawa masuala haya ya kiikolojia katika makundi yafuatayo:

##### **4.1.1 Wanyama na ndege**

Wanyama na vilevile ndege wamejitokeza katika matini chanzi *Song of Songs* na katika kutafsiriwa kwao katika matini lengwa *Wimbo Ulio Bora*, mambo mbalimbali yamejitokeza. Kuna hali ambapo istilahi za kuwatajia wanyama zimehawilishwa katika lugha lengwa kwa njia ambapo kunadhihirika ujitokezaji wa istilahi hizo katika matini lengwa. Kwa mujibu wa nadharia tuliyoitumia ya masuala mahususi ya kitamaduni, hii ni kwa sababu istilahi zote au dhana zote zinapatikana katika utamaduni wa lugha zote. Kwa mfano:

##### **Doves**

Neno hili limetumika mara sita (6) katika matini chanzi. Katika mifano yote sita, neno hili limetafsiriwa kwa njia inayodhihirisha ulinganifu wa kidhana kwa kuwa dhana husika kwa mujibu wa nadharia ya tafsiri ya masuala mahususi ya kitamaduni zinapatikana katika lugha zote. Tazama mfano ufuatao:

***Song of Songs 5:12***

“His eyes are as beautiful as **doves** by a flowing brook, doves washed in milk and standing by the stream.”

***Wimbo Ulio Bora 5:12***

“Macho yake ni kama ya **hua** kandokando ya vijito vya maji, aliyeogeshwa kwenye maziwa, yamepangwa kama vito vya thamani.”

Istilahi ‘dove’ vilevile imejitokeza katika sura ya kwanza mstari wa kumi na tano (1:15) pamoja na sura ya tano mstari wa pili (5:2), sura ya pili mstari wa kumi na nne (2:14), sura ya nne mstari wa kwanza (4:1) pamoja na sura ya sita mstari wa tisa (6:9) ikiwa imetafsiriwa kwa njia sawa na mfano huu.

**Foxes**

Istilahi nyingine ya kuwatajia wanyama ambayo imetumika katika matini chanzi ni ‘foxes’.

Kwa mfano:

***Song of Songs 2:15***

“Catch the **foxes**, the **little foxes**, before they ruin our vineyard in bloom.”

***Wimbo Ulio Bora 2:15***

“Tukamatie **mbweha**, **mbweha wadogo** wale wanaoharibu mashamba ya mizabibu, mashamba yetu ya mizabibu yalichanua.”

Katika mfano huu, neno hili limetafsiriwa kama mbweha, hali inayosababisha ulinganifu wa kitadhana. Ulinganifu huu unatokana na dhana husika kupatikana katika lugha zote husika. Hata hivyo, virai vinavyotokana na neno hili kama vile ‘little foxes’ vinadhihirisha ukosefu wa ulinganifu wa kidhana kwani nomino na kivumishi katika kirai haki vimedhihirisha tofauti za kisintaksia matini chanzi inapolinganishwa na matini lengwa.

**Hart**

Kuna mifano ya istilahi za kutajia masuala mahususi ya kitamaduni ambazo zimedhihirisha kutojitokeza kwazo katika matini lengwa inapolinganishwa na matini chanzi. Mfano kama huu ni neno ‘hart’ ambalo linaashiria jinsia ya kiume katika matini chanzi lakini katika matini lengwa, neno ‘ayala’ ambalo limetumika kama tafsiri ya neno hili haliakisi jinsia. Hali hii kwa mujibu wa nadharia ya tafsiri ya masuala mahususi ya kitamaduni inatokana na dhana husika kukosekana katika lugha lengwa. Tazama mfano ufuatao:



***Song of Songs 2:9***

“My beloved is like a roe or a young **hart**: behold, he standeth behind our wall, he looketh forth at the windows, shewing himself through the lattice.”

***Wimbo Ulio Bora 2:9***

“Mpendwa wangu ni kama paa, au **ayala**. Tazama, asimama nyuma ya ukuta wetu, achungulia dirishani, atazama kimiani.”

Katika mfano huu, neno ‘hart’ ambalo linaashiria jinsia ya kiume katika matini chanzi, limetafsiriwa katika matini lengwa kwa jinsia ambavyo jinsia inayoakisiwa katika matini chanzi haijitokezi katika matini lengwa. Hali hii kwa mujibu wa nadharia ya tafsiri ya masuala mahususi ya kitamaduni inatokana na ukweli kuwa lugha lengwa haina istilahi ya kutajia wanyama hawa kwa njia ambayo inadhihirisha jinsia zao. Neno hili pia limejitokeza katika sura ya pili mstari wa kumi na saba (2:17) pamoja na sura ya nane mstari wa kumi na nne (8:14) ambapo masuala haya haya ya kitafsiri yameibuliwa.

**Hinds**

Mnyama mwingine ambaye ametafsiriwa kwa njia ambayo inadhihirishi ulinganifu kati ya matini mbili husika ni ‘hind’. Neno hili pia limejitokeza katika matini chanzi likiashiria jinsia ya kike. Tazama mfano ufuatao:

***Song of Songs 2:7***

“I charge you, O ye daughters of Jerusalem, by the roes, and by the **hinds** of the field, that ye stir not up, nor awake my love, till he please.”

***Wimbo Ulio Bora 2:7***

“Nawasihi, enyi binti za Yerusalemu, kwa paa na kwa **ayala** wa porini, msiyachochee mapenzi, wala kuyaamsha, hata yatakapoona vema yenyewe.”

Katika mfano huu, neno ‘hind’ ambalo linaashiria jinsia ya kike katika matini chanzi, limetafsiriwa katika matini lengwa kwa jinsi ambavyo jinsia inayoakisiwa katika matini chanzi haijitokezi katika matini lengwa. Hali hii kwa mujibu wa nadharia ya tafsiri ya masuala mahususi ya kitamaduni inatokana na ukweli kuwa lugha lengwa haina istilahi ya kutajia wanyama hawa kwa njia ambayo inadhihirisha jinsia zao. Neno hili pia limejitokeza katika sura ya tau mstari wa kumi na tano (3:5) ambapo masuala haya haya ya kitafsiri yameibuliwa.

## **Mbuzi**

Neno lingine ambalo limetumika liwataja wanyama ni neno ‘goats’ ambalo limetafsiriwa katika matini lengwa kama ‘mbuzi’ linaibua hali ya ulinganifu wa kidhana. Hali hii inatokana na dhana hii kuwepo katika lugha chanzi na vilevile lugha lengwa. Kwa mfano:

### ***Wimbo Ulio Bora 4:1***

“Tazama, u mzuri, mpenzi wangu, u mzuri, macho yako ni kama ya hua, nyuma ya barakoa yako. Nywele zako ni kama **kundi la mbuzi**, wakijilaza mbavuni pa mlima Gileadi.”

### ***Song of Songs 6:5***

“Turn away thine eyes from me, for they have overcome me: thy hair is as a **flock of goats** that appear from Gilead.”

### ***Wimbo Ulio Bora 6:5***

“Uyageuzie macho yako mbali nami, kwa maana yamenitisha sana. Nywele zako ni kama kundi la mbuzi, wakijilaza mbavuni pa Gileadi.”

Katika mifano hii, vilevile, maneno ‘flock of goats’, fungu ambalo limetafsiriwa kama ‘kundi la mbuzi’ yanadhihirisha hali ambapo mkakati wa ulinganifu fafanuzi umetumika kuyatafsiri masuala haya mahususi ya kitamaduni. Hivi ni kumaanisha kuwa mananeo haya yametafsiriwa kimaelezo ama kwa kutoa maelezo yake katika lugha lengwa kwa sababu kwa mujibu wa nadharia ya tafsiri ya masuala mahususi ya kiamaduni, dhana hizi zinakosa misamiati ya kutajia katika lugha lengwa.

## **4.1.2 Mimea**

Kundi hili linadhihirisha hali ya ulinganifu na vilevile kujitokeza kwa ulinganifu katika istilahi husika matini mbili husika zinapolinganishwa. Hali hii kwa mujibu wa ndharia tuliyoitumia ya masuala mahususi ya kitamaduni, hali hi inatokana na dhana husika kupatikana katika lugha chanzi na vilevile lugha lengwa. Tazama mifano ifuatayo:

### ***Song of Songs 7:12***

“Let us get up early to the vineyards; let us see if the vine flourish, whether the tender grape appear, and the **pomegranates** bud forth: there will I give thee my loves.”

### ***Wimbo Ulio Bora 7:12***

“Twende mapema hadi mashamba ya mizabibu, tuone kama mizabibu umechanua, na maua yake yamefunuka; kama **mikomamanga** imetoa maua; huko nitakupa upendo wangu.”

***Song of Songs 2:1***

“I am only a wild flower in Sharon, a **lily** in a mountain valley.”

***Wimbo Ulio Bora 2:1***

“Mimi ni ua la uwandani, ni **fahirisi** ya mabondeni.”

Ulinganifu katika mifano hii unatokana na uhalisia kuwa misamiati ya kurejela dhana husika (pomegranates na lilies) ipo katika lugha lengwa kama ilivyo ‘plants’ (mimea). Aidha, katika mfano ‘apple tree’ uliotafsiriwa kama ‘mti wa mtofaa’ na ‘pomegranate trees’ mikomamanga, panadhihirika hali ambapo lugha mbili husika zinatoa majina hasa ya miti kwa kuihusisha na matunda yatokanayo na miti hiyo.

Kando na mimea hii ambayo imedhihrisha ulinganifu kati ya matini chanzi na matini lengwa, kuna mimea mingine ambayo imedhihirisha kutojitokeza kwa istilahi hizi katika lugha lengwa matini hiyo lengwa ikilinganishwa matini chanzi. Kwa mfano:

***Song of Songs 4:13***

“Thy plants are an orchard of pomegranates, with **pleasant fruits**; camphire, with spikenard,”

***Wimbo Ulio Bora 4:13***

“Machipuko yako ni bustani ya komamanga, yenye **matunda mazuri**, hina na nardo,”

Katika mfano hii mtafsiri kwa mujibu wa nadharia tuliyoitumia ya mtafsiri ya masuala mahususi ya kitamaduni ametumia mkakati wa kitafsiri wa ulinganifu fafanuzi. Hali hii imesababisha kutojitokeza kwa ulinganifu kati ya dhana hii mahususi katika matini lengwa na matini chanzi.

**Rose of Sharon**

Msamiatu huu ambao umetumika katika matini chanzi ukitaja ua mahusui. Tazama mfano ufuatao:

***Song of Songs 2:1***

“I am only a **wild flower in Sharon**, a lily in a mountain valley.”

***Wimbo Ulio Bora 2:1***

“Mimi ni **ua la uwandani**, ni fahirisi ya mabondeni.”

Katika mano huu, fungu ‘flower of Sharon’ ambalo limetafsiriwa kwa njia ya kifasiri kama ‘ua la uwandani’ . Mkakati huu wa kitafsiri ndio unaosababisha ukosefu wa ulinganifu katika dhani hii kati ya matini husika kwa mujibu wa nadharia ya tafsiri ya masuala mahususi ya kitamaduni.

### **Apple tree**

Mfano mwingine ambapo kunaibuka tofauti kati ya matini chanzi na matini lengwa ni pale ambapo maneno ‘apple tree’ yametafsiriwa kama ‘mpera’ . Tazama mfano huu:

#### ***Song of Songs 2:3***

“As the **apple tree** among the trees of the wood, so is my beloved among the sons. I sat down under his shadow with great delight, and his fruit was sweet to my taste.”

#### ***Wimbo Ulio Bora 2:3***

“Kama **mpera** kati ya miti ya msituni, kadhalika mpendwa wangu kati ya vijana. Niliketi kivulini mwake kwa furaha, na matunda yake niliyaonja kuwa matamu.”

Katika tafsiri hii, neno mpera ambalo kwa kawaida huwa ni mti uzao mapera, limetumika kama tafsiri ya ‘apple tree’, hali ambayo inasababisha ukosefu wa ulinganifu katika dhana husika matini chanzi na matini lengwa zinapoliganishwa. Toauti hii inaweza kuwa imetokana na wakati ambapo tafsiri hii ilifanywa (1952) ambapo huenda neno ‘mtofaa’ au ‘mtufaha’ kama ilivyo katika tafsiri za baadaye kama tafsiri ya Biblia Habari Njema (1996) halikuwa limeanza kutumika.

### **4.1.3 Pepo**

Dhana ya pepo kama mojawapo ya dhana katika kundi la kwanza la ikolojia, imejitokeza katika sura ya nne mstari wa kumi na sita. Tazama mfano ufuatao:

#### ***Song of Songs 4:16***

“Awake, O **north wind**; and come, **thou south**; blow upon my garden, that the spices thereof may flow out. Let my beloved come into his garden, and eat his pleasant fruits.”

#### ***Wimbo Ulio Bora 4:16***

“Amka, **kaskazi**; nawe uje, **kusi**; vumeni juu ya bustani yangu, manukato ya bustani yatokee. Mpendwa wangu na aingie bustanini mwake, akayale matunda yake mazuri.”

Mfano huu unadhihirisha ulinganifu kati ya dhana za kitamaduni katika matini mbili husika. Maoni yetu ni kwamba dhana hizi zinapatikana katika lugha mbili husika kwa mujibu wa nadharia tuliyoihusisha katika utafiti huu ya tafsiri ya masuala mahususi ya kitamaduni.

#### 4.1.4 Milima

Milima pia imejitokeza katika matini chanzi; *Song of Songs* na istilahi hizi za kutajia milima inapolinganishwa jinsi zilivyo katika matini chanzi na matini lengwa, masuala tofauti ya kitafsiri huibuka. Tazama mifano ifuatayo:

*Song of Songs 4:1*

“Behold, thou art fair, my love; behold, thou art fair; thou hast doves' eyes within thy locks: thy hair is as a flock of goats, that appear from **mount Gilead**.”

*Wimbo Ulio Bora 4:1*

“Tazama, u mzuri, mpenzi wangu, u mzuri, macho yako ni kama ya hua, nyuma ya barakoa yako. Nywele zako ni kama kundi la mbuzi, wakijilaza mbavuni pa **mlima Gileadi**.”

*Song of Songs 4:6*

“Until the day break, and the shadows flee away, I will get me to the **mountain of myrrh**, and to the **hill of frankincense**.”

*Wimbo Ulio Bora 4:6*

“Hata jua lipunge, na vivuli vikimbie, nitakwenda kwenye **mlima wa manemane**, na kwenye **kilima cha ubani**.”

*Song of Songs 4:8*

“Come with me from Lebanon, my spouse, with me from Lebanon: look from the top of Amana, from the top of Shenir and Hermon, from the lions' dens, from the **mountains of the leopards**.”

*Wimbo Ulio Bora 4:8*

“Bibi arusi, njoo pamoja nami toka Lebanoni, pamoja nami toka Lebanoni. Shuka kutoka kilele cha Amana, kutoka vilele vya Seniri na Hermoni; kutoka mapangoni mwa simba, kutoka **milimani mwa chui**.”

Katika mifano hii, neno ‘mountain’ ambalo limetumika katika sura ya pili mstari wa nane (2:8), sura ya nne mstari wa kwanza (4:1), sura ya pili mstari wa kumi na saba (2:17), sura ya nne mstari wa sita (4:6), sura ya nane mstari wa kumi na nne (8:14) limetafsiriwa kama mlima au milima kutegemea muktadha. Aidha, neno ‘hill’ ambalo limetumika katika sura ya pili mstari wa nane (2:8) pamoja na sura ya nne mstari wa sita (4:6) limetafsiriwa kama kilima au vilima kutegemea muktadha. Hali hii ya ulinganifu katika dhana hizi kati ya matini mbili husika kwa mujibu wa nadharia tuliyoitumia ya tafsiri ya masuala mahususi ya kitamaduni inatokana na hali ambapo lugha chanzi na vile vile lugha lengwa zinatautisha dhana mbili husika na zina misamiati ya kurejelea dhana husika.

#### 4.1.5 Mashamba

Dhana mbalimbali za kurejelea mashamba yamejitokeza katika matini lengwa. Dhana hizi ni pamoja na ‘vineyard au vineyards’ ambayo imejitokeza katika sura ya kwanza mstari wa sita (1:6), dhana ya ‘garden au gardens’ ambayo imejitokeza katika sura ya nne mstari wa kumi na mbili (4:12), sura ya nne mstari wa kumi na tano (4:15), sura ya nne mstari wa kumi na sita (4:16), sura ya tano mstari wa kwanza (5:1), sura ya sita mstari wa pili (6:2), sura ya sita mstari wa kumi na moja (6:11) pamoja na sura ya nane mstari wa kum na tatu (8:13). Dhana nyingine ni ‘orchard’ ambayo imejitokeza katika sura ya nne mstari wa kumi na tatu (4:13). Tazama mifano ifuatayo:

##### *Song of Songs 1:6*

“Look not upon me, because I am black, because the sun hath looked upon me: my mother's children were angry with me; they made me the keeper of the **vineyards**; but mine own **vineyard** have I not kept.”

##### *Wimbo Ulio Bora 1:6*

“Msinichunguze kwa kuwa ni mweusi, kwa sababu jua limeniunguza. Wana wa mamangu walinikasirikia, waliniweka niwe mlinzi wa **mashamba ya mizabibu**; bali **shamba** langu mwenyewe sikulilinda.”

##### *Song of Songs 4:12*

“A **garden** inclosed is my sister, my spouse; a spring shut up, a fountain sealed.”

##### *Wimbo Ulio Bora 4:12*

“**Bustani** iliyofungwa ni dada yangu, bibi arusi, kijito kilichofungwa, chemchemi iliyotiwa mhuri.”

##### *Song of Songs 4:13*

“Thy plants are an **orchard** of pomegranates, with pleasant fruits; camphire, with spikenard,”

##### *Wimbo Ulio Bora 4:13*

“Machipuko yako ni **bustani** ya komamanga, yenye matunda mazuri, hina na nardo,”

Katika kundi hili, maneno ‘orchad’ na ‘garden’ yametafsiriwa kwa neno moja ‘bustani’ huku neno ‘vineyard’ likitafsiriwa kama ‘shamba la mzabibu au mashamba ya mzabibu’ kutegemea mukatadha. Katika mifano hii, inadhihirika kuwa lugha lengwa haitofautishi maneno ‘orchad’ na garden na hivyo panaibuka hali ya kutojitokeza kwa ulinganifu kati ya dhana hizi katika lugha husika kwa mujibu wa nadharia ya tafsiri ya masuala mahususi ya kitamaduni.

#### 4.1.6 Mabonde

Dhana ya mabonde imejitokeza katika sura ya pili mstari wa kwanza (2:1) ikidhihirisha masuala mahususi ya kitafsiri. Tazama mfano ufuatao:

*Song of Songs 2:1*

“I am the rose of Sharon, and the lily of the **valleys**.”

*Wimbo Ulio Bora 2:1*

“Mimi ni ua la uwandani, ni fahirisi ya **mabondeni**.”

Katika mfano huu, ulinganifu wa kidhana kati ya matini mbili husika unadhihirika kwa kuwa lugha zote mbili zina msamiati wa kurejelea dhana ya ‘valley’ kwa mujibu wa nadharia ya tafsiri ya masuala mahususi ya kitamaduni.

#### 4.1.7 Chemchemi na vijito vya maji

Katika matini chanzi, kunajitokeza dhana za kurejelea chemchemi, vijito na visima vya maji. Kwa mfano, kuna dhana ya ‘spring’ katika sura ya nne mstari wa kumi na mbili (4:12), dhana ya ‘fountain’ katika sura ya nne mstari wa kumi na mbili (4:12) na sura ya nne mstari wa kumi na tano (4:15), dhana ya ‘stream’ katika sura ya nne mstari wa kumi na tano (4:15) pamoja dhana ya ‘well’ katika sura ya nne mstari wa kumi na tano (4:15). Dhana ya mwisho ni ya ‘rivers’ katika sura ya tano mstari wa kumi na mbili (5:12). Tazama mifano ifuatayo:

*Song of Songs 4:12*

“A garden inclosed is my sister, my spouse; a **spring** shut up, a **fountain** sealed.”

*Wimbo Ulio Bora 4:12*

“Bustani iliyofungwa ni dada yangu, bibi arusi, **kijito** kilichofungwa, **chemchemi** iliyotiwa mhuri.”

*Song of Songs 4:15*

“A **fountain of gardens**, a well of living waters, and **streams** from Lebanon.”

*Wimbo Ulio Bora 4:15*

“Wewe ndiwe chemchemi ya bustani yangu, kisima cha maji yaliyo hai, **vijito** vya Lebanoni viendavyo kasi.”

*Song of Songs 5:12*

“His eyes are as the eyes of doves by the **rivers** of waters, washed with milk, and fitly set.”

*Wimbo Ulio Bora 5:12*

“Macho yake ni kama hua penye **vijito**, wakioga kwa maziwa, wakiikalia mito iliyojaa;”

Katika kundi hili, dhana ‘spring’, ‘stream’ pamoja na ‘rivers’ zimetafsiriwa kama ‘kijito au vijito’ kutegemea muktadha. Hali hii kwa mujibu wa nadharia ya tafsiri ya masuala mahusi ya kitamaduni inatokana na uhalisia kuwa lugha chanzi inazitofautisha dhana hizi huku lugha lengwa ikikosa misamiati ya kuzirejelea dhana husika na kuzitofautisha. Aidha, maneno ‘fountain’ na ‘well’ yametafsiriwa kama ‘chemchemi’ na ‘kisima’ mtawalia katika hali inayodhihirisha ulinganifu wa kidhana kwa sababu dhana zote zinapatikana katika lugha zote husika kwa mujibu wa nadharia ya tafsiri ya masuala mahususi ya kitamaduni.

#### **4.2 Vifaa vya kitamaduni**

Katika kundi hili la vifaa vya kitamaduni, pia pamedhihirika hali ya ulinganifu wa dhana husika katika matini zote mbili kwa sababu dhana husika zinapatikana katika lugha ya Kiingereza na Kiswahili. Dhana hizi katika matini chanzi ni pamoja na:

##### **Thread**

Dhana hii imejitokeza katika sura ya nne msatri wa tatu (4:3) ikidhihirisha ulinganifu wa kidhana kati ya matini chanzi na matini lengwa. Tazama mfano huu:

##### ***Song of Songs 4:3***

“Thy lips are like a **thread** of scarlet, and thy speech is comely:  
thy temples are like a piece of a pomegranate within thy **locks**.”

##### ***Wimbo Ulio Bora 4:3***

“Midomo yako ni kama **uzi** mwekundu, na kinywa chako ni kizuri; mashavu yako ni kama nusu kipande cha komamanga, nyuma ya barakoa yako.”

Katika mfano huu, neno ‘thread’ limetafsiriwa kama ‘uzi’, hali inayohirisha ulinganifu wa kidhana kwa kuwa dhana hii inapatikana katika lugha zote husika kwa mujibu wa nadharia ya tafsiri ya masuala mahususi ya kitamaduni.

##### **Myrrh**

Dhana hii imejitokeza katika matini chanzi mara nane. Mifano hii inapatikana katika sura ya kwanza mstari wa tatu (1:13), sura ya tatu mstari wa sita (3:6), sura ya nne mstari wa sita (4:6), sura ya nne mstari wa kumi na nne (4:14), sura ya tano mstari wa kwanza (5:1), sura ya tano mstari wa tano (5:5) pamoja na sura ya tano mstari wa kumi na tatu (5:13). Katika mifano yote hii, neno hili limetafsiriwa kama ‘manemane’.



***Song of Songs 5:1***

“I am come into my garden, my sister, my spouse: I have gathered my **myrrh** with my spice; I have eaten my honeycomb with my honey; I have drunk my wine with my milk: eat, O friends; drink, yea, drink abundantly, O beloved.”

***Wimbo Ulio Bora 5:1***

“Naingia bustanini mwangu, dada yangu, bibi arusi, nachuma **manemane** yangu na rihani, nala sega la asali na asali yangu, nanywa divai yangu na maziwa. Kaleni, rafiki zangu, kanyweni, naam, nyweni sana, wapendwa wangu.”

***Song of Songs 5:13***

“His cheeks are as a bed of spices, as sweet flowers: his lips like lilies, dropping sweet smelling **myrrh**.”

***Wimbo Ulio Bora 5:13***

“Mashavu yake ni kama matuta ya rihani ambayo hufanyizwa manukato; midomo yake ni kama nyinyoro, inadondosha matone ya **manemane**;”

Katika tafsiri ya neno hili, kunaibuka hali ya ukosefu wa ulinganifu wa kidhana. Hali hii kwa mujibu wa nadharia ya tafsiri ya masuala mahususi ya kitamaduni inatokana na kuwepo kwa dhana husika katika lugha zote husika.

**Marble**

Dhana hii imejitokeza mara moja katika matini chanzi. Katika mfano huu, kunadhihirika ulinganifu wa kidhana kwa sababu kwa mujibu wa nadharia ya tafsiri ya masuala mahususi ya kitamaduni dhana hii inapatikana katika lugha zote husika. Tazama mfano ufuatao:

***Song of Songs 5:15***

“His legs are as pillars of **marble**, set upon sockets of fine gold: his countenance is as Lebanon, excellent as the cedars.”

***Wimbo Ulio Bora 5:15***

“Miguu yake ni kama nguzo za **marimari**, zilizowekwa juu ya misingi ya dhahabu; sura yake ni kama Lebanoni, ni bora mfano wa mierezi;”

**Banner**

Dhana hii imejitokeza mara tatu katika matini chanzi. Mifano hii imejitokeza katika sura ya pili mstari wa nne (2:4), sura ya sita mstari wa nne (6:4) pamoja na sura ya sita mstari wa kumi (6:10). Katika mifano hii, dhana hii imedhihirisha ulinganifu wa kidhana kama ilivyo katika mfano ufuatao:

***Song of Songs 6:4***

“Thou art beautiful, O my love, as Tirzah, comely as Jerusalem, terrible as an **army** with **banners**.”

***Wimbo Ulio Bora 6:4***

“Mpenzi wangu, u mzuri kama Tirza, mwenye kupendeza kama Yerusalemu, wa kutisha kama jeshi lenye **bendera**.”

Katika mfano huu, dhana hii imedhihirisha ulinganifu wa kidhana kwani dhana husika kwa mujibu wa nadharia ya tafsiri ya masuala mahususi ya kitamaduni, inapatikana katika lugha zote husika.

**Garments**

Dhana hii imetumika mara moja katika sura ya nne mstari wa kumi na moja (4:11) kama ilivyo katika mfano huu:

***Song of Songs 4:11***

“Thy lips, O my spouse, drop as the honeycomb: honey and milk are under thy tongue; and the smell of thy **garments** is like the smell of Lebanon.”

***Wimbo Ulio Bora 4:11***

“Bibi arusi, midomo yako yadondosha asali, asali na maziwa viko chini ya ulimi wako; na harufu ya **mavazi** yako ni kama harufu ya Lebanoni.”

Katika mfano huu, dhana hii vilevile inadhihirisha ulinganifu kati ya matini mbili husika kwa sababu inapatikana katika lugha zote zinazohusika katika tafsiri husika.

**Gold**

Neno hili ‘gold’ limetumika mara sita katika matini chanzi ambapo ni katika sura kwanza mstari wa kumi (1:10), sura ya kwanza mstari wa kumi na moja (1:11), sura ya tatu mstari wa kumi (3:10), sura ya tano mstari wa kumi na moja (5:11), sura ya tano mstari wa kumi na nne (5:14) pamoja na sura ya tano mstari wa kumi na tano (5:15). Katika mifano hii, neno hili limetafsiriwa kama ‘dhahabu’, hali inayoibua ulinganifu wa kidhana. Hali hii kwa mujibu wa nadharia ya tafsiri ya masuala mahususi ya kitamaduni inatokana na kuwepo kwa dhana husika katika lugha zote husika. Tazama mfano ufuatao:

***Song of Songs 5:14***

“His hands are as **gold** rings set with the beryl: his belly is as bright ivory overlaid with sapphires.”

***Wimbo Ulio Bora 5:14***

“Mikono yake ni kama mianzi ya **dhahabu**, iliyopambwa kwa zabarajadi; kiwiliwili chake kama kazi ya pembe, iliyonakishiwa kwa yakuti samawi;”

**Wine**

Dhana hii imejitokeza mara sita katika matini lengwa ambapo ni katika sura ya kwanza mstari wa pili (1:2), sura ya kwanza mstari wa nne (1:4), sura ya nne mstari wa kumi (4:10), sura ya tano mstari wa kwanza (5:1), sura ya saba mstari wa tisa (7:9) pamoja na sura ya nane mstari wa pili (8:2). Tazama mfano ufuatao:

***Song of Songs 7:9***

“And the roof of thy mouth like the best **wine** for my beloved, that goeth down sweetly, causing the lips of those that are asleep to speak.”

***Wimbo Ulio Bora 7:9***

“Na kinywa chako kama **divai** iliyo bora, kwa mpendwa wangu inashuka taratibu, ikitiririka midomoni mwao walalao.

Katika mfano huu, sawa na mifano mingine kama ilivyotajwa hapo juu, neno hili limetafsiriwa kama divai, hali inayoibua ulinganfu wa kidhana kati ya matini mbili husika. Hali hii kwa mujibu wa nadharia ya tafsiri ya masuala mahususi ya kitamaduni inatokana na dhana husika kupatikana katika lugha zote husika.

**Tents**

Dhana hii imejitokeza katika matini chanzi mara mbili katika sura ya kwanza mstari wa tano (1:5) pamoja na sura ya kwanza mstari wa nane (1:8). Tazama mfano huu:

***Song of Songs 1:5***

“I am black, but comely, O ye daughters of Jerusalem, as the **tents of Kedar**, as the curtains of Solomon.”

***Wimbo Ulio Bora 1:5***

“Mimi ni mweusi mweusi, lakini napendeza, enyi binti za Yerusalemu, mfano wa **hema za Kedari**, kama mapazia yake Sulemani.”

Katika tafsiri ya dhana hii, masuala mbalimbali ya kitafsiri yanaibuka. Kwanza, dhana hii inadhihirisha ulinganifu wa kidhana kati ya lugha chanzi na lugha lengwa ambapo imetafsiriwa kama ‘mahema’. Vilevile dhana hii katika muktadha wa mfano huu ‘tents of Kedar’, fungu ambalo limetafsiriwa kama ‘mapazia ya Kedari’; tafsiri ilifanywa kwa njia ya kuhawilisha. Mkakati huu wa kuhawilisha kwa mujibu wa nadharia ya tafsiri ya masuala mahususi ya

kitamaduni unasababisha ukosefu wa kidhana kwa kuwa dhana husika inakosa mguso kamili wa lugha lengwa.

### **Tower**

Dhana hii imejitokeza mara nne katika matini chanzi amabapo ni katika sura ya nne mstari wa nne (4:4), sura ya saba mstari wa nne (7:4) pamoja na sura ya nane mstari wa kumi (8:10). Katika mifano hii, neno ‘tent’ limetafsiriwa kama ‘mnara’ hali inayoibua ulinganifu wa kidhana. Tazama mifano ifuatayo:

#### ***Song of Songs 4:4***

“Thy neck is like the **tower of David** builded for an armoury, whereon there hang a thousand bucklers, all shields of mighty men.”

#### ***Wimbo Ulio Bora 4:4***

“Shingo yako ni kama **mnara wa Daudi**, uliojengwa pa kuwekea silaha; ngao elfu zimetungikwa juu yake, zote ni ngao za mashujaa.”

#### ***Song of Songs 7:4***

“Thy neck is as a **tower of ivory**; thine eyes like the fishpools in Heshbon, by the gate of Bath-rabbim: thy nose is as the **tower of Lebanon** which looketh toward Damascus.”

#### ***Wimbo Ulio Bora 7:4***

“Shingo yako ni kama huo **mnara wa pembe**; macho yako kama viziwa vya Heshboni, karibu na mlango wa Beth-rabi; pua yako ni kama **mnara wa Lebanoni**, unaoelekea Dameski;”

Hata hivyo, virai vinavyotokana na dhana hii kama vile ‘tower of ivory’ vimetafsiriwa kupitia mkakati wa tafsiri ya moja kwa moja. Mkakati huu kwa mujibu wa nadharia ya tasiri ya masuala mahususi ya kitamaduni unasababisha ukosefu wa ulinganifu wa kidhana.

### **Frankincense**

Dhana hii imetumika katika matini chanzi mara tatu ambapo ni katika sura ya tatu mstari wa sita (3:6), sura ya nne mstari wa sita (4:6) pamoja na sura ya nne mstari wa kumi na nne (4:14). Tazama mfano ufuata:

#### ***Song of Songs 3:6***

“Who is this that cometh out of the wilderness like pillars of smoke, perfumed with myrrh and **frankincense**, with all powders of the merchant?”

***Wimbo Ulio Bora 3:6***

“Ni nani huyu apandaye kutoka nyikani, mfano wake ni nguzo za moshi; afukizwa **manemane** na ubani, na mavumbi ya manukato yote ya mchuuzi?”

Neno hili katika mifano yote husika, limetafsiriwa kama ‘ubani’. Tafsiri hii inapanua maana ya ‘frankincense’ kwa kuwa ‘frankincense’ ni aina ya ‘incense’ dhana ambayo ndiyo hutafsiriwa kama ‘ubani’. Hali hii kwa mujibu wa nadharia ya tafsiri ya masuala mahususi ya kitamaduni inatokana na lugha chanzi kutofautisha dhana mbili husika ilhali lugha lengwa haizitofautishi dhana husika.

**Spice**

Neno hili limetumika limejitokeza mara nane (8) katika matini chanzi ambapo ni katika sura ya nne mstari wa kumi (4:10), sura ya nne mstari wa kumi na nne (4:14), sura ya nne mstari wa kumi na sita (4:16), sura ya tano mstari wa kwanza (5:1), sura ya tano mstari wa kumi na tatu (5:13), sura ya sita mstari wa pili (6:2), sura ya nane mstari wa pili (8:2), sura ya nane mstari wa kumi na nne (8:14). Katika mifano hii, tafsiri ya dhana hii imedhihirisha masuala mbalimbali ya kitafsiri. Kwanza, kuna mifano ambapo dhana hii imetafsiriwa kama ‘manukato’. Hali hii imedhihirika katika sura ya nne mstari wa kumi (4:10), sura ya nne mstari wa kumi na sita (4:16) pamoja na sura ya nane mstari wa kumi na nne (8:14). Tazama mfano ufuatao:

***Song of Songs 4:10***

“How fair is thy love, my sister, my spouse! how much better is thy love than wine! and the smell of thine ointments than all **spices!**”

***Wimbo Ulio Bora 4:10***

“Jinsi pendo lako lilivyo nzuri, dada yangu, bibi arusi, ni nzuri kupita divai; na harufu ya marhamu yako yapita **manukato** ya kila namna.”

Tafsiri nyingine ya dhana hii ni pale ambapo mtafiri ametumia neno ‘rihani’ kutafsiri ‘spice’. Mwekeo huu wa kutafsiri dhana husika umejitokeza katika sura ya sita mstari wa pili (6:2), sura ya tano mstari wa kwanza (5:1) pamoja na sura ya tano mstari wa kumi na tatu (5:13). Tazama mfano ufuatao:

***Song of Songs 5:1***

“I am come into my garden, my sister, my spouse: I have gathered my myrrh with my **spice**; I have eaten my honeycomb with my honey; I have drunk my wine with my milk: eat, O friends; drink, yea, drink abundantly, O beloved.”

***Wimbo Ulio Bora 5:1***

“Naingia bustanini mwangu, dada yangu, bibi arusi, nachuma manemane yangu na **rihani**, nala sega la asali na asali yangu, nanywa divai yangu na maziwa. Kaleni, rafiki zangu, kanyweni, naam, nyweni sana, wependwa wangu.”

Mwisho, kuna mifano ambayo inasawiri dhana hii ikitafsiriwa kama ‘kolezi’. Mifano kama hii inapatikana katika sura ya nane mstari wa pili (8:2) pamoja na sura ya nne mstari wa kumi na nne (4:14). Tazam mfao huu:

***Song of Songs 4:14***

“Spikenard and saffron; calamus and cinnamon, with all trees of frankincense; myrrh and aloes, with all the chief **spices**.”

***Wimbo Ulio Bora 4:14***

“Nardo na zafarani, mchai na mdalasini, na miti yote iletayo ubani, manemane na udi, na **kolezi** kuu zote.”

Katika mifano yote hii, tafsiri husika zimeibua hali ya ukosefu wa ulinganifu wa kidhana kwa kuwa misamiati mitatu iliyotumika haiakisi dhana husika kama ilivyo katika lugha lengwa. Hali hii kwa mujibu wa nadharia ya tafsiri ya masuala mahususi ya kitamaduni inatokana na dhana husika kukosekana katika lugha lengwa.

Licha ya vifaa hivi vya kitamaduni kudhahirisha ulinganifu wa kidhana kati ya matini mbili husika, virai vinavyotokana na vifaa hivi kama vile ‘chief spices’ ambacho kimetafsiriwa kama ‘kolezi kuu’ na vilevile ‘best wine’ ambacho kimetafsiriwa kama ‘divai iliyo bora’ vinadhahirisha ukosefu wa ulinganifu wa kidhana kwani vimetafsiriwa kijumla bila kuakisi masuala mahususi katika virai husika kwenye matini chanzi. Aidha, virai ‘my spice’ ambacho kimetafsiriwa kama ‘kolezi’ pamoja na kirai ‘my myrrh’ vimedhahirisha ukosefu wa ulinganifu kwa sababu za tofauti katika muundo wa kisintaksia pamoja na udondoshaji wa vipashio muhimu katika matini chanzi wakati wa kuhawilishwa hadi matini lengwa. Kwa sababu hizi, vifaa hivi vya kitamaduni vinadhahirisha kiwango kikubwa cha ukosefu wa ulinganifu wa kidhana matini chanzi na matini lengwa zinapolinganishwa.

### **4.3 Utamaduni wa asasi na taasisi za kijamii**

Asasi mbalimbali zimeakisiwa katika matini chanzi ambazo katika kuhawilishwa kwazo hadi lugha lengwa, masuala fulani ya kitafsiri huibuka. Asasi ambazo ziliibuka ni kama vile asasi ya kijeshi, asasi ya ufalme pamoja na asasi ya ndoa. Tazama mifano ifuatayo:

***Song of Songs 3.7***

“Behold his bed, which is Solomon's; threescore valiant men are about it, of the valiant of Israel.” (asasi ya kijeshi)

***Wimbo Ulio Bora 3:7***

“Tazama, ni machela yake Sulemani; mashujaa sitini waizunguka, wa mashujaa wa Israeli.”

***Song of Songs 3.9***

“King Solomon made himself a chariot of the wood of Lebanon.” (asasi ya ufalme)

***Wimbo Ulio Bora 3:9***

“Mfalme Sulemani alijitengenezea machela ya miti ya Lebanoni;”

***Song of Songs 3.11***

“Go forth, O ye daughters of Zion, and behold king Solomon with the crown wherewith his mother crowned him in the day of his espousals, and in the day of the gladness of his heart.” (asasi ya ndoa)

***Wimbo Ulio Bora 3:11***

“Tokeni, enyi binti za Sayuni, mtazameni Mfalme Sulemani, amevaa taji alilovikwa na mamaye, siku ya posa yake, siku ya furaha ya moyo wake.”

Katika kundi la utamaduni wa asasi na taasisi za kijamii, asasi zote zimehawilishwa kwa njia inayodhihirisha ulinganifu wa dhana husika katika matini zote mbili. Hali hii kwa mujibu wa nadharia ya tafsiri ya masuala mahususi ya kitamaduni ni kwa sababu dhana hizi zimeakisiwa kwa njia ya kiurejelzi na hivyo urejelezi huo umejitokeza pia katika matini lengwa.

#### **4.4 Utamaduni wa kazi na burudani**

Kazi mbalimbali zimeakisiwa katika matini chanzi. Kazi hizi ni pamoja na ususi au ufumaji, uchungaji, usonara, ulinzi pamoja na useremala. Kazi hizi zinapohawilishwa hadi matini lengwa, masuala fulani ya kitafsiri huibuka. Tazama mifano ifuatayo:

***Song of Songs 1:5***

“I am black, but comely, O ye daughters of Jerusalem, as the tents of Kedar, as the curtains of Solomon.” (ususi)

***Wimbo Ulio Bora 1:5***

“Mimi ni mweusi, lakini napendeza, enyi binti za Yerusalemu, mfano wa hema za Kedari, kama mapazia yake Sulemani.”

***Song of Songs 1:7***

“Tell me, O thou whom my soul loveth, where thou feedest, where thou makest thy flock to rest at noon: for why should I be as one that turneth aside by the flocks of thy companions?”  
(uchungaji)

***Wimbo Ulio Bora 1:7***

“Nijulishe, ee mpendwa wa nafsi yangu, ni wapi utakapolisha kundi lako, ni wapi utakapolilaza aduhuri. Kwa nini niwe kama aliyefungiwa shela, karibu na makundi ya wenzako?”

***Song of Songs 1:8***

“If thou know not, O thou fairest among women, go thy way forth by the footsteps of the flock, and feed thy kids beside the shepherds' tents.” (ususi na uchungaji)

***Wimbo Ulio Bora 1:8***

“Usipojua, wewe uliye mzuri katika wanawake, shika njia uzifuate nyayo za kondoo, na kuwalisha wana-mbuzi wako karibu na hema za wachungaji.”

***Song of Songs 1:10***

“Thy cheeks are comely with rows of jewels, thy neck with chains of gold.” (usonara – vyombo vya dhahabu)

***Wimbo Ulio Bora 1:10***

“Mashavu yako ni mazuri kwa mashada, shingo yako kwa mikufu ya vito.”

***Song of Songs 1:11***

“We will make thee borders of gold with studs of silver.”  
(usonara – vyombo vya dhahabu)

***Wimbo Ulio Bora 1:11***

“Tutakutengenezea mashada ya dhahabu, yenye vifungo vya fedha.”

***Song of Songs 3:3***

“The watchmen that go about the city found me: to whom I said, Saw ye him whom my soul loveth?” (ulinzi)

***Wimbo Ulio Bora 3:3***

“Walinzi wazungukao mjini waliniona; Je! Mmemwona mpendwa wa nafsi yangu? ”

***Song of Songs 3:9***

“King Solomon made himself a chariot of the wood of Lebanon.” (useremala)



***Wimbo Ulio Bora 3:9***

“Mfalme Sulemani alijitengenezea machela ya miti ya Lebanoni.”

Kundi hili la utamadui wa kazi na burudani sawa na lile la utamaduni wa asasi na taasisi za kijamii, dhana zote zimehawilishwa kwa njia inayodhihirisha ulinganifu wa dhana husika katika matini zote mbili. Hali hii kwa mujibu wa nadharia ya tafsiri ya masuala mahususi ya kitamaduni ni kwa sababu dhana hizi zimeakisiwa kwa njia ya kiurejelezi na hivyo urejelezi huo umejitokeza pia katika matini lengwa.

**4.5 Utamaduni wa ishara na tabia**

Katika matini chanzi ya Song of Songs, ishara na tabia mbalimbali zimedhihirika. Ishara na tabia hizi zinapohawilishwa hadi matini lengwa, masuala mbalimbali ya kitafsiri huibuka.

Tazama mifano ifuatayo:

***Song of Songs 1:2***

“Let him kiss me with the kisses of his mouth: for thy love is better than wine.” (**ishara ya mapenzi**)

***Wimbo Ulio Bora 1:2***

“Heri midomo yako inibusu, maana pendo lako ni bora kuliko divai.”

***Song of Songs 2:7***

“I charge you, O ye daughters of Jerusalem, by the roes, and by the hinds of the field, that ye stir not up, nor awake my love, till he please.” (**tabia ya kuapa**)

***Wimbo Ulio Bora 2:7***

“Nawasihi, enyi binti za Yerusalemu, kwa paa na kwa ayala wa porini, msiyachochee mapenzi, wala kuyaamsha, hata yatakapoona vema yenyewe.”

***Song of Songs 8:1***

“O that thou wert as my brother, that sucked the breasts of my mother! when I should find thee without, I would kiss thee; yea, I should not be despised.” (**tabia ya kuonyesha mapenzi hadharani haikubaliki**)

***Wimbo Ulio Bora 8:1***

“Laiti ungekuwa kama ndugu yangu, aliyeyanyonya matiti ya mamangu! Kama ningekukuta huko nje, ningekubusu, asinidharau mtu.”

***Song of Songs 8:6***

“Set me as a seal upon thine heart, as a seal upon thine arm: for love is strong as death; jealousy is cruel as the grave: the coals

thereof are coals of fire, which hath a most vehement flame.”  
(ishara ya uaminifu)

***Wimbo Ulio Bora 8:6***

“Nitie kama mhuri moyoni mwako, kama mhuri juu ya mkono wako; kwa maana upendo una nguvu kama mauti, ka wivu ni mkali kama ahera. Mwako wake ni mwako wa moto na miali yake ni miali ya Yahu.”

Ishara na tabia ambazo zimedhihirika katika mifano hii ni pamoja na tabia ya kuonyesha mapenzi kwa njia ya busu, tabia ya kuapa kwa njia ya wanyama, tabia ya kuonyesha mapenzi hadharani haikubaliki pamoja na ishara ya uaminifu au udhati wa jambo wa njia ya kutia muhuri. Kundi hili la ishara na tabia za kijamii linaakisi dhana zote zikiwa zimehawilishwa kwa njia inayodhihirisha ulinganifu wa dhana husika katika matini zote mbili. Hali hii kwa mujibu wa nadharia ya tafsiri ya masuala mahususi ya kitamaduni ni kwa sababu dhana hizi zimeakisiwa kwa njia ya kiurejelezi na hivyo urejelezi huo umejitokeza pia katika matini lengwa.

#### **4.6 Mahitimisho**

Sura hii kimsingi imeshughulikia dhana mahususi za kitamaduni ambapo tumetalii jinsi ambapo dhana hizi zimejitokeza katika matini chanzi *Song of Songs*. Pamoja na kuonyesha dhana hizi katika matini chanzi, tumezibainisha katika matini lengwa *Wimbo Ulio Bora* lengo letu likiwa ni kutathmini kujitokeza au kutojitokeza kwa dhana hizi katika matini lengwa. Jukumu hili tumelitekeleza kwa kufuata makundi matano ya masuala mahususi ya kitamaduni aliyopendekeza Newmark (1988) ambayo ni pamoja na ikolojia, vifaa vya kitamaduni, utamaduni wa asasi na taasisi za kijamii, utamaduni wa kazi na burudani na mwisho utamaduni wa ishara na tabia.

Uchunguzi wetu umedhihirish kuwa kwa kulinganisha matini zote husika, kunazo hali ambapo kunajitokeza ulinganifu wa dhana hizi katika matini chanzi na matini lengwa. Hali hii inatokana na kuwepo kwa dhana hizi katika lugha chanzi na vilevile lugha lengwa. Adha, kunazo hali ambapo kunadhihirika kutojitokeza kwa dhana hizi katika matini lengwa ikilinganishwa na matini chanzi. Kwa mujibu wa utafiti wetu, kutojitokeza huku kunatokana na dhana hizi kutokuwepo katika lugha lengwa, jambo linalomfanya mtafsiri kutumia mikakati mbalimbali kama alivyopendekeza Newmark (1988). Mikakati hii kulingana na utafiti wetu ndiyo inaibua hali ya kutokuwa na ulinganifu katika dhana hizi katika matini mbili husika. Miongoni mwa mikakati ambayo imetumik ni uhawilishaji, ulinganifu fafanuzi, udondoshi,

maelezo ya ziada na hata mikakati jumuishi. Katika makundi yote matano, panajitokeza hali ya kujitokeza kwa dhana hizi za kitamaduni katika matini lengwa tukiilinganisha na matini chanzi. Hata hivyo, makundi yaliyodhihirisha ujitokezaji wa dhana hizi ni yale ya utamaduni wa asasi na taasisi za kijamii, utamaduni wa kazi na burudani na ya utamaduni wa ishara na tabia. Vilevile, matokeo ya uchunguzi wetu yanashiria kuwa makundi yaliyoonyesha kutojikeza kwa dhana hizi mahususi za kitamaduni ni yale ya ikolojia na vifaa vya kitamaduni; makundi ambayo ndiyo yamedhihirisha mifano mingi zaidi katika matini zote. Kimsingi, tumepata kutokana na uchunguzi wetu kuwa kwa kulinganisha matini lengwa ***Wimbo Ulio Bora*** na matini chanzi ***Song of Songs***, kuna kiasi kikubwa cha kutojitokeza kwa masuala mahususi ya kitamaduni. Hali hii tumehusisha na tofauti kati ya lugha mbili husika ambazo ni lugha ya Kiingereza katika matini chanzi na lugha ya Kiswahili katika matini lengwa.

## SURA YA TANO

### HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

#### 5.0 Utangulizi

Utafiti huu ulilenga kuchunguza kutojitokeza kwa lugha ya kitamathali na urejeleaji wa kijinsia katika *Wimbo Ulio Bora* kama matini lengwa, matini hii inapolinganishwa na matini chanzi *Song of Songs*. Kwa msingi huu, utafiti wetu ulikuwa utafiti linganishi ambapo matini tulizojikita kwazo zilikuwa ni kitabu cha *Song of Songs* katika lugha ya Kiingereza na tafsiri yake katika lugha ya Kiswahili; *Wimbo Ulio Bora*.

Nadharia iliyoongoza kazi yetu ilikuwa ni nadharia ya Newmark (1988) ya masuala mahususi ya kitamaduni mwegemeo wetu ukiwa kwenye kuonyesha ulinganifu wa kitamathali na wa urejeleaji wa kijinsia katika matini mbili husika. Tafsiri ya bibilia tuliyoitumia ni ya King James Version katika lugha ya Kiingereza na Swahili Union Version katika lugha ya Kiswahili.

#### 5.1 Hitimisho

Utafiti huu ulikusudia kuchunguza kutojitokeza kwa lugha ya kitamathali pamoja na urejeleaji wa kijinsia katika *Wimbo Ulio Bora* kwa kukilinganisha kitabu hiki na matini asilia *Song of Songs*. Utafiti huu uliongozwa na madhumuni matatu yafuatayo: Kwanza, tulilenga kuchunguza ili kubaini kujitokeza au kutojitokeza kwa lugha inayoashiria urejeleaji wa kijinsia katika *Wimbo Ulio Bora* matini hii ikilinganishwa na matini chanzi *Song of Songs*. Kuhusu suala hili, uchunguzi wetu ulibaini kuwa kuna hali ya urejeleaji wa kijinsia katika matini chasili *Song of Songs* ambapo lugha inayorejelea jinsia ya kike na ya kiume imebainika wazi. Utafiti wetu aidha umebaini kuwa urejeleaji huu wa kijinsia umebainika katika matapo mbalimbali huku jinsia ya kike na ya kiume zikidhihirika katika matapo yote. Matapo haya ni pamoja na tapo la nomino jumla au nomino ya kawaida zinazoakisi jinsia ya kike na ya kiume. Nomino hizi zinataja wanyama na hata binadamu na katika hali zote hizo kulidhihirika kiasi kikubwa cha kutodhihirika kwa urejeleaji wa kijinsia katika matini lengwa.

Tapo lingine ni lile lililohusu virai nomino vinavyoakisi jinsia ya kike na ya kiume. Virai hivi, sawa na nomino ya kawaida vilidhihirisha kiasi kikubwa cha kutojitokeza kwa ulinganifu wa kijinsia matini chanzi inapolinganishwa na matini lengwa. Pamoja na matapo haya, pia palikuwa na tapo la viwakilishi vinavyoakisi jinsia. Viwakilishi hivi vilikuwa ni vile virejeshi, vimilikishi, vya mtenda pamoja na vya yambwa. Tapo hili ndilo lilionyesha kiasi kikubwa zaidi cha kutojitokeza kwa ulinganifu wa kijinsia huku takriban viwakilishi vyote vikionyesha

kutojitokeza kwa ulinganifu huu wa kijinsia. Tapo la mwisho ni lile lililohusu vivumishi vya sifa ambapo kama matapo mengine, tapo hili pia lilidhihirisha kutojitokeza kwa urejeleaji wa kijinsia. Kimsingi, utafiti wetu ulionyesha kuwa kitabu cha *Song of Songs* kinadhihirisha urejeleaji unaohusu jinsia. Hata hivyo kitabu hicho kama matini chanzi kikilinganishwa na matini lengwa *Wimbo Ulio Bora*, panadhihirika ukosefu wa ulinganifu katika urejeleaji wa kijinsia. Hali hii tulihusisha na tofauti kati ya lugha chanzi na lugha lengwa katika ubainishaji wa masuala ya kijinsia. Aidha tumeihsisha hali hii na mbeko katika tafsiri hasa pale ambapo mtafsiri anahiari kutumia neno lisiloakisi jinsia katika matini lengwa wakati ambapo pana neno katika matini lengwa ambalo linaweza kutumika katika muktadha husika kuakisi jinsia husika.

Lengo letu la pili lilihusu kuchunguza ni kwa kiasi gani kuna kutojitokeza kwa ulinganifu wa kitamathali kati ya *Wimbo Ulio Bora* matini hii ikilinganishwa na matini chanzi ya *Song of Songs*. Kuhusiana na lengo hili, tulijikita katika tamathali tatu pekee ambazo zilikuwa ni tashbihi, tashihisi pamoja na sitiari. Tamathali hizi zote tatu zilidhihirika katika matini chanzi na matini lengwa ambapo utafiti wetu ulionyesha kuwa matini lengwa ikilinganishwa na matini chanzi, kunadhihirika kiasi kikubwa cha kutojitokeza kwa ulinganifu wa kitamathali wa tamathali husika. Utafiti wetu umeonyesha kuwa kutojitokeza huku kwa lugha ya kitamathali katika matini lengwa kunatokana na sababu mbalimbali. Kwanza ni pale ambapo tamathali ya aina fulani katika matini chanzi inageuka kuwa ya aina tofauti katika matini lengwa. Kwa mfano, hali ambapo sitiari katika matini chanzi inabadilika kuwa tashbihi katika matini lengwa.

Jambo lingine ambalo lilisababisha kutojitokeza kwa lugha ya kitamathali ni pale ambapo mpangilio wa kisintaksia wa maneno katika matini chanzi unatofautiana na ule uliopo katika matini lengwa. Hali hii ilijitokeza hasa kwenye virai nomino ambapo kivumishi na nomino zilibadili nafasi zao kutokana na mpangilio tofauti kuhusu aina hizi mbili za maneno katika lugha lengwa na lugha chanzi. Suala lingine ambalo lilisababisha tofauti za kitamathali kati ya matini mbili husika ni tofauti kati ya lugha husika katika kubainisha jinsia. Kwa sababu hii, pale ambapo lugha lengwa ilikosa kudhihirisha jinsia iliyopo kwenye matini asilia basi pakatokea hali ya kutojitokeza kwa ulinganifu wa kitamathali. Pamoja na sababu hizi, uchunguzi wetu ulibaini kuwa kunazo hali ambapo ukosefu wa ulinganifu wa kitamathali ulisababishwa na mtafsiri kutumia neno ambalo ama linabana au linapanua dhana au maana ya dhana fulani katika matini lengwa.

Mwisho, tulijitahidi kuzidadavua dhana mahususi za kitamaduni na jinsi ya kujitokeza kwake katika matini lengwa tukilinganisha na matini chanzi kwa lengo la kubainisha changamoto zinazohusiana na uhawilishaji wa dhana mahususi za kitamaduni kati ya matini chanzi na matini lengwa. Utafiti wetu ulibaini kuwa dhana hizi mahususi za kitamaduni katika *Song of Songs* zimedhihirika katika makundi matano kama alivyopenekeza Newmark (1988) ambayo ni pamoja na kundi la ikolojia, kundi la vifaa vya kitamaduni, kundi la utamaduni wa kazi na burudani, kundi la utamaduni la asasi na taasisi za kitamaduni, pamoja na utamaduni wa ishara na tabia za kijamii. Makundi haya yanadhihirisha kiwango kikubwa cha kutojitokeza kwa ulinganifu katika masuala haya mahususi ya kitamaduni, matini mbili husika zinapolinganishwa. Kutojitokeza huku kwa dhana hizi mahususi za kitamaduni katika lugha lengwa ndiyo ilikuwa njia kuu ya kudhihirika kwa changamaoto katika kuzihawilisha dhana hizi. Kwa kuzingatia lengo letu hili la tatu, changamoto kuu iliyodhihirika katika uhawilishaji wa masuala mahususi ya kitamaduni ni kutokuwepo kwa istilahi katika lugha lengwa za kurejelea dhana mbalimbali zilizopo katika matini chanzi. Changamoto hii inatokana na ukweli kuwa, kwa sababu ya tofauti kati ya lugha ya Kiingereza na Kiswahili, kuna dhana ambazo ni mahususi katika lugha ya Kiingereza kwani lugha ya Kiswahili inakosa istilahi za kuzirejelea. Kwa mfano ubainishaji wa kijinsia ambao unadhihirika wazi katika matini chanzi lakini urejeleaji huo haujitokezi katika matini lengwa. Changamoto nyingine iliyodhihirika katika uhawilishaji wa dhana hizi mahususi za kitamaduni ni pale ambapo mtafsiri anajipata kati ya mbeko zinazoshawishi tafsiri kufanywa kwa namna fulani na istilahi inayofaa kutumika kuhawilisha dhana husika. Changamoto hii pia ilichangia katika kutojitokeza kwa dhana mahususi za kitamaduni katika matini lengwa inapolinganishwa na matini chanzi.

## 5.2 Mapendekezo

Utafiti wetu ulikitwa kwenye kitabu cha *Song of Songs* na tafsiri yake katika lugha ya Kiswahili; *Wimbo Ulio Bora*. Hivi ni kumaanisha kuwa kuna jumla ya vitabu sitini na sita kwenye agano jipya na agano la kale ambavyo havikuhusishwa katika utafiti wetu. Kwa sababu upeo na mipaka ya kazi yetu ilitufunga kwenye kitabu hiki peke yake, kuna uhitaji wa utafiti kufanywa kuhusu vitabu vingine vinavyosalia ili kutathmini masuala ya kitafsiri yanayoibuka kutokana na tafsiri ya vitabu hivyo katika lugha ya Kiswahili kwa kuvilinganisha na vitabu hivyo katika lugha ya Kiingereza.

Isitoshe, utafiti wetu ulitubana kuchunguza tu tamathali tatu ambazo ni tashbihi, tashihisi na sitiari. Jambo hili linaacha pengo ambalo linastahili kufanyiwa utafiti ambalo ni kuchunguza

tamathali nyingine ambazo zimedhihirika katika kitabu husika (*Wimbo Ulio Bora*) kama vile kinaya kwa kukilinanisha na matini asilia; *Song of Songs*. Kwa hivyo, pana haja ya kufanyia tamathali hizi nyingine utafiti linganishi ili kutathmini jinsi ambavyo masuala ya kitafsiri yanavyojitokeza katika uhawilishaji wa tamathali hizi kutoka lugha ya Kiingereza hadi ya Kiswahili kwa kurejelea vitabu husika.

Kando na haya, utafiti wetu ulikitwa kwenye uchunguzi wa tamathali pekee, jambo ambalo linaacha pengo la kuzibwa. Kwa mfano, uhawilishaji wa maudhui pamoja na uhawilishaji wa mandhari mbalimbali katika vitabu husika pia unastahili kutafitiwa ili kubaini masuala ya kitafsiri yanayoibuka kutokana na uhawilishaji huu. Ni maoni yetu kuwa kwa kufanya hivi, tafiti hizi zitaweza kuibua mijadala muhimu ya kitafsiri ambayo itatoa michango ya thamani katika uwanja mzima wa tafsiri.

## MAREJELEO

- Aissi, L. (1987) *An Analytical Study of the Process of Translation*. Tasnifu ya Uzamifu: Chuo Kikuu cha Salford.
- Ali, C.W (1981) *The Problems of Translating From English into Swahili. As exemplified by V.O.K. news items*. Tansifu ya Uzamili: Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Aixelá, F. (1996). *Culture-specific items in translation*. In R. Álvarez & M. C. Vidal (Eds.), *Translation, power, subversion* (pp. 52–77). Clevedon: Multilingual Matters.
- Baker, M. (1992) *In Other Words ; A Coursebook on Translation*. USA and Canada : Routledge.
- Bassnett, S. (2002). *Translation studies*, (3rd ed.). London: Routledge.
- Casagrande, J. B. (1954). *The ends of translation*. *International Journal of American Linguistics*, 20 (4), 335-340.
- Chama cha Biblia Kenya na cha Tanzania .*Bibilia Takatifu*: Nairobi na Dodoma.
- Chebet, D. J (2014) *Encountering the Female Voice in the Song of Songs: Reading the Song of Songs for the Dignity of Kenyan Women*. Tasnifu ya Uzamifu: Chuo Kikuu cha Stellenbosch.
- Elewa, A. (2014) Features of translating religious texts. *Journal of Translation*, 10(1), 25-33.
- \_\_\_\_\_ (2011) *The grammar of translation: A five-level course in the theory and practice of translation*. Cairo: New Vision Press.
- Even-Zohar, I. (2000) The Position of Translated Literature within the Literary Polysystem. *The Translation Studies Reader*. Ed. Lawrence Venuti. London: Routledge: 192–197.



- Gambier, Y. (2004). *Doubts and Directions in Translation Studies*. The Netherlands: John Benjamins.
- Gentzler, E. (1993) *Contemporary Translation Theories*, London: Routledge.
- \_\_\_\_\_ (2001) *Contemporary Translation Theories* (Juzuu la pili) Clevedon: Multilingual Matters Limited.
- Kothari C.R. (1985) *Reserch Methodology Methods and Techniques*. New Delhi: Wiley Easton Limited.
- Larson, L. M (1984) *Meaning-Based Translation. A Guide to Cross Language Equivalence*. Newyork: University Press of America.
- Lefevere, A. (1975) *Translating Poetry*. Amsterdam: Van Gorcun Assen.
- Lewis, R. (2006) *When Cultures Collide: Leading across Cultures*. Boston and London: Nicolas Brealey International.
- \_\_\_\_\_ (1992) *Translation, Rewriting and the Manipulation of Literary Fame*. London: Routledge.
- \_\_\_\_\_ (2002). *Translation, history, culture: A source book*. London: Routledge.
- Lyu, S. (2001) *The Considerations of Interpretation Through the Function of Imagery in the Song of Songs and Its Application to the Current Believing Community*. Tasnifu ya Uzamifu: Chuo Kikuu cha Liberty.
- Malmkjær, K. (2015) Key Cultural Texts in Translation. <http://translatingcultures.org.uk>.
- Mgullu, S. (2014) *Mtalaa wa Isimu*. Nairobi: Longhorn Publishers.
- Mule, K. (2002) *Translation, Mistranslation, and Cultural Theory: African Inflections, Challenges, and Prospects*. *Metamorphoses*, spring 2002 .10.1 Academic

- Munday, J. (2001). *Introducing Translation Studies: Theories and Application*. London: Routledge.
- \_\_\_\_\_ (2007) *Style and Ideology in Translation. Latin American Writing in English*. New York: Routledge.
- Mutie, E. K (1997) *Sanaa katika Tafisiri: Matatizo na Athari Zake*. Tasnifu ya Uzamili: Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Mwakio, L.W (2016) *Matumizi ya Tashbihi, sitiari na taashira katika damu nyeusi nahadithi nyingine*.Tasnifu ya Uzamili: Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Mweri (2010) *Utangulizi wa Isimu*. Nairobi: KLB.
- Namulungu, R.I.S (1997) *Ukiushi katika Tafisiri: Uhakiki wa Shamba la Wanyama*. Tasnifu ya Uzamili: Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Newmark, P (1982) *Approaches to Translation*, Oxford: Pergamon Press.
- \_\_\_\_\_ (1988) *A Textbook of Translation*. United Kingdom: Prentice Hall International Ltd.
- \_\_\_\_\_ *Translation and Culture*.In *Meaning in Translation*. Ed. B. Lewandowska-Tomaszczyk. Frankfurt: Peter Long GmbH, 171-182.
- Nord, C. (1997) *Translating as a Purposeful Activity: Functionalist Approaches Explained*. Manchester: St. Jerome.
- Ntarandwi, M. (2004) *Uhakiki wa Kazi za Fasihi*. Tasnifu ya Uzamifu: Augustana College, Rock Island.
- Nzyoka S. (2014) *Tathmini ya Tafisiri na Mikakati ya Kutafisiri Tamathali za Usemi katika Tamthilia ya antigonli*. Tasnifu ya Uzamili: Chuo Kikuu cha Kenyatta.

- Omondi, F.O (1997) *Dhana na Matatizo ya Tafsiri: Tathmini ya Risasi Zianzapu Kuchanua*. Tansifu ya Uzamili: Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Omuya, R.A (2017) *Usimilishwaji wa Biblia kama Fasihi ya Watoto kwa Kutumia Hadithi Teulekutoka kwa Biblia ya Watoto*. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta.
- Raja, S.A (2016) *Translating Religious Terms and Culture in „The Sealed Nectar“: A Model for Quality Assessment*. Tasnifu ya Uzamifu: Chuo Kikuu ch Leeds.
- Robinson, D. (1997) *Western translation theory: From Herodotus to Nietzsche*.
- Ryanga, C.W. (1985) *Vitabu Vya Kutafsiriwa na Fasihi ya Kiswahili*. Katika Tuki Vol 52. Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam.
- Saberi, D. (2015) *Translators' Strategies for the Translation of Cultural Markers from English into Persian in a Literary Text*. Tasnifu ya Uzamili: Chuo Kikuu cha Putra Malasya.
- Sewell, W. (2009) *The Concept of Culture*. Washington University: St. Louis Press.
- Shiroko, E.M (2014) *Challenges of Translating Symbolism, Wordplay and Repetition in Plays: A Case Study of S.A Mohamed's 'Amezidi' and its Translation 'He's Far Too Much' By Sarah Weschler and Niwaeli Kimambo*. Tasnifu ya Uzamili: Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Swaleh, A. (2011) *A Criteria of Mapping and Construction of Gender Identity and Authority in Selected Kiswahili Novels*. Tasnifu ya Uzamifu: Chuo Kikuu cha of Nairobi.
- The Holy Bible* (King James Version) (1798). Nashville Mexico City: Thomas Nelson.
- Venuti, L. (1992). *Rethinking translation: Discourse, subjectivity, ideology*. London:

Routledge.

\_\_\_\_\_ (1995) *The translators invisibility: A History of Translation*. New York: Routledge.

\_\_\_\_\_ (2001) *Strategies of Translation: Routledge Encyclopedia of Translation Studies*. Ed. London and New York: Routledge.

\_\_\_\_\_ (2002) *On The Different Methods of Translating*. The Translation Studies reader.

\_\_\_\_\_ (2004) *The translation studies reader*. London and New York: Taylor & Francis  
Routledge.

Waihia, G. (2011) *Sarufi Fafanuzi ya Kiswahili*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Wamitila, K.W. (2003) *Kamusi ya Fasihi, Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publishers.

\_\_\_\_\_ (2008) *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Vide-muwa  
Publishers. Nairobi.

Wilss, W. (1982) *The Science of Translation: Problems and Methods*. Tübingen: Gunter  
Narr.

Yana, S.M (2018) *Analyzing Translation of Metaphor: A Case Study*. ISSN 2573-6434  
(Print) ISSN 2573-6426 (Online) Vol. 2, No. 1, 2018  
[www.scholink.org/ojs/index.php/sll](http://www.scholink.org/ojs/index.php/sll).

Zaja O. (1986) *Fasihi Tafsiri katika Ukuzaji wa Fasihi ya Kiswahili*. Tasnifu ya Uzamili:  
Chuo Kikuu cha Nairobi.

\_\_\_\_\_ (2006) *Siting Text, Culture, Context and Pedagogy in Literary Translation*. Tasnifu ya  
Uzamifu: Chuo Kikuu cha Kenyatta.